**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 9 Julai, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuweka mezani Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kuweka mezani Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii, kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mezani Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo, kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 167

**Tatizo la Barabara Kata ya Makuburi**

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA (k.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la barabara ya *River Side* – Makoka – Kibangu – Kimara Korogwe kata ya Makuburi limekuwa sugu na kwa kuwa tatizo hilo limewahi kutolewa taarifa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na kutolewa ahadi kwamba ingefanyiwa matengenezo lakini ahadi hiyo haikuweza kutekelezwa kwa sababu haikuwekwa kwenye makisio ya Bajeti ya mwaka 2006/2007:-

(a) Je, Serikali ina mpango wowote wa kuitengeneza barabara hiyo katika mwaka wa fedha 2007/2008?

(b) Kwa kuwa, barabara hiyo inapita maeneo yenye udongo wa mfinyanzi ambao husababisha utelezi, na vilevile haina mifereji ya kutolea maji wakati wa mvua hivyo kuwa kero kwa wananchi wa maeneo hayo, Je, Serikali ina mipango gani ya muda mfupi na mrefu ya kuitengeneza barabara hiyo kwa kuichonga, kuweka mifereji na makalvati, ili iweze kupitika nyakati zote bila matatizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu :-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalumu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imekuwa ikizifanyia matengenezo barabara zilizopo kwenye Kata ya Makuburi kila hali ya kifedha inaporuhusu ili kuzifanya zipitike katika kipindi kirefu cha mwaka.

Kwa mara ya mwisho Manispaa ilizifanyia matengenezo ya kuzichonga kwa greda barabara za Kata hiyo zenye urefu wa jumla ya Kilomita 11.5 mwezi Julai, 2006. Barabara ya Makoka – Kibangu ni mojawapo kati ya barabara hizo. Kazi yote hii iliigharimu Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni jumla ya Sh.3,793,500/=. Barabara zilizofanyiwa matengenezo ni *External* – JWTZ Mabibo (Km 2.3), JWTZ Mabibo – Mandela *Road* kupitia SAS (Km 1.7), Makoka – Kibangu (Km 3.7), Makoka – Uwanjani (Km 1.3) na *International School – River Side* (Km 1.5). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imetenga Sh.10,000,000/= kwa kila kata kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara zake muhimu. Kutokana na umuhimu wa barabara hii, inategemewa kuwa Kata za Makuburi na Kimara zitapewa kipaumbele kwa barabara hii kwa vile inapita kwenye kata zote mbili.

(b) Mheshimiwa Spika, Barabara hii ilifanyiwa ukaguzi na kuainisha gharama za matengenezo ya muda mfupi na ya muda mrefu. Gharama za matengenezo ya muda mfupi zimekadiriwa kuwa ni Sh. 78,815,000/= ili kuifanya ipitike na zile na matengenezo ya muda mrefu zimekadiriwa kuwa ni Sh. 677,008,000/=.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni haikuweza kuweka mradi huu kwenye mpango wa matengenezo kwa mwaka 2007/2008. Hata hivyo Serikali ina nia nzuri ya kufanyia matengenezo barabara zake, tatizo ni ufinyu wa Bajeti.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA :** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninamshukuru na Waziri kwa majibu yake, pamoja na hayo naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ningependa Waziri sasa awahakikishie wananchi wa Kata ya Makuburi ni lini kazi itaanza hasa ikizingatiwa kwamba barabara kutokana na hali ya udongo wa eneo lile iko kwenye hali mbaya na sasa hivi haipitiki kwa kiwango kikubwa.

Je, ni lini sasa baada ya milioni hizo kumi kutengwa kazi itaanza na wananchi watashirikishwa vipi katika kazi hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelekeza kwamba njia zote zinazowezekana zitafutwe kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam na kwa kuwa eneo la Kimara hasa Kimara - Korogwe ni eneo linalokumbwa sana na msongamano huu na kwa kuwa barabara hii ya Makoko – Makuburi – *River Side* inaweza kupunguza sana msongamano huu.

Je, Waziri atakubaliana kwamba sasa kuna haja ya kuongeza fedha angalau hata kama siyo hizo 600 zinazokamilisha basi angalau zifike nusu ili barabara hii iweze kupitika na kupunguza msongamano katika eneo la Kimara ?

**SPIKA :** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, inaelekea huyu Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, anavielewa sana vichoro vya Makuburi - Kimara. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kama ifuatavyo. Katika swali lake la kwanza kama mnavyofahamu kwamba mwaka huu kulikuwa na mvua kubwa sana barabara zisingeweza kutengenezwa kwa kipindi kile cha mvua, nina uhakika baada ya mvua hizi barabara hizi zitaanza kutengenezwa kwa hela zilizotengwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, ni kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu ameziagiza Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam kuhakikisha kwamba barabara zinatengenezwa ili kupunguza msongamano katikati ya Jiji la Dar es Salaam. Barabara hizo zitakazotengenezwa ni zile ambazo zinaingia moja kwa moja katika Jiji la Dar es Salaam na zitatengenezwa kwa awamu siyo zote zitatengenezwa kwa wakati mmoja.

Kwa hiyo ninamwomba Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa avute subira barabara hizi zitakuwa zinatengenezwa kulingana na kipaumbele.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu ningependa kuongeza majibu ya ziada ya swali la Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Kinondoni ni mojawapo ya Manispaa au Halmashauri za Nchi nzima ambao tumenunua greda letu wenyewe, tumenunua matipa matano na vifaa mbalimbali vya kutengeneza barabara. Kwa bahati mbaya magreda yetu yamekuwa yakiharibika hapa na pale lakini tumekwisha yapatia ufumbuzi na tumekarabati na sasa hivi milioni 10 zimetengwa kila kata kwa hakika zitatosha. Lakini manispaa imeweka mkakati madhubuti kabisa wa kutumia greda yetu na matipa yetu angalau kukarabati hizi barabara ili ziweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuongeza pia Madiwani wa Makuburi pamoja na Diwani wa Kimara ni madhubuti sana, Mheshimiwa Mahmudu Mlingo ameleta suala hili mpaka kwenye chama na tumeamua kwamba tutatia mkazo mkubwa sana wa barabara za Kimara na Makuburi. Ninaomba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na sisi ili tuweze kutembelea na kusaidiana kuhakikisha kwamba barabara hizo zinapitika. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nadhani Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, umeisikia hiyo ofa ya kufuatana na Mheshimiwa Rita Mlaki, huko Makuburi?

Na. 168

**Gari la Wagonjwa na Madaktari – Kituo cha Afya Kharumwa**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza :-

Kwa kuwa, Kituo cha Afya Kharumwa hulaza wagonjwa Wilayani Geita na kinahudumia pia wagonjwa kutoka Wilaya ya Shinyanga Vijijini na Kahama; na kwa kuwa kituo hicho kiko mbali sana na hospitali za Geita na Sengerema:-

(a) Je, ni lini Serikali itakipatia gari la wagonjwa kituo hicho ili kunusuru maisha ya wagonjwa hususan akina mama wajawazito na watoto wanaopata rufaa kwenda hospitali za Wilaya na Mkoa?

(b) Je, ni lini Serikali itapewa Madaktari, Waganga, Wakunga na Wauguzi wa kutosha katika kituo hicho?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu :-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Philipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale wanaohudumiwa na kituo cha afya cha Kharumwa wanapata shida kubwa kutokana na kukosekana kwa gari la wagonjwa. Pia nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, umbali uliopo kati ya kituo hicho cha Afya na Hospitali ya Wilaya ni mrefu hasa wakati wakipata rufaa.

Ili kukiwezesha Kituo cha Afya cha Kharumwa kutoa huduma bora kwa wananchi, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imetenga fedha katika Bajeti ya mwaka 2007/2008, kwa ajili ya ununuzi wa gari la kuhudumia wagonjwa katika kituo hicho.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu fika umuhimu wa kuwepo madaktari, waganga, wakunga na wauguzi wa kutosha katika vituo vya afya kikiwemo Kituo cha Afya cha Kharumwa ili kutoa huduma inayotosheleza kwa wananchi. Serikali inaendelea na mpango wa kuongeza madaktari, waganga, wakunga na wauguzi katika hospitali pamoja na Vituo vya Afya na Zahanati kwa awamu kwa kadiri wanavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 Halmashauri ya Wilaya ya Geita imepokea jumla ya watumishi wapya 18 wa kada mbalimbali wa Idara ya Afya. Watumishi watatu kati ya hawa (Afisa tabibu (1), na wauguzi (2) walipangiwa kufanya kazi katika Kituo cha Afya cha Kharumwa.

Kwa sasa Kituo cha Afya cha Kharumwa kina jumla ya watumishi 18 wa kada mbalimbali kama ifuatavyo:- Daktari (1), *Clinical officers* (2), wauguzi wakunga (4), *Pharmaceutical Assistant (2), Laboratory assistants* (2) *Health Officer* (1) na *Medical Attendants (7).* Hii ni sawa na asilimia (62%) ya mahitaji yake kwani kwa mujibu wa ikamu Kituo cha Afya kinatakiwa kuwa na jumla ya watumishi 29 wa kada mbalimbali. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Geita inapaswa kuweka mazingira ya kuvutia zikiwemo nyumba za watumishi katika Kituo cha Afya cha Kharumwa ili watumishi watakaoajiriwa waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niuliza swali ambalo siyo dogo sana la nyongeza. Lakini kabla sijauliza napenda nichukue nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu niipongeze sana Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa kuweza kutenga pesa kununua gari la wagonjwa kwa ajili ya kituo cha Kharumwa. (*Makofi*)

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kuwapo umuhimu wa huduma mbalimbali kama watumishi katika hospitali hiyo na kwa kuwa ni kweli wananchi wengi sana wa Wilaya ya Geita, Kahama, Sengerema wanahudumiwa na kituo hicho.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuleta mashine au vifaa vya kupimia kama vile *x-ray*, *ultra sound*, vifaa vya kupima sukari, *ECO*, *ECG* katika kituo hicho ili kuhudumia wananchi hao ?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kumjibu Mheshimiwa James Musalika, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, vifaa alivyovitaji vinahitaji utaalamu mkubwa, kupeleka vifaa inawezekana lakini kama hakuna wataalam vitakaa bila kutumika. Hivi vifaa vimeorodheshwa kufuatana na uwezo wa kuvitumia na sasa hivi vyote alivyovitaja tunapeleka kwenye Hospitali za Wilaya na katika Hospitali ya Wilayani kwake hivi vifaa vipo. Kwa hiyo, mpaka hapo tutakapokuwa na wataalam wa kutosha kuwapeleka kwenye Vituo vya Afya na hivyo vifaa vile vile vitapelekwa huko. (*Makofi*)

**MHE. ERNEST G. MABINA :** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Geita ina watu zaidi ya laki nane na katika huduma za *ambulance* au gari la wagonjwa hakuna katika Wilaya ya Geita na inasababisha wananchi wengi kutibiwa kwa waganga wa kienyeji.

Je, Serikali inasemaje angalau katika Wilaya ya Geita ipate gari la wagonjwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Hata lingepatikana gari kama mna tabia ya kwenda kwa waganga wa kienyeji litatumika kwenda huko huko, tunahamia Wizara ya Nishati na Madini. (*Kicheko*)

Na. 169

**Uimarishaji wa Sekta ya Madini**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza :-

Kwa kuwa katika miaka ya hivi karibuni Sekta ya Madini imeendelea kukua kwa kasi lakini mchango wake katika pato la Taifa ni mdogo na kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Nne imekusudia kuongeza kiwango cha madini yanayochimbwa na kusafirisha nje kwa mauzo :-

(a) Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wadogo wanatoa mchango unaostahili katika pato la Taifa kama ilivyo kwa wachimbaji wakubwa?

(b) Je, Serikali inawasaidia vipi wachimbaji wadogo wadogo wa madini waliotapakaa kwenye maeneo mbalimbali ya Kahama, hususan walioko katika eneo la Mwaboko, Kata ya Idahim katika kuboresha maarifa yao katika uchimbaji madini?

(c) Je, kuna kampuni ngapi za utafiti wa madini ya dhahabu katika Wilaya ya Kahama na ni muda gani kampuni hizo zimekuwa zikifanya utafiti huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu :-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali Mheshimiwa James Daud Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a), (b) na (c), naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa mchango unaotolewa na wachimbaji wadogo wa madini katika uchumi wa Taifa. Mchango huo ni pamoja a ugunduzi wa maeneo yenye madini, uzalishaji wa madini na utoaji wa ajira na mapato kwa wakazi wa vijijini. Hata hivyo, uchimbaji mdogo wa madini hujatoa mchango unaotarajiwa kwenye uchumi kutokana na changamoto mbalimbali zinazoikabili ikiwa ni pamoja na teknolojia duni ukosefu wa mitaji na ukosefu wa masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Daud Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa uchimbaji mdogo unaotoa mchango unaostahili katika pato la Taifa, baadhi ya mikakati iliyowekwa na Serikali ni ifuatavyo:-

(1) Kubadili na kuboresha uchimbaji mdogo ili ufanyike kwa mpangilio mzuri na wa kisasa;

(2) Kuhamasisha watu na kampuni binafsi kutengeneza, kusambaza na kuuza zana na vifaa vya uchimbaji madini hapa nchini;

(3) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini;

(4) Kutenga maeneo yaliyo wazi kwa ajili ya uchimbaji mdogo;

(5) Kuunda kitengo maalumu katika Idara ya Madini cha kusimamia maendeleo ya shughuli za uchimbaji mdogo wa madini;

(6) Kuendeleza ubia bain aya wachimbaji wadogo na wakubwa ili kuwezesha uhawilishaji wa teknolojia na kuongeza kwa kiasi kikubwa kiwango cha uchimbaji wa madini; na

(7) Kuanzisha mifuko maalumu ya mitaji kwa ajili ya kuhudumia wachimbaji wadogo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali katika sehemu (a), Serikali kupitia wataalamu wa madini waliopo ofisi zetu za kanda ikiwemo ofisi yenu ya madini Kahama inatoa huduma za ushauri wa kitaalamu katika uchimbaji, uchenjuaji na biashara

ya madini kwa wachimbaji wadogo nchini. Elimu hii ni muhimu katika kuboresha maarifa yao katika uchimbaji wa madini.

Meshimiwa Spika, natoa wito kwa wachimbaji wadogo wanaoendesha shughuli zao Wilayani Kahama kuitumia vizuri Ofisi ya Madini Kahama katika kuboresha shughuli zao za uchimbaji na kuinua kipato chao na Taifa kwa ujumla. Aidha, natoa wito kwa wachimbaji wadogo wote nchini waendeshe shughuli zao kwa kufuata sheria na kanuni za madini ikiwemo kuuza madini yao kwa wanunuzi wanaotambulika kisheria na si vinginevyo.

(c) Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kahama kuna kampuni 13 zenye leseni za utafutaji mkubwa wa madini (*prospecting license*). Chini ya Sheria ya Madini ya mwaka 1998, leseni za utafutaji wa madini zina uhai wa miaka mitatu ya awali na huweza kuhuishwa kwa vipindi vingine viwili vya miaka miwili miwili. Jumla ya kipindi hicho kwa pamoja ni miaka saba. Kazi ya utafutaji madini inaweza kuchukua muda mrefu zaidi kutengeneza mafanikio ya hatua moja hadi nyingine.

Mheshimiwa Spika, moja ya kampuni zinazofanya utafutaji wa madini katika maeneo ya Wilaya ya Kahama ni kampuni ya *Barrick*. Kampuni hii imefanikiwa kugundua mashapo na pia inategemea kuanzisha mgodi wa Buzwagi kwa ajili ya uchimbaji wa dhahabu. Haya ni mafanikio yanayotokana na utafiti wa madini katika Wilaya ya Kahama.

**MHE. JAMES D. LEMBELI :** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa hivi sasa mchakato wa mgodi mpya wa dhahabu wa Buzwagi ulioko nje kidogo ya mji wa Kahama unaendelea ikiwa pamoja na zoezi la kulipa fidia wananchi na wachimbaji wadogo wadogo waliokuwa wakifanya kazi katika eneo hilo, zoezi la kulipa wananchi linaonekana kuendelea vizuri lakini zoezi la kuwalipa wachimbaji wadogo wadogo waliokuwa wakifanya kazi katika eneo hilo hasa eneo la Mwime, Mwendakulima na Chapulwa linaelekea kuwa na matatizo makubwa kiasi kwamba Serikali inatumia nguvu.

Je, Waziri anaweza kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba wananchi hao wachimbaji wadogo wadogo hawanyanyaswi na walipwe pesa zao kabla ya mashimo yao kufukiwa?

(c) Kwa kuwa utafiti wa madini katika eneo la Mwabomba katika Kata Idahina umeendelea kwa muda mrefu hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wa eneo hilo ambao walikuwa wakitumia maeneo hayo kwa ajili ya kilimo na ufugaji.

Je, Serikali inaweza kuwahakikishia wananchi wa kata hii kwamba watafiti hao kama hawajagundua hayo madini wanaondoka? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI :** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa James Lembeli, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa James Lembeli, kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia hatma ya wananchi wake katika jimbo lake kutokana na matarajio ya kuanzishwa mgodi wa Buzwagi katika eneo la jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza naomba kumhakikishia Mheshimiwa James Lembeli kwamba wachimbaji wadogo watapata haki zao kama inatarajiwa lakini pia kama alivyokiri mwenyewe kwamba zoezi la kuwafidia wananchi linaendelea vizuri na kwa kweli katika hili ni pamoja na wachimbaji wadogo, fedha kadhaa imeshalipwa na tunaendelea vizuri na tunaomba tu Mheshimiwa James Lembeli tuzidi kushirikiana naye ashirikiane na ofisi yetu na Wizara yetu kwa ujumla ili kuhakikisha kwamba wale wananchi wachache ambao bado hawajachukua na hawajaanza kupokea fidia zao tuwashawishi waanze kupokea.

Mheshimiwa Spika, la pili, utafutaji kama tulivyoeleza kwenye jibu la msingi unafuata sheria, naomba nizidi kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini kwamba Serikali haitaruhusu utafutaji au uchimbaji ufanyike kinyume cha sheria kwa hiyo tunazidi kuwahakikishia wananchi wa Jimbo la Kahama na hasa maeneo ya Mwabomba pamoja na Idahina kwamba watafutaji wa madini walioko pale wanafuata sheria na Serikali inafuatilia kuhakikisha hawakiuki sheria zilizopo ambazo zinawezesha kufanya hizo shughuli.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA :** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali dogo la nyongeza. Mheshimiwa Waziri katika jibu lake la msingi amesema kwamba wachimbaji wadogo wajipange ili waweze kupewa maeneo lakini tatizo kubwa la wachimbaji wadogo ni kufikiriwa kupewa maeneo, mfano wachimbaji wa Matabe wameshapeleka maombi yao muda mrefu Wizara ya Nishati na Madini na baadaye wakafukuzwa wakatolewa sehemu ambayo nafikiri walikuwa wanataka kupewa na Serikali.

Je, kwa kuwa nia hiyo ipo ya kuwasaidia ni lini sasa watapewa kibari ili waweze kuendelea kufanya kazi kusudi waweze kujiajiri na waondokane na tabu waliyonayo sasa hivi. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI :** Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, eneo la Matabe ni Hifadhi ya Taifa na kuna utaratibu ambao unalinda lile eneo la Hifadhi ya Taifa kabla halijaruhusiwa kufanya shughuli yoyote na utaratibu wa kisheria ni kwamba Wizara yangu inabidi iombe Wizara ya Maliasili, jambo hilo tumeshalifanya sasa taratibu zinafuatwa ikiwa wataona vigezo ambavyo tumeomba sisi hilo eneo watupe kusudi tuweze kuwapatia wachimbaji wadogo wadogo.

Lakini na wenyewe maliasili wana vigezo ambavyo wanavifuata wakiridhika kwamba linaweza kutolewa watatuarifu na wakishatuarifu ndio tumwarifu Mheshimiwa

Mbunge na wakazi wa eneo hilo ili kuunda kamati ya kuweza kugawa eneo kwa wachimbaji wadogo wadogo.

Na. 170

**Ukamilishaji wa Miradi ya Umeme**

**MHE. CLEMENCE BEATUS LYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwongozo wa mpango wa Bajeti ya mwaka 2007/2008 umesisitiza kutoa kipaumbele cha kuendeleza utekelezaji wa miradi iliyokwishaanza ili kukuza uchumi na kuboresha maisha ya Watanzania; na kwa kuwa, miradi ya kupeleka umeme katika vijiji vya Kibaoni, Muungano na Mkono wa Mara katika Kata ya Mabwerebwere, vijiji vya Kivugu, Msanze Sekondari na Mkwatani vilivyo jirani na Wilaya ya Kilosa inakidhi vigezo vilivyoelekezwa na Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwani iliahirishwa miaka mitatu (3) iliyopita baada ya *survey* kukamilika:-

Je, Serikali itakuwa tayari kutekeleza miradi hiyo katika Bajeti ya mwaka huu, 2007/2008 ambayo katika baadhi ya vijiji wananchi waliagizwa na *TANESCO* wang'oe Minazi, Miembe, Mikorosho na wakafanya hivyo na nguzo za umeme zilisimikwa lakini mpaka leo umeme haujapelekwa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mbunge wa Mikumi, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kijiji cha Kondoa – Kilosa, ujenzi wa laini kubwa ya msongo wa kilovolti 33 yenye urefu wa kilometa 0.5 ulikwishamalizika. Kazi iliyobakia ambayo ni ujenzi wa transfoma ya ukubwa wa *50kVA, 33/0.4kV* na laini ndogo ya msongo wa kiloVolti 0.4 yenye jumla ya urefu wa kilomita 1. kazi hii haijafanyika kwa sababu ya ukosefu wa fedha.Vijiji vya Mkwatani, Mkono wa Mara, Kivungu, Sekondari ya Masanze, na Kibaoni ni maeneo yaliyokwishafanyiwa upembuzi yakinifu. gharama za kusambaza umeme kwenye vijiji na maeneo hayo ni shilingi 82,236,026.00. Kijiji cha Muungano bado hakifanyiwa upembuzi yakinifu. wizara yangu imeiagiza *TANESCO* kufanya tathmini hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Bajeti ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini ni finyu. Hata hivyo, uanzishwaji wa Uwakala wa Nishati Vijijini (*REA*) utasukuma utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wake wawe wavumilivu wakati Serikali ikiendelea na mchakato wa kuendelea na mipango wa *REA*.

**MHE. CLEMENCE BEATUS LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa wananchi wamepata hasara katika baadhi ya vijiji kwa kung'oa mikorosho, miembe na minazi kwa kipindi kirefu na wamekosa mazao na kipato chochote ambacho wangekitumia kutokana na mazao hayo na zaidi ya yote wamekosa hata umeme. Kweli Serikali haiwaonei huruma wananchi hawa angalau katika maeneo ambayo nguzo zimesimama zikapelekewa umeme ili kuwatia moyo wale wanaovuta subira?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba nijibu swali la Mheshimiwa Clemence Lyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, narudia kusisitiza tena hapa kwamba kwa niaba ya Waziri wangu kwamba Serikali inawaonea huruma sana wananchi ambao maeneo yao yalifanyiwa upembuzi yakinifu na kama nilivyosema baadhi ya maeneo yameshafyekwa mazao ya wananchi na mali zao zikaathirika.

Lakini kama nilivyosema nia njema ya Serikali kwa kiasi fulani imekwazwa na ufinyu wa Bajeti, lakini tunatambua kwamba mfuko wa kusambaza huduma ya umeme vijijini utakapoanza tutahakikisha kwamba maeneo yote ambayo yamefanyiwa upembuzi yakinifu yakiwemo maeneo ya Mheshimiwa Mbunge, tutahakikisha kwamba yanahudumiwa kwa nafasi za awali kabisa.

**SPIKA:** Sasa ni zamu ya Wizara ya Usalama wa Raia swali linaulizwa Mheshimiwa Joyce Nhamanilo Machimu.

Na. 171

**Vitendo vya Uhalifu - Shinyanga na Mwanza**

**MHE. JOYCE NHAMANILO MACHIMU** aliuliza:-

Kwa kuwa, jambazi au mhalifu hatoi taarifa siku anapoamua kufanya uhalifu hasa ukataji mapanga na kuukatili uhai wa binadamu kwa maeneo ya Mikoa ya Shinyanga na Mwanza.

(a) Je, ni halali kwa Polisi kuwakamata na kuwaweka rumande viongozi wa vitongoji na vijiji badala ya mhalifu kwa sababu kwamba, mauaji yametokea kwenye eneo lake?

(b) Je, Serikali inathibitisha kuwa, kwa kuwaweka rumande viongozi hao ndiyo kutokomezwa kwa vitendo vya ukataji mapanga?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Nhamanilo Machimu, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Msingi za ukamataji au kuweka mtu mahabusu ni kwamba Polisi anaweza kumkamata au kumweka mtu Mahabusu pale tu ambapo ni muhimu kufanya hivyo na pale tu ambapo ana Mamlaka ya Kisheria kufanya hivyo. Aidha, sababu za ukamataji ni kumzuia mtu kutenda au kuendelea kutenda kosa la jinai au tendo lolote lililo kinyume na Sheria, kuwezesha kufanyika kwa upelelezi kuhusiana na tuhuma za kosa dhidi ya mtuhumiwa au kufanikisha zoezi la mtuhumiwa kufikishwa mbele ya Mahakama ili kujibu mashitaka yoyote yanayomkabili.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, kwa ruksa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Nhamanilo Machimu lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, si halali kuwakamata na kuwaweka rumande viongozi wa vijiji na vitongoji badala ya mhalifu kwa sababu kwamba mauaji yametokea kwenye eneo lake. Makosa ya mauaji kama yalivyo makosa mengine ya jinai, mara yanapotokea hushughulikiwa kwa kuzingatia misingi ya Sheria na taratibu za nchi. Hivyo, haitakiwi kimkamata na kumfikisha Mahakamani mtu yeyote pasipo kuwa na ushahidi wa kutosha wa kumwunganisha mtuhumiwa na shitaka husika.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaamini kuwa kwa kufuata misingi ya Sheria na kuendelea kuimarisha ulinzi ndiyo njia sahihi ya kutokomeza uhalifu nchini ikiwemo ukataji wa mapanga.

Mheshimiwa Spika, Serikali haitamvumilia mtu yeyote yule ambaye hatatekeleza wajibu wake kwa kufuata misingi ya Sheria na taratibu zilizowekwa na hasa kwa kuwabambikizia kesi wananchi wasiokuwa na hatia, hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa wananchi wote kwamba wanatakiwa kuheshimu na kuzingatia Sheria za nchi na waache tabia ya kujichukulia Sheria mikononi mwao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joyce Nhamanilo Machimu swali la nyongeza.

**MHE. JOYCE NHAMANILO MACHIMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba si halali kukamatwa viongozi hao. Je, Serikali haioni kwamba kuwakamata na kuwaweka rumande viongozi hao ni kuvunja haki zao?

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Wakuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Vituo vya Polisi na Wakuu Upelelezi katika maeneo yanayotokea matokeo kwa kuwa njia moja au nyingine wanahusika na usalama wa raia wa eneo hilo na wakati mwingine wanahusika katika kutoa ruhusa ya kukamatwa kwa viongozi hao?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA URAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruksa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joyce Nhamanilo Machimu, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba ukamataji unafuata taratibu za Sheria na siku zote Serikali yetu inaendelea kusimamia misingi ya Sheria hivyo kwa wale wanaokamatwa ni wale tu ambao watavunja utaratibu wa Sheria na pale inapoonekana mtu huyu hana kosa huachiwa mara moja.

Mheshimiwa Mbunge, kama una malalamiko yoyote yanaonekana kuna watu ambao wamekatwa kinyume cha taratibu naomba tuonane tuzungumze juu ya jambo hili ili tulipatie ufumbuzi wa kudumu. Hatuna nia yoyote ya kumpa mtu yoyote usumbufu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa kauli gani? Kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana sana Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mwanza na Tabora kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kushirikiana na Wizara yetu katika kuhakikisha usalama wa wananchi wetu kwenye maeneo haya.

Nyote mnajua kipindi cha nyuma mauaji yalikuwa makubwa sana katika maeneo hayo kwa jitihada za Wakuu wa Mikoa hawa kushirikiana na Wizara yetu na Askari Polisi wameweza kwa kiasi kikubwa sana kupunguza uhalifu huo.

Kwa hiyo, ni vema tukaendelea kuwapa moyo waendelee kufanya kazi hizo na wanafanya kazi zao kwa mujibu wa sheria na pale inapovunjwa sheria zipo hatua na taratibu zinazochukuliwa ili kwa mtu huyo kuomba haki yake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa swali la nyongeza.

**MHE. DR. WILBROD PETER SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kama kuna taarifa kuhusiana na waliokamatwa na kwamba yuko tayari kuzungumza, na kwa kuwa kule Kasulu kuna Mwenyekiti wa Kijiji amekamatwa kwa kuwa alitimiza jukumu lake la kwenda kuangalia mtu aliyeuawa na kwa kuwa huyu mtu mpaka leo yuko ndani na kesi

haijaenda Mahakamani na Waziri ameniambia linafanyiwa uchunguzi lakini ni zaidi ya mwaka mmoja ambayo ni kinyume na haki za binadamu.

Je, Waziri anatoa kauli gani kwa mtu wa aina hii.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema tunafanya kazi zetu kwa mujibu wa taratibu za Sheria na hatupo tayari kumwonea mtu yeyote na kama wakati mwingine kesi ina utata ni lazima uchunguzi wa kina ufanywe ili kuhakikisha Sheria ya kila mmoja inafuata mkondo wake na ila mmoja anapata haki yake kwa mujibu wa sheria. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER KABADI NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Ili kudhibiti uhalifu huu hususan wanaofanyiwa wanawake kwa kukatwa mapanga na ninafahamu wengi kwamba vituo vya Polisi viko maeneo machache sana kwenye Kata zetu. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuhakikisha kwamba tunaweka vituo vya Polisi kila Kata?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, kama ifuatavyo:

Kama nilivyosema katika majibu yangu mbalimbali yaliyotangulia napenda nisema yafuatayo:

Kwa sasa Jeshi la Polisi linafanya tathmini ya kina kujua mahitaji ya kipolisi ya ujenzi wa vituo vya Polisi nchi nzima na mara zoezi hili litakapokamilika nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge tutachukua kila jitihada kujenga vituo vya Polisi hatua kwa hatua kwa mujibu wa uwezo wa Serikali.

Pale ambapo kuna matatizo makubwa hivi sasa tumechukua hatua za ziada kuona kwamba tunakipa upembeleo maalum kuhakikisha maeneo hayo yanashughulikiwa mapema iwezekanavyo kuondoa tatizo la uhalifu katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Ni zamu sasa ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, swali linaulizwa na Mbunge wa Morogoro Mjini, Mheshimiwa Dr. Mzeru Omary Nibuka.

Na. 172

**Ulipaji wa Fidia ya Ardhi**

**MHE. DR. MZERU OMARY NIBUKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Vijiji Na. 5 ya mwaka huo huo hazijafutwa, hasa katika vipengele Na. 3 (g) na 3(g) (3) ambavyo vinasimamia ulipaji wa fidia na ufafanuzi uko wazi.

(a) Je, Serikali sasa inawaambia nini wananchi wa milima ya Uluguru ambao wamehamishwa bila kuzingatia utaratibu uliolezwa katika sheria husika (kwa vile hawakupata fidia) waakati wamepoteza mashamba na nyumba?

(b) Je, Serikali itawasaidiaje wananchi waliokumbwa na mkasa wa kuchukuliwa mashamba yao ili kuingizwa kwenye mradi wa kupima viwanja 4,000 kama vile Kata ya Kihonda na kwingineko katika Manispaa ya Morogoro?

(c) Je, Serikali itawachukulia hatua gani watendaji wanaovuruga Sheria wakati wa kutekeleza majukumu yao katika siku zijazo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Mzeru Omary Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, (a) mpaka sasa hakuna wananchi wanaoishi Milima ya Uluguru waliohamishwa na kupoteza mashamba na nyumba zao. Serikali ipo katika hatua ya kuwatambua wananchi hao na kuthamini mali zao. Utaratibu utakapokamilika, wananchi watahamishwa kwa mujibu wa Taratibu na Sheria.

Mheshimiwa Spika, (b) Manispaa ya Morogoro inatekeleza mradi wa kupima viwanja 4,000 katika Kata ya Kihonda kwenye maeneo yafuatayo:

- Kihonda Kilimanjaro;
- Likobe; na
- Msembe na Mgulu wa Ndege.

Maeneo haya yalikuwa ni mashamba ya Mkonge ambayo yalitaifishwa na Serikali mwaka 1967. Mnamo mwaka 1974 hadi mwishoni mwa miaka ya 80 maeneo haya yalitolewa kwa wananchi kwa muda kwa ajili ya kilimo cha nguvu kazi kwa masharti ya kutojenga nyumba wala kupanda mazao ya kudumu.

Lengo la Serikali lilikuwa ni kuhakikisha kuwa inaepuka gharama ya fidia wakati wa upanuzi wa mji utakapofika.

Mnamo mwaka 2004 Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilifuta Hati za Mashamba hayo ya Mkonge ili kupisha upangaji na upimaji wa viwanja katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 Kifungu 3 kifungu kidogo 1 (g) stahili ya fidia ni wale wanaomiliki ardhi chini ya Hati ya Kuandikishwa (*Granted Right of Occupancy*) na ardhi inayomilikiwa kilima yaani *Customer Right of Occupancy.* Kwa mujibu wa Sheria hiyo, fidia inayopaswa kulipwa ni pamoja na thamani ya ardhi tupu, maendelezo ya nyumba na mazao ya kudumu pale inapoathirika kufuatia maamuzi ya Serikali yanapofanywa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sheria hiyo, wananchi walioruhusiwa na Serikali kulima katika maeneo ya mashamba hayo ya Mkonge kwa muda, hawana stahili ya kulipwa fidia ya maendeleo yoyote kwa sababu ya wamiliki wa ardhi hiyo kimila wala miliki ya ardhi chini ya hati ya kuandikishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali huwachulia hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria na Taratibu watendaji wake pindi inapobainika kuwa wamekiuka Sheria katika utekelezaji wa majukumu yao.

**MHE. DR. MZERU OMARY NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini swali linakuja ni kwamba atakubaliana na mimi kwamba ninapozungumzia milima ya Uluguru ni pamoja na Morogoro Vijijini ambapo baadhi ya wananchi tayari wameshashuka mabondeni kwa kutekeleza amri ya Serikali?

Mashamba haya ya Sehemu za Kihonda ambayo wananchi wamenyang'anywa ni mashamba ambayo yaligawiwa na Serikali yenyewe kabla ya mwaka 1984 na mpaka ilipofika mwaka 2004 maana yake sasa hivi ni miaka 20. Sasa unapozungumzia kwanza katika kugawa hayo mashamba ni kwamba wananchi hawakuwa wameambiwa kwamba watakaa kwa muda gani. Kwa hiyo, wananchi walichukua hayo mashamba na wakalima mazao mbalimbali na Serikali ghafla ikaamu kuwanyang'anya mashamba hayo.

Je, Serikali haioni kwamba imefanya makosa kwa sababu haikutoa taarifa huko nyuma na kwa kuzingatia kwamba kulikuwa na mazao katika mashamba yao?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Mzeru Omary Nibuka Mbunge wa Morogoro Mjini kama ifuatavyo;

Ninamuomba sana Mheshimiwa Dr. Mzeru Omary Nibuka akubaliane na Serikali kwamba watu walioanza kushuka kutoka Milimani hawakutolewa na Serikali kinachofanyika sasa hivi katika maeneo ya Milima ya Uluguru ambayo ni vyanzo vya maji na pia kuna miteremko ambayo inaharibu mazingira kwa wale wanaolima kutokana na mmomonyoko hayo ndiyo tumeyalenga na ndiyo ambayo sasa wataalamu wetu wapo na wanashirikiana na kila ngazi kuanzia Kata mpaka Manispaa yenyewe kuhakikisha kwamba tunaokoa eneo hili.

Nitamuomba Mheshimiwa Dr. Mzeru Omary Nibuka kama tutakuwa tuna utata nitakuwa tayari kwa sababu Morogoro ni njiani kwenda Dar es Salaam tupite Morogoro tutazame hayo maeneo tuongee na wananchi na kutatua hayo matatizo.

Mheshimiwa Spika, la pili napenda kujibu kuwa mashamba tuliyoyachukua mwaka 2004 kama Serikali labda kwa ufafanuzi zaidi ni Madaraka Sisal Estate ambayo ilikuwa na Hati Miliki Namba 9,583 na ilikuwa ni ya miaka 99. Shamba lingine ni Mazimbu Sisal Estate ambalo pia lina Hati Miliki na tumezifuta zote. Hayo ndiyo tunapima viwanja 4,000 na tumewapa milioni 400,000 ili kuondoa matatizo haya.

Pili, kuondoa wasiwasi kwa wananchi wa Morogoro watakaohama kutoka milimani tumetafuta ekari 400 eneo la Kiegea katika Manispaa ya Morogoro ndipo tutakapopeleka hao wananchi tutakaowahamisha milimani.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Dr. Mzeru Omary Nibuka ambaye ni Mbunge wa pale atupe ushirikiano tuweze kuwasaidia wale wananchi na kunusuru milima ya Uluguru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana tunahamia sasa Wizara ya Miundombinu, swali lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini lakini badala yake nimearifiwa Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, ataliuliza hilo.

Na. 173

**Kiwanja cha Ndege Mtwara**

**MHE. RAYNALD ALFONS MROPE (k.n.y. MHE. MOHAMED SAID SINANI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kiwanja cha ndege cha Mtwara kinahudumia abiria wengi na kwamba, ndege za *Precision* huenda Mtwara kila siku wakati ndege za *ATC* hufanya safari zake Mtwara mara tatu katika juma moja na hapo hapo ndege ziendazo Msumbiji na Comoro hupitia uwanja huo wa Mtwara.

Je, ni lini Serikali itaweka mtambo wa kukagua mizigo *(screening)* na kujenga jengo la abiria kwani lililopo sasa ni bovu sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Said Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:-

Kufuatia tukio la kigaidi lijulikano kama *September 11* ambapo Ndege za abiria zilitekwa nyara na kurushwa hadi Mjini New York na kasha kubamizwa kwenye Jengo la Kituo cha Biashara cha Kimataifa yaani *World Trade Centre* Mjini New York, Marekani tarehe 11/9/2001.

Shirika la Kimataifa la usafiri wa anga yaani *ICAO* lilielekeza kuhusu kuimarishwa kwa ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege vyote duniani bila kujali ni vya kimataifa au kitaifa.

Hivyo, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ilianzisha utaratibu maalum kwa kutenga fedha za kugharamia miradi ya ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege nchini uitwao *Aviation Security Fund*. Fedha za mpango huu wa kuimarisha ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege nchini hutumika katika ujenzi wa uzio, kutoa mafunzo kwa maafisa usalama na wadau viwanjani, na kununua vifaa vya usalama kwa ajili ya ukaguzi wa maeneo ya viwanija na mitambo ya ukaguzi wa abiria na mizigo.

Kupitia mfuko huu wa fedha kiwanja cha ndege Mtwara kitapatiwa mtambo wa kukagua mizigo na abiria yaani (*screening*) katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa jengo jipya la abiria katika kiwanja cha ndege cha Mtwara, mamlaka ya viwanja vya ndege ina mpango wa muda mrefu wa kulijenga jengo hilo kwa awamu. Mamlaka itaanza kuandaa michoro katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2007/2008 na kwa kutegemea upatikanji wa fedha kuanza ujenzi katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2008/2009.

Pia mamlaka ya viwanja vya ndege inaendelea na matengenezo ya ukarabati wa jengo hilo ili kuliweka katika hali nzuri kwa matumizi ya abiria wanaotumia kiwanja hicho.

**MHE**. **RAYNALD ALFONS MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ningeomba kuuliza kwamba:

Moja, kwa kuwa ndege za *Precision* na *ATC* zinakwenda siku zote isipokuwa Alhamisi tu na kwa kuongezeka abiria kwa upande wa Mtwara. Je, Wizara haiwezi kushawishi mashirika haya yakapanga ratiba ya siku ya Alhamisi kwenda Mtwara?

Pili, kutokana na kugunduliwa kwa gesi *Mnazi Bay* na pia kuwepo kwa fununu za mafuta katika eneo la Mtwara hivi sasa kuna abiria wengi wanaotembelea Mtwara yaani abiria wa kitaifa na kimataifa. Je, Waziri haoni umuhimu wa kupandisha hadhi kiwanja cha Mtwara ili ndege ziweze kushuka usiku na mchana? Na sasa hivi Mtwara kuna umeme mwingi sana kwa hiyo hakuna wasiwasi usiku pale patakuwa panawaka kama mchana tu.

**SPIKA:** Majibu Waziri wa Miundombinu, ingawa nadhani kwa kawaida ndege hutua siyo kushuka, lakini ameomba zishuke. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, napenda nimjibu Mheshimiwa Mrope maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa ndege huwa zinatua, kushuka ni hatari sana kwa ndege.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza uwezekano wa ndege zetu *Air Tanzania* na *Precision* kuweza kuwa na safari siku ya Alhamisi tutaongea na wenzetu tuone kwa nini siku hiyo wanakuwa hawatoi huduma hiyo.

La pili, ni kweli sasa hivi kutokana na shughuli za kiuchimi kuongezeka katika ukanda huo ambao sisi tunaita Ukanda wa Mtwara *Corridor* ni kweli kabisa na baada ya upatikanaji wa gesi asilia pale Songosongo shughuli za kiuchimi na kijamii zimeongezeka sana katika eneo hilo. Ombi la kukipandisha hadhi kiwanja chetu cha Mtwara ni wazo zuri kwa sababu katika mpango ambao tunao kuhusu viwanja vyetu nchini moja ya viwanja ambavyo tunaviona ni muhimu sana ni kiwanja cha Mtwara. Kwa hiyo, tuna mipango hiyo ya kuweza kukiboresha ili kiweze kuruhusu ndege kubwa za kisasa na pia kiwanja chenyewe kiweze kuhudumia abiria na ndege hizo kwa kiwango cha kimataifa.

Huko tunakokwenda ndiyo ushindani mkubwa ambao tunataka kuona kwa ukanda huu.(*Makofi*)

Na. 174

**Ushughulikiaji wa Mikataba Mbalimbali**

**MHE. OMAR S. KWAANGW'** aliuliza:-

Kwa kuwa, ni muhimu sana kuhakikisha kwamba, maslahi ya nchi yetu yanalindwa Kiserikali katika Mikataba mbalimbali ambayo Serikali husaini:-

(a) Je, utaalamu wa kisheria wa Mawakili wa Serikali na wa watu wengine katika fani husika unaunganishwa vipi ili kulinda maslahi ya Taifa hasa katika maeneo muhimu kama madini, Gesi, Mafuta, kodi na mambo yahusuyo fedha?

(b) Kwa kuwa kazi kubwa ya Bunge ni kusimamia na kuishauri Serikali. Je, ni katika hatua ipi kabla ya mkataba hasa ile mikubwa ambapo Bunge na Kamati zake linaweza kutoa ushauri wake kabla ya Mkataba husika haujasainiwa na Serikali?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** Alijibu:-

Napenda kujibu la Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' Mbunge wa Babati Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Omar Kwaangw' kwamba Serikali inahakikisha kwamba inalinda maslahi ya Taifa inapojadili mikataba kwa kuunganisha taaluma mbalimbali katika kuichambua m ikataba hiyo kabla ya kusainiwa, kwa kuunda timu za majadiliano (*Government Negotiating Team*). Timu hizi hujumuisha wataalam wa fani mbalimbali zinazohusika kama vile sheria kodi ajira uhamiaji ambao hujumuika na wataalamu wengine mahususi katika sekta inayoingia mikataba. Timu hizo huipitia mikataba na kuweka msimamo wa pamoja utakaokuwa msingi wa majadiliano na upande mwingine. Kwa kuwa, kuundwa kwa timu kama hizi, kunaiwezesha Serikali kuandaa hoja zitakazotumika wakati wa majadiliano, ni wazi hatua hiyo huiwezesha Serikali kulinda maslahi yake na ya wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi ya kujadili na kufunga mikataba ni ya utendaji. Katiba yetu imejengeka katika msingi wa mgawanyo wa mamlaka ambapo Serikali inawajibika kwa shughuli za utendaji. Madaraka ya Bunge kama Msimamizi Mkuu wa shughuli za Serikali ni kuweka masharti ya jumla kama itabidi, kwa kutunga sheria, kupitisha sera au kuidhinisha bajeti ya Serikali. Tayari Bunge limetunga Sheria ya Manunuzi ya Umma, Sheria ya Mikataba na kadhalika ambazo huiongoza Serikali katika kufunga mikataba ya manunuzi.

Bunge halipaswi kufanya kazi ya kupitia mikataba kabla ya kusainiwa ili lenyewe libaki na uhalali wa kuhoji na kuiwajibisha Serikali kwa mujibu wa dhana ya mgawanyo wa mamlaka na kuchungana, kukosoana na kuwajibishana kwa lugha ya kingereza *checks and balances*. Serikali itaendelea kupokea maoni ya kuongeza uwazi, uwajibika bila kulimbikiza madaraka katika chombo kimoja cha dola.

Mheshimiwa Spika naomba kulihakikishia Bunga lako tukufu kuwa Serikali inawajibika kwa wananchi kupitia Bunge hili hususan katika mikataba inayoisaini hivyo Bunge linaweza kuhoja Serikali kwa utaratibu uliowekwa. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niliulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, tatizo kubwa katika eneo hili la mikataba ambalo limetajwa mara nyingi ni suala la uwazi na uwajibikaji na hasa inapotokea tatizo. Je, Serikali iko tayari kuandaa taarifa kila mwaka ya wale ambao wamefanya vibaya katika mikataba ili itusaidie kuisimamie Serikali badala ya kila wakati Wabunge kuuliza tatizo la uwazi na uwajibikaji katika mikataba?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Omar S. Kwaangw' kwa kuuliza swali la nyongeza na ninaomba kujibu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimelihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali iko tayari kupokea mawazo ya kuongeza uwazi na uwajibikaji katika masuala ya Mikataba na kwa hiyo wakati wowote ule kupitia Kamati mbalimbali za Bunge, Bunge linaweza likahoji mikataba ambayo inataka kuiona na kwa hiyo kuongeza uwazi wa mikataba hiyo kwa Bunge lako Tukufu.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa, mikataba hiyo imeshawahi kuulizwa na Kamati za Bunge na tukakataliwa kupewa. Je, Mheshimiwa Waziri utatuhakikishiaje kwamba tunaweza tukapata mikataba hiyo au ni kwanini tulikataliwa?

**WAZIRI WA KATIBA NA MAMBO YA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kumshukuru Mheshimiwa Mohammed Habib Juma Mnyaa kwa swali lake la nyongeza.

Napenda kujibu swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika kuna mikataba ya aina mbili yaani kuna mikataba ya nchi na nchi kwa hiyo nchi ya Tanzania na nchi nyingine na kuna mikataba ya kibiashara. Yote hayo yanaweza yakahojiwa na Bunge lako Tukufu isipokuwa jambo ambalo nalisisitiza ni kufuata utaratibu hasa kwa mikataba ya biashara ambayo wakati mwingine kuna usiri ndani yake katika kulinda maslahi ya biashara yenyewe.

Lakini kwa kufuata taratibu kwa mfano kupitia Kamati zinazohusika bado Bunge linaweza likataka mikataba hiyo na kuweka ile siri inayotakiwa lakini wakati huo huo kupata taarifa zinazotakiwa.

Na. 175

**Ujenzi wa Mabwawa Makubwa na Madogo**

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka huu hali ya hewa imebadilika sana Wilayani Lushoto kutokana na ukame uliosababisha mito mingi na vyanzo vya maji kukauka:-

Je, Serikali itakuwa tayari kutuma wataalam kuainisha maeneo ya kujenga mabwawa makubwa na madogo na kusaidia kugharamia ujenzi wa mabwawa hayo ili upatikanaji wa maji safi na salama ufikie angalau 70%?

**SPIKA:** Nitahadharishe tu kama kutakuwa na nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri huyu kapata mialiko ya kutosha kabisa kutembelea mikoa mbalimbali. Sitakubali tena mialiko mingine. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunilinda juu ya kupata mialiko kama wenzangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Lushoto ni miongoni mwa Wilaya zenye hali nzuri ya hewa, mvua za kutosha na vyanzo mbalimbali vya maji ya mtiririko.

Mheshimiwa Spika, katika kukidhi mahitaji ya maji kwa matumizi ya binadamu katika maeneo mbalimbali nchini, Serikali inajenga mabwawa katika maeneo kame. Lengo la mpango huo ni kuwa na vyanzo endelevu vya maji. Katika ujenzi huo, kipaumbele kimewekwa kwenye maeneo kame na yasiyokuwa na vyanzo mbadala vya maji.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kutambua kuwa ujenzi wa bwawa kama chanzo cha maji kwa matumizi ya binadamu ni gharama kubwa. Gharama hii, inatokana na ujenzi wa tuta la bwawa na mtambo wa kusafisha maji yaliyohifadhiwa kwenye bwawa. Hata hivyo, gharama hizi ambazo mwishowe hubebwa na mtumiaji maji, zinaweza kuepukika tu kama kuna vyanzo mbadala kama vile chemichemi, maji ya chini ya ardhi, mito na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali ya ukame iliyojitokeza kati ya mwaka 2005 na 2006, kwa wastani Wilaya ya Lushoto ina vyanzo vingi vya maji, ikilinganishwa na maeneo mengine nchini. Wilaya ina vyanzo vya maji vilivyopo milimani, vinavyoweza kuendelezwa kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama kwa gharama nafuu ya uendeshaji na matengenezo.

Kwa sasa, kipaumbele cha ujenzi wa mabwawa kimewekwa kwenye maeneo kame. Ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi Wilayani Lushoto, namshauri Mheshimiwa Mbunge aendelee kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya katika kuainisha miradi ya maji itakayotumia vyanzo asili vilivyopo na kutelekezwa chini ya Program ya maendeleo ya sekta ya maji. Wizara yangu ipo tayari kutoa ushauri wa kiufundi kwa Wilaya ya Lushoto kuhusu ujenzi wa miradi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mabwawa pale itakapohitajika.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Wilaya ya Lushoto ni Wilaya ya milimani, tunaishi kwa kilimo cha mboga na matunda. Mwaka jana mito yetu mingi ilikauka, tuliamini kwamba ujenzi wa mabwawa utasaidia kutupatia maji ya kunywa, maji ya kumwagilia na ikiwezekana mitambo midogo ya kuzalisha umeme. Je, Serikali ipo tayari kutusaidia katika hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama jibu langu la awali lilivyosema ni kwamba, miradi yote hii ya maji inapitia katika Halmashauri zetu za Wilaya. Kwa hali hiyo basi, miradi ya maji ambayo Mheshimiwa Mbunge anachoomba iweze kufanyika, namshauri arudi kwenye Halmashauri ya Wilaya ili waweze kuipendekeza na kuibua miradi hiyo.

Kwa hivi sasa kwa Wilaya ya Lushoto na katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge kuna miradi mitatu mikubwa ambayo itaweza kusaidia maji. Yeye naomba akashirikiane nao kama hii itakidhi sehemu hizo. Miradi hiyo ikiwemo Mhelo, Mlola na Ngulu, lakini hata hivyo pia Jimbo lake la Lushoto limefanikiwa kupata hela za *quick wins* na hela hizo zinakwenda katika sehemu ambazo nina uhakika zitaweza kukidhi mahitaji hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima yako na ruhusa yako naomba nimtajie haraka haraka. Kuna mradi wa mtiririko ambao maji yapo na sasa umeomba hela mradi huu unaitwa Malimbwi.

Pia kuna mradi mwingine wa kuchimba visima iko mitatu ambayo ni Malindi, Kwekaga na Lendwai. Pia kuna mradi mwingine katika Jimbo lako wa mtiririko na maji yapo ambao unaitwa Irete-Iyongoi na mwingine pia mradi wa *gravity scheme* unaita Ngulu na nina uhakika kwamba miradi hii itatosheleza sehemu mbalimbali na kama kuna zaidi ya hapo aibue kwa kupitia kwenye Halmashauri. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Ninayo tu matangazo machache. Kwanza wapo wageni wangu kwenye *Speaker's Gallery*, Viongozi wa Chama cha Walimu Tanzania. Nikiwatamka wageni wetu naomba msimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwatambua. Kwanza ni Ndugu Gracian Mkoba, Rais wa Chama cha Walimu Tanzania, karibu sana na hongera sana kwa ushindi wa uchaguzi. (*Makofi*)

Halafu yupo Ndugu Yahya Msulwa – Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu, Tanzania; halafu yupo rafiki yangu Ndugu Mohamed Utali, Mweka Hazina Taifa wa Chama cha Walimu na mwenyeji wao Bwana Sudi Mzense - Katibu wa Chama cha Walimu Manispaa ya Dodoma. Karibuni sana. (*Makofi*)

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi anaitwa Bwana Benjamini Sitta, ambaye yeye ni mwanawe, kijana huyu ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni yake binafsi aliyoianzisha mwenyewe inaitwa *E-Life Group*, inayofanya kazi ya mawasiliano ya *Internet*. (*Makofi*)

Ahsante Ben. Simama basi bwana, loh! Ulikuwa umesimama ukaanza kuketi tena kabla sijamaliza *introduction*. Tunakushukuru sana sisi wazazi wako kwa kuwa wewe si mzigo ni baraka kwa sababu unajitegemea na mara kwa mara ukipata dola zako unatusaidia. Ahsante. (*Kicheko*)

Wageni wengine ni kama ifuatavyo: Wapo walimu wakuu sabini wa shule za msingi za Manispaa ya Morogoro. Walimu mliotoka Morogoro mnaweza kusimama pale

mlipo. Nadhani wapo njiani, tuwaombee safari njema kwa sababu barabara nazo zina matatizo.

Wapo hapa kwenye *gallery*, wakuu wa Vyuo vya Ualimu na Waratibu wa Elimu Wilaya wa Mkoa wa Dodoma, hata wa Dodoma nao, ahaa wale pale, ahsanteni sana wageni wetu. Wapo vijana ishirini na tatu kutoka Tanzania Bara na Visiwani ambao wameletwa kujifunza jinsi demokrasia ya uwakilishi inavyofanya kazi, wameletwa na taasisi ya Tanzania *Youth Alliance* (*TAYOA*), naomba wasimame, wale pale, ahsante karibuni sana vijana na karibuni zaidi wale mnaotoka ng'ambo ya bahari huko Zanzibar. Karibuni sana.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Lawrence Masha ambao ni Mama Stella Masha, mke wa Naibu Waziri. Sijui wako wapi, Mheshimiwa Naibu Waziri siku nyingine ufanye utaratibu watu kama hawa hukaa *Speaker's Gallery* pamoja na watoto wao. Stella Masha naomba asimame, Amani Masha na Lawrence Masha Junior, sijui naye atakuwa Mwanasheria. (*Makofi*)

Wageni wetu wengine Bungeni ni walimu watano wa shule ya chekechea Mvumi *Mission*, wageni wa Mheshimiwa John Malecela, Mbunge wa Mtera, wako wapi? Wale pale, karibuni sana. Nashukuru sana, mna kazi ngumu sana ya kufundisha chekechea. Siku nyingine ni vizuri mje na chekechea hao mnaowafundisha ili nao waone Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Charles Mlingwa, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Mifugo ana mgeni wake ambaye ni Bwana Samson Masele, mpiga kura, amemwunga mkono vizuri sana kule Shinyanga Mjini lakini pia ni shemeji yake. Yule pale, karibu sana Bwana Masele na uendelee kumwunga mkono kijana huyu Mlingwa, anafanya kazi vizuri sana hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mikutano, Mheshimiwa Alhaj Missanga ameniomba nitangaze kwamba Kamati ya Miundombinu wajumbe wake wakutane leo saa saba mchana, ukumbi Na. 231, Jengo la Utawala.

Mheshimiwa William Shellukindo ameniomba nitangaze kwamba, Kamati ya Uwekezaji na Biashara wakutane leo saa saba mchana, Ukumbi Na. 219, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, mwenzetu Mheshimiwa Ponsiano Nyami alikuwa amekwenda nje kwa masomo na amerejea. Ningeomba asimame pale alipo, ahaa yule pale. Amehitimu vizuri na amesema niwasomeeni ujumbe ufuatao. Waheshimiwa Wabunge msome sana *computer*, hivi sasa ndio ukombozi wa pekee wa kuijua dunia ya ulimwengu wa leo, kwa urahisi pia wa utafutaji, utafiti wa *data*, *computer* ni msingi muhimu sana. Ahsante sana umetupa moyo. (*Makofi*)

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008**
**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii iliyochambua makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kwanza kuwashukuru kipekee Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Makamu wa Rais Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Waziri Mkuu Edward Ngoyai Lowassa kwa msukumo walioutoa katika ujenzi wa shule za sekondari. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wote wa ngazi zote wa Chama na Serikali kwa juhudi walizozifanya katika kuhamasisha wananchi ambao walishiriki kikamilifu katika ujenzi na hatimaye usajili wa shule mpya 1,084 za sekondari nchini mwaka 2007.

Nawashukuru pia Waheshimiwa Naibu Mawaziri wote kwa kushiriki katika zoezi la ufuatiliaji wa ujenzi wa shule za sekondari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kwa niaba ya Wizara yangu kutoa pole kwa Wabunge wote na wananchi kwa kifo cha Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Bunge na Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mbunge Viti Maalum. Daima tutawakumbuka kwa jinsi walivyojitolea maisha yao kuitumikia nchi yetu kwa juhudi kubwa. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi.

Nachukua nafasi hii pia kutoa pole kwa ndugu wa abiria wote waliofariki katika ajali nyingi zilizotokea hivi karibuni zikiwemo za Mikoa ya Arusha na Singida. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza wafuatao kwa kuteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali: Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro, aliyekuwa Mbunge Viti Maalum na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, aliyekuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, aliyekuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge), Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji; Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mbunge wa Sengerema kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kwa kuchaguliwa na Wananchi wa Tunduru kuwa Mbunge

wao na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge Viti Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa hotuba yake ambayo imetoa tathmini, mwenendo na mwelekeo wa uchumi wa Taifa kwa jumla na Mheshimiwa Zakhia Hamdani Meghji, Waziri wa Fedha, kwa hotuba yake iliyoelezea kwa ufasaha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2007/2008.

Bajeti hii imetoa kipaumbele kwa sekta muhimu katika kukuza uchumi ikiwemo Sekta ya Elimu ambayo inao wajibu mkubwa katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) kwa kuboresha nguvu kazi ya Taifa kwa njia ya elimu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu Edward Ngoyai Lowassa, kwa Hotuba yake iliyofafanua mambo muhimu ya elimu yaliyoamuliwa na kutekelezwa na Serikali. (*Makofi*)

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Mawaziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Mwantumu Bakari Mahiza, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Jimbo la Kalambo, kwa ushirikiano, uaminifu na uadilifu waliouonesha kwangu, kwa viongozi wetu Wakuu Serikalini na kwa watumishi wote Wizarani. Aidha, natoa shukrani zangu kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Professa Hamisi Omar Dihenga na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Oliver Paul Mhaiki, pamoja na Afisa Elimu Kiongozi Ndugu Ricky Abiud Mpama kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Omari Shaban Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini, kwa ushauri na maelekezo iliyoyatoa ya kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi baada ya uchambuzi wao wa kina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekabidhiwa kusimamia na kutekeleza majukumu yafuatayo:

(a) Elimu ya Awali;
(b) Elimu ya Msingi;
(c) Elimu ya Sekondari Kidato cha 1 - 6;
(d) Elimu itolewayo kwa wenye mahitaji maalumu;
(e) Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi;
(f) Mafunzo ya Ufundi;
(g) Mafunzo ya Ualimu Daraja A na Stashahada;
(h) Kuandaa na kusimamia mitaala ya shule, vyuo vya ualimu na ufundi;
(i) Kuhakiki na kupima ubora wa elimu kwa kuendesha ukaguzi wa shule;

(j) Kutunga na kuendesha mitihani ya kitaifa ya Darasa la IV, VII, Kidato cha 2, 4 na 6 na mitihani ya Elimu ya Ualimu na Ufundi;

(k) Kutafiti, kutunga sera, kupanga na kuratibu mipango ya elimu; na

(l) Kutoa miongozo ya uendeshaji na kusimamia kazi za Wakala, Taasisi na Mabaraza Wizara ambayo ni:

  (i) Baraza la Mitihani Tanzania *(NECTA);*

  (ii) Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania *(TLSB);*

  (iii) Kituo cha Maendeleo Dakawa;

  (iv) Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA);*

  (v) Taasisi ya Elimu Tanzania *(TIE);*

  (vi) Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima *(IAE);* na

  (vii) Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu *(ADEM)*.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia na kutekeleza majukumu yake, Wizara inaongozwa na:

(a) Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995;

(b) Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na rekebisho Na. 10 la mwaka 1995 na Na. 2 la mwaka 1998;

(c) Sheria Na. 1 ya Mafunzo ya Ufundi Stadi ya mwaka 1994;

(d) Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya mwaka 2025;

(e) Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA); na

(f) Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne imeamua kuipa kipaumbele Sekta ya Elimu kwa kutambua kuwa elimu ni nyenzo muhimu katika kupambana na ujinga, maradhi na umaskini. Elimu ni mhimili mkuu katika kuleta maendeleo ya haraka na Maisha Bora kwa kila Mtanzania. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na rekebisho lake la mwaka 2005, Ibara ya 11 kifungu cha tatu inaielekeza Serikali kufanya jitihada kuhakikisha kwamba watu wote wanapata fursa sawa ya kupata elimu katika ngazi zote. Aidha, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hotuba yake ya kulizindua Bunge jipya Mjini Dodoma tarehe 30 Desemba, 2005 alisisitiza kuwa elimu itakuwa ajenda muhimu ya Serikali ya Awamu ya Nne. Alibainisha pia kuwa Serikali itashirikiana na wananchi na wadau wengine wa elimu kujenga vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, maabara na vyoo kama Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala CCM ya mwaka 2005 inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha takribani miaka miwili tangu Serikali ya Awamu ya Nne kuingia madarakani, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wananchi imefanya kazi kubwa ya kuhakikisha kuwa zaidi ya asilimia 75 ya wanafunzi wote wanaofaulu Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi wanaingia sekondari. Katika mwaka 2007/2008 Wizara yangu inakusudia kuweka kipaumbele katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, ujenzi wa nyumba za walimu ambapo tutajenga nyumba 1500 zitakazogharimu kiasi cha shilingi bilioni 13.5 sawa na 59% ya fedha zote za ujenzi zilizotengwa katika Wizara yangu kwa mwaka 2007/2008, pili, ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari na Mafunzo ya ualimu vyenye thamani ya shilingi bilioni 15.2 na tatu kuendelea kutoa mafunzo kazini kwa ajili ya kuwawezesha walimu wa masomo hasa masomo ya sayansi na hesabu ambayo katika ngazi zote mbili za sekondari *(O Level* na *A Level)* mwaka 2006 na 2007 hayakuwa na matokeo mazuri. Hivyo kiasi cha shilingi bilioni 1.5 zimetengwa kwa ajili ya mafunzo kazini ilikuinu kiwango cha ufaulu wa masomo hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inasimamia, kuratibu na kutoa sera na miongozo mbalimbali kuhusu Elimu ya Awali na Msingi. Elimu hii ni haki ya kila mtoto na ni muhimu kwa kumjengea misingi imara ya kujua kusoma, kuandika na kuhesabu. Aidha, Elimu ya Msingi ni nyenzo muhimu katika kumuandaa mtoto kwa ngazi za juu za elimu. Mikakati na miradi mbalimbali imeanzishwa ili kuboresha elimu ya msingi na kutoa fursa sawa ya elimu kwa watoto wote.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) awamu ya kwanza ulianza mwaka 2002 na kukamilika mwaka 2006. Mwaka 2006/2007 ulikuwa wa kuandaa na kukamilisha awamu ya pili ya MMEM (2007 - 2011) ambapo utekelezaji utaanza mwaka 2007/2008. Pamoja na maandalizi hayo, miradi ya Shule Zenye Mazingira Yanayomjali Mtoto, Kukomesha Ajira Mbaya kwa Watoto na Mradi wa Lishe Shuleni ilitekelezwa. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na wadau ilitekeleza kazi zifuatazo:

(a) Kuandikisha wanafunzi 795,011 katika shule na madarasa ya Awali ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 125,874 sawa na asilimia 18.8 ya wanafunzi 669,137 walioandikishwa mwaka 2006;

(b) Kuandikisha wanafunzi 1,407,812 wa Darasa la I sawa na asilimia 120.7 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,166,737;

(c) Kujenga vyumba vya madarasa 2,303 kwa kutumia Ruzuku ya Maendeleo ya shilingi 7,139,300,000. Hili ni ongezeko la vyumba vya madarasa 1,443 ya lengo la kujenga vyumba vya madarasa 860;

(d) Kujenga nyumba 2,183 za walimu hususan kwenye Halmashauri 104 za vijijini, kwa kutumia Ruzuku ya Maendeleo ya shilingi 7,858, 800,000. Hili ni ongezeko la nyumba 1,683 ya lengo la kujenga nyumba za walimu 500 sawa na asilimia 336.6;

(e) Kuratibu ajira ya walimu wapya 6,565 katika Halmashauri zote;

(f) Kufuatilia, kuratibu na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) katika Halmashauri 56 sawa na asilimia 42 ya lengo la kutathmini Halmashauri 121:

(i) Kuhakiki vituo vyote 8,384 na kusimamia mafunzo kwa walimu wa MEMKWA 7,489 sawa na asilimia 89.6;
(ii) Kununua na kusambaza vitabu 180,000 sawa na asilimia 55 ya vitabu 325,726 vilivyokusudiwa;
(iii) Kuendesha warsha ya Kitaifa kwa wawakilishi 80 wa wadau wa elimu ili kubainisha mafanikio na changamoto; na
(iv) Kutoa mtihani wa Darasa la IV kwa wanafunzi 36,668 ambapo 30,919 sawa na asilimia 84 walifaulu na kujiunga na mfumo rasmi wa shule za msingi (Darasa la V na VI);

(g) Kuratibu Mtihani wa Darasa la IV na VII kwa wanafunzi 3,091waliotolewa katika ajira mbaya (mashambani, migodini na majumbani) katika Mradi wa Kukomesha Ajira Mbaya ya Watoto kupitia MEMKWA, ambapo wanafunzi 2,129 sawa na asilimia 69.0 walifaulu na kujiunga na mfumo rasmi wa shule. Mradi unatekelezwa katika mikoa ya Arusha, Manyara, Tabora, Singida, Dodoma, Iringa na Dar es Salaam;

(h) Kutoa Ruzuku ya Uendeshaji kwa wanafunzi 7,879,688 ambapo shilingi 24,817,299,800 zilipelekwa kwenye Halmashauri zote. Kati ya fedha hizo shilingi 8,526,919,920 zilitengwa kununulia vitabu na shilingi 3,500,000,000 zilitengwa kununulia vivunge vya sayansi na hisabati;

(i) Kutoa chakula cha mchana na huduma ya maji kwa wanafunzi pamoja na kupanda miti ya kivuli na matunda katika shule za Msingi 622 za Mpango wa Shule Zenye Mazingira Yanayomjali Mtoto unaotekelezwa katika Halmashauri za Kisarawe, Masasi, Songea (V), Musoma (V), Ngara na Makete;

(j) Kufuatilia utekelezaji wa Mradi wa Lishe katika shule 315 za kutwa na 15 za bweni uliohusisha ujenzi wa visima vinne, majiko 58 na matangi ya maji manne katika shule za mradi katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Arusha. Mafanikio ya mradi ni pamoja na ongezeko la mahudhurio kutoka asilimia 77.5 mwaka 2003 hadi asilimia 81.0 mwaka 2006 na kupungua kwa mdondoko wa wanafunzi kutoka asilimia 6.0 mwaka 2003 hadi asilimia 3.4 mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008, Wizara itaanza utekelezaji wa awamu ya pili ya MMEM (2007 - 2011) unaotoa kipaumbele kwa Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi ili kuyafikia malengo ya Elimu kwa wote, Malengo ya Maendeleo ya Milenia na MKUKUTA. Katika kufikia azma hii, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI na Wadau mbalimbali itatekeleza kazi zifuatazo:

(a) Kuandaa na kusambaza miongozo ya utekelezaji wa MMEM II;

(b) Kutoa mafunzo kwa watendaji na wasimamizi wa elimu ili kujenga uwezo wa usimamizi wa MMEM II;

(c) Kufuatilia uandikishaji wanafunzi 1,033,000 wa Elimu ya Awali wenye miaka 5 - 6 na wanafunzi 1,197,459 wa Darasa la I wenye umri wa miaka 7;

(d) Kukarabati majengo na miundombinu ya shule maalum ya Serikali inayotumia Kiingereza 'Arusha *School'* ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(e) Kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa MEMKWA;

(f) Kufuatilia matumizi ya ruzuku ya uendeshaji wa shule inayotolewa ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(g) Kuanzisha Mpango wa Shule Zenye Mazingira Yanayomjali Mtoto katika Halmashauri zenye mdondoko wa wanafunzi na mahudhurio hafifu za Hai, Magu, Makete, Bagamoyo, Mtwara (V) na Temeke kwa ufadhili wa *UNICEF;*

(h) Kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mradi wa Lishe Shuleni na kujenga majiko 35 na matangi sita ya maji katika shule za mradi kwa ufadhili wa Mpango wa Chakula Duniani;

(i) Kuratibu ukaguzi wa fedha za MMEM 2006/2007, tathmini ya utekelezaji wa MMEM II, utekelezaji wa mtaala ulioboreshwa na malipo ya posho ya walimu wanafunzi;

(j) Kuratibu na kufuatilia utoaji wa elimu kwa watoto walioondolewa katika ajira mbaya, katika Halmashauri za Kondoa, Iramba, Iringa(V), Arusha (M), Arumeru, Simanjiro, Urambo, Temeke, Ilala, Kinondoni, Mwanza (J), Lindi (V) na Kilwa kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani; na

(k) Kuratibu utoaji wa Elimu ya Awali na MEMKWA kwa watoto 10,000 walioondolewa katika ajira mbaya, katika kata mbili kwa kila Halmashauri za Kwimba, Ilemela, Igunga, Urambo na Iramba. Mradi utatekelezwa kwa ushirikiano na shirika la '*Winrock International*' kupitia mradi wa '*Tanzanian Education Alternatives for Children (TEACH)'*.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kusimamia, kuratibu na kuimarisha utoaji wa elimu ya sekondari Kidato cha 1 - 6 na kuwahamasisha wananchi kushiriki katika ujenzi wa Shule za Kutwa hususan maeneo ambayo hayana shule za kutosha.

Aidha, msisitizo umewekwa katika kuongeza usawa kijinsi na kuongeza fursa zaidi kwa makundi mbalimbali wakiwemo wenye ulemavu na yenye tofauti ya mapato. Sanjari na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), Mradi wa *Prevention and Awareness in Schools of HIV and AIDS (PASHA)* utaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, nchi yetu imepata mafanikio makubwa katika upanuzi wa Elimu ya Sekondari kama inavyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Mafanikio haya yametokana na wananchi kuitikia wito wa serikali wa kuchangia katika ujenzi wa shule za sekondari.

Aidha, matokeo ya mwitikio huo yamewezesha ongezeko la idadi ya shule za sekondari za Serikali kutoka shule 1,202 mwaka 2005 hadi kufikia shule 2,774 Mei 2007 zikiwemo shule 488 zilizojengwa mwaka 2006 na shule 1,084 zilizojengwa mwaka 2007 hadi kufikia mwezi Juni. (*Makofi*)

Ujenzi wa shule 488 mwaka 2006 uliwezesha wanafunzi 243,359 sawa na asilimia 79.8 ya waliofaulu Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2005 kujiunga na kidato cha 1 mwaka 2006.

Kabla ya juhudi hizo, ni wanafunzi 148,412 sawa na asilimia 48.6 tu kati ya wanafunzi 305,062 waliofaulu walikuwa wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2006.

Ujenzi wa shule 1,084 uliwezesha wanafunzi 401,011 ambao ni asilimia 85.6 kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2007 kati ya wanafunzi 468,279 waliofaulu Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, kabla ya juhudi hizi, ni wanafunzi 231,282 sawa na asilimia 49.4 tu ya waliofaulu walikuwa wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu. Haya ni mafanikio makubwa ya kujivunia ambapo lengo lililowekwa lilifikiwa la zaidi ya asilimia 75 ya wanafunzi waliofaulu Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2006 wamejiunga na Elimu ya Sekondari. Pamoja na mafanikio hayo Wizara ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kuchangia ujenzi wa madarasa mapya 1,631 katika shule za sekondari za wananchi Kidato cha I - 4 na madarasa 128 katika shule za sekondari zenye Kidato cha 5 na 6. Aidha, mchango huu umewezesha shule 1,160 kujengwa ambapo shule 1,084 zimesajiliwa baada ya kukidhi vigezo;

(b) Kutoa ruzuku ya kuchangia ujenzi wa nyumba 1,000 za walimu katika shule za sekondari za serikali hususan vijijini;

(c) Kuchangia ujenzi wa maabara 2 kwa shule moja kila Mkoa;

(d) Kuchangia ujenzi wa majengo ya maktaba katika shule 30 za Serikali na ujenzi wa vyoo katika shule 47 za Serikali;

(e) Kutoa ruzuku ya ukarabati wa shule 16 za Kitaifa kati ya 30 zilizopangwa;

(f) Kuratibu na kufuatilia ukarabati wa miundombinu katika shule zenye wanafunzi wenye ulemavu za Njombe, Pugu na Jangwani na Kazima;

(g) Kugharimia wanafunzi 33,865 wa Kidato cha I - 4 wanaotoka kwenye familia zenye kipato duni na wasichana 147 waliokuwa wakigharimiwa na Mradi wa '*Girls Secondary Education Support'* (*GSES)* uliokwisha mwaka 2003;

(h) Kuchangia ujenzi wa hosteli katika shule za Ketumbeine (Arusha), Kiwere (Tabora), Madwanga (Lindi), Msitu wa Tembo (Manyara) na Kizigo (Singida);

(i) Kutoa fedha za punguzo la ada kwa wanafunzi 417,712 katika shule za kutwa 1,694;

(j) Kutoa fedha za ujenzi wa mabweni 24 katika shule 24 zenye kidato cha 5 na 6;

(k) Kudahili wanafunzi 401,011 wakiwemo wasichana 188,846 na wavulana 212,165 kujiunga na kidato cha I mwaka 2007;

(l) Kudahili wanafunzi 21,791 kujiunga na Kidato cha 5 wakiwemo wasichana 8,639 na wavulana 13,152;

(m) Kugharimia mafunzo ya walimu 40 katika Stashahada ya Uzamili ya Elimu, walimu 6 Shahada ya Uzamili ya Elimu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na walimu 97 Shahada ya Hisabati katika Chuo Kikuu cha Tumaini;

(n) Kugharimia vitabu na utafiti kwa walimu 150 wanaosoma Chuo Kikuu Huria;

(o) Kugharimia ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule 1,715 za Serikali na shule 104 zisizo za Serikali; na

(p) Kuwapatia mafunzo ya Uongozi na Menejimenti Wakuu wa Shule 450 na Waratibu 103 wa Elimu ya Sekondari wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, kwa kushirikiana na wadau wa elimu, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kugharimia wanafunzi 42,710 wa Kidato cha 1 - 4 na wanafunzi 3,352 wa Kidato cha 5 na 6 wanaotoka kwenye familia zenye kipato duni;

(b) Kuratibu na kufuatilia ukarabati wa miundombinu katika shule zenye wanafunzi wenye ulemavu: Moshi Ufundi, Moshi Sekondari, Lugalo, Mpwapwa, Korogwe, Iringa na Kazima;

(c) Kuendelea kutoa ruzuku ya punguzo la ada na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na vya wanafunzi wenye ulemavu kwa shule za Serikali;

(d) Kuendelea kutoa ruzuku ya kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa shule zisizo za Serikali ambazo zinakidhi vigezo vilivyowekwa;

(e) Kuchangia ujenzi wa hosteli 10 kwa ajili ya wasichana katika maeneo ya wafugaji na yaliyo nyuma kielimu;

(f) Kuchangia ujenzi wa madarasa 800 na vyoo 76 katika shule za Serikali;

(g) Kujenga madarasa 128 ya Kidato cha 5 na 6. Madarasa 60 yatajengwa katika shule mpya 30 na 68 yatajengwa kwenye shule za zamani za '*A level'*;

(h) Kujenga maabara 84, maktaba 30, majengo ya utawala 14 na kukarabati shule 15 za Serikali;

(i) Kutoa ruzuku ya kuchangia ujenzi wa nyumba 1,500 za walimu katika shule za sekondari za serikali husan kwenye maeneo yenye mazingira magumu;

(j) Kuendesha mafunzo kuhusu MMES kwa ajili ya viongozi wa ngazi ya Mkoa na Wilaya;

(k) Kuwapatia mafunzo ya Uongozi na Menejimenti Wakuu wa shule wapya, Bodi za Shule, Timu za Menejimenti za shule na maafisa walioko makao makuu;

(l) Kuendelea kugharimia mafunzo ya walimu wa Shahada ya Kwanza: 500 Chuo Kikuu Huria, 120 Chuo Kikuu cha Tumaini na Shahada ya Uzamili 10 Chuo Kikuu cha Dar es salaam; na

(m) Kuendeleza matumizi ya TEHAMA katika mchakato wa kufundisha na kujifunza.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza MMEM na MMES, Wizara yangu iliendelea kuratibu, kusimamia na kuimarisha utoaji wa mafunzo tarajali na kazini kwa walimu wa Daraja A na Stashahada. Kutokana na mipango hiyo mikakati iliwekwa kuandaa walimu bora wa shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006/2007 Wizara yangu imefanikiwa kutekeleza yafuatayo kulingana na mikakati na malengo iliyojiwekea:-

(a) Kufunga na kuviunganisha kwenye mtandao wa intaneti kwa njia ya *satellite (VSAT System)* vyuo vya ualimu vya Serikali;

(b) Kutoa mafunzo kwa wanachuo 7,200 wa mafunzo ya ualimu tarajali Daraja A na 4,390 wa Stashahada;

(c) Kuendesha mafunzo maalumu ya mbinu za kufundishia kwa wahitimu 6,000 wa Kidato cha 6 wenye sifa;

(d) Kugharimia mafunzo ya wakufunzi 645 wanaojiendeleza: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 17 na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania 628 pamoja na walimu 1,500 wa leseni wanaosoma katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania;

(e) Kugharimia maandalizi ya muhtasari wa kufundisha TEHAMA katika Vyuo vya Ualimu;

(f) Kuendesha mafunzo kwa walimu 86 kwa ajili ya kufundisha somo la Kifaransa katika shule 46 za msingi;

(g) Kuendesha mafunzo ya ualimu Daraja A kwa njia ya moduli kwa walimu 21,519 wa Daraja B/C ambapo 20,021 sawa na asilimia 92.1 walifaulu mtihani wa Mafunzo ya Ualimu Kazini (MUKA);

(h) Kutoa mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kuhusu *'Cisco-IT Essentials Networking'* kwa wakufunzi 80 na *'International Computer Driving Licence' (ICDL)* kwa wakufunzi 32;

(i) Kupanga walimu wanafunzi 6,103 wa mafunzo tarajali Daraja A kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo na 3,170 wa Stashahada kuanza kazi;

(j) Kutoa mafunzo kwa wakufunzi na walimu 2,650 wa shule za msingi kuhusu ufundishaji wa Elimu ya UKIMWI kwa kutumia mbinu bainifu. Mafunzo yaligharimiwa na UNICEF;

(k) Kutoa mafunzo ya Elimu ya UKIMWI kwa walimu 61 kutoka mikoa ya Mtwara na Lindi kwa msaada wa *UNICEF* na *UNAIDS* kupitia *UNESCO*;

(l) Kukamilisha rasimu ya Mkakati wa Maendeleo na Menejimenti ya Walimu (*Teacher Development and Management Strategy-TDMS*); na

(m) Kukarabati Vyuo vya Ualimu vya Katoke, Mhonda, Vikindu, Kinampanda, Ndala, Mpuguso, Kabanga, Bustani, Singachini, Ilonga, Mtwara Ufundi, Murutunguru na Kasulu.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2007/2008. Maendeleo endelevu ya elimu yanahitaji kuwepo kwa walimu wa kutosha wenye sifa katika shule na vyuo vyote, pamoja na mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia. Ili kufanikisha azma hiyo, mwaka 2007/2008 Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha maandalizi ya miundombinu ya mtandao wa TEHAMA katika vyuo vyote 32 vya ualimu vya Serikali;

(b) Kutoa mafunzo kwa wanachuo 9,000 wa mafunzo ya ualimu tarajali Daraja A watakaofundisha katika madarasa ya Awali na shule za Msingi;

(c) Kutoa mafunzo kwa wanachuo 6,498 wa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu watakaofundisha katika shule za sekondari. Muda wa mafunzo haya ni mwaka mmoja chuoni na mwaka wa pili utakuwa wa kufundisha kwa vitendo shuleni ili kupunguza pengo la mahitaji ya walimu;

(d) Kutoa mafunzo ya matumizi ya njia na mbinu bainifu katika ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu 105 wa Elimu Maalumu na Sayansi Kimu wanaoomba kujiunga na mafunzo ya kujiendeleza katika Vyuo vya Ualimu;

(e) Kuendesha mafunzo mafupi kwa awamu kwa Maafisa elimu wa Mikoa 21, watendaji wa Idara na Taasisi 26, Wakaguzi wa Shule wa Kanda na Wilaya 131, Wakuu wa vyuo 32, Maafisaelimu wa Wilaya 123, Wakufunzi 160 na Walimu wawezeshaji 246 kuhusu wajibu na majukumu yao katika utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo na Menejimenti ya Walimu ili waweze kumudu majukumu yao kwa ufanisi;

(f) Kutoa elimu ya masuala mtambuko, huduma za afya na kinga ya maambukizi ya UKIMWI kwa wakufunzi, wanachuo na jumuia zinazozunguka vyuo vya ualimu;

(g) Kuendesha mafunzo ya ualimu Daraja A kwa njia ya moduli kwa walimu 1,600 wa Daraja B/C walioshindwa mtihani wa (MUKA); na

(h) Kutoa mafunzo kazini kwa walimu wa sekondari katika masomo ya Lugha 200, Sayansi 200, Hisabati 200 na Mafunzo Maalumu kwa Walimu 5000 wa Leseni.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina jukumu la kuhakikisha utoaji bora wa taaluma na uendeshaji fanisi wa shule pamoja na kutoa ushauri kwa wadau wa elimu kuhusu njia bora za ufudishaji na ujifunzaji, mahitaji ya mafunzo kwa walimu, na uanzishaji wa shule.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara ilitekeleza kazi zifuatazo:

(a) Kukagua asasi 13,695 sawa na asilimia 68 ya lengo la kukagua asasi 20,112 (Kielelezo Na. 1). Aidha, ukaguzi maalumu kwa ajili ya usajili wa shule mpya ulifanyika katika shule 1,084;

(b) Kutoa nakala 500 za Mwongozo wa Mafunzo ya Awali ya Ukaguzi wa Shule na nakala 1,500 za Kiongozi cha Mkaguzi wa Shule;

(c) Kuboresha mazingira ya kazi kwa wakaguzi wa shule kwa:-(i) Kukarabati ofisi 20 za wilaya; (ii) Kununua samani za ofisi katika wilaya 12; (iii) Kutoa mafunzo

kabilishi kwa wakaguzi wa shule 1,064 kuhusu mitaala ya Elimu ya Msingi na Sekondari iliyoboreshwa; na (iv) kununua magari 16 kwa ajili ya Kanda za Kati, Kusini, Mashariki, Magharibi, Nyanda za Juu, Kaskazini Mashariki na Ziwa pamoja na Wilaya za Korogwe, Ludewa, Lindi (V), Mwanga, Hanang, Kondoa, Serengeti, Ulanga na Urambo.

(d) Kuratibu na kuendesha Mtihani wa Taifa Kidato cha 2 mwaka 2006 ambapo vituo 1,790 vilisajili watahiniwa 220,617. Watahiniwa 209,967 walifanya mtihani wakiwemo wasichana 102,563 sawa na asilimia 49.0 na wavulana 107,404 sawa na asilimia 51.0. Watahiniwa 159,972 sawa na asilimia 76.2 walifaulu, kati yao wasichana 70,482 sawa na asilimia 33.6 na wavulana 89,490 sawa na asilimia 42.6.

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kuhakikisha ubora na kudhibiti viwango vya elimu itolewayo, katika mwaka 2007/2008, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukagua asasi 23,126 (Kielelezo Na. 2);

(b) Kuboresha mazingira ya kazi kwa wakaguzi wa shule kwa kununua vifaa vya ofisi na samani katika wilaya 20 na kununua magari 15 kwa ajili ya ofisi za wilaya;

(c) Kutoa mafunzo ya awali ya ukaguzi wa shule kwa wakaguzi wa shule wapya 100 na mafunzo ya Uongozi na Menejimenti kwa wakaguzi 42 wa shule; na

(d) Kutoa elimu ya UKIMWI kwa wafanyakazi 200 wa Idara ya Ukaguzi wa Shule na kutoa huduma kwa watakaobainika kuwa na VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inasimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 na utoaji wa Nyaraka na Miongozo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Aidha, Wizara inaratibu na kusimamia Elimu ya Watu Wazima, Elimu kwa Redio, Elimu Maalumu, Elimu ya UKIMWI, Ushauri Nasaha, Elimu ya Mazingira na Usajili wa Shule.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu huratibu utoaji wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi wa Shule kupitia Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Walioikosa (MEMKWA) na Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA). Katika mwaka 2006/2007, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

(a) Kufuatilia utekelezaji wa Waraka wa Elimu Na. 3 wa mwaka 2006 katika mikoa 21 na kubaini kuwa Halmashauri 52 kati ya 123 zimeingiza mipango ya EWW katika bajeti zao;

(b) Kuratibu na kufuatilia mafunzo ya wawezeshaji wa MEMKWA katika Halmashauri 123 na MUKEJA katika Halmashauri 34 na kubaini kuwa mafunzo ya MEMKWA yalifanyika katika kila Halmashauri;

(c) Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa kuratibu na kusimamia mipango ya Elimu ya Watu Wazima kwa maafisa watendaji 84 ngazi ya Halmashauri kutoka mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Iringa; na

(d) Kufanya utafiti bainifu kuhusu utoaji wa Elimu ya Haki za Binadamu katika Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya upembuzi bainifu ili kupata taarifa sahihi zitakazosaidia kuandaa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya EWW kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Cuba;

(b) Kuandaa Mpango Mkakati wa Elimu kuhusu Haki za Binadamu Kanda ya Ziwa ili kujenga uelewa kuhusu madhara ya ukiukwaji wa Haki za Binadamu katika jamii;

(c) Kuratibu mafunzo ya wawezeshaji wa MEMKWA na MUKEJA katika Halmashauri 123;

(d) Kukarabati Vituo vya Uchapaji Makao Makuu na Kituo cha Kisomo Mwanza; na

(e) Kuratibu mpango wa majaribio wa matumizi ya mbinu bainifu katika kufundisha Kisomo cha Kujiendeleza katika wilaya za majaribio za Temeke na Mvomero.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Elimu Maalumu. Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2006/2007.Wizara yangu inaratibu Elimu kwa ajili ya watu wenye ulemavu hususan kupanga na kusimamia uimarishaji na upanuzi wa huduma za elimu. Katika jitihada za kuongeza nafasi za kuandikisha shule watoto wenye ulemavu, Wizara inatekeleza mfumo mpya wa Elimu Jumuishi. Mfumo huo unatumia shule za kawaida kuandikisha na kutoa elimu kwa watoto wenye ulemavu na watoto wasio na ulemavu kwa pamoja. Katika mwaka 2006/2007, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

(a) Kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia wanafunzi wenye ulemavu: wasioona na wenye uoni hafifu, viziwi na viziwi wasioona, wenye ulemavu wa akili na wenye *Otizim* vyenye thamani ya shilingi 314,791,000;

(b) Kuchapa na kusambaza vitabu vya kiada kwa shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu;

(c) Kuchapa na kusambaza nakala 1,000 za Mwongozo wa Mwezeshaji wa Mafunzo ya Elimu Jumuishi;

(d) Kutoa mafunzo ya Elimu Jumuishi kwa Walimu 432 katika Halmashauri 18; na

(e) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wataalamu wa Elimu Maalumu ya Wasioona na Wenye Uoni Hafifu 50, Wenye Ulemavu wa Akili na Wenye *Otizim* 50, Viziwi na Viziwi Wasioona 50.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa Mpango Mkakati wa kupanua na kuendesha Elimu Maalumu nchini kwa ushirikiano na Serikali ya *Finland*;

(b) Kununua na kusambaza; (i) Vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule zinazotoa Elimu Maalumu: Msingi 228, Sekondari 24 na Vyuo vya Ualimu vya Patandi, Tabora, Mpwapwa, Singachini na Vikindu; na(ii) Visaidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu walioandikishwa katika Shule za Msingi 78, Sekondari 24 na Vyuo 5 vya Ualimu;

(c) Kuendesha mafunzo ya wawezeshaji 708 wa Elimu Jumuishi katika Halmashauri 32 kutoka katika mikoa ya Kigoma, Iringa, Shinyanga na Manyara; na

(d) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa walimu wataalamu wa Elimu Maalumu 200 kikanda (Wasioona na Wenye Uoni Hafifu 50, Wenye Ulemavu wa Akili na Wenye *Otizim* 50, Viziwi na Viziwi Wasioona 50 na Wenye Ulemavu wa Viungo 50).

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inashughulikia usajili wa shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu kwa kuzingatia vigezo na taratibu zilizowekwa. Katika mwaka 2006/2007 Wizara imetekeleza yafuatayo:-

(a) Kusajili shule 160 zisizo za Serikali: Awali 7, Msingi 2, Awali na Msingi 63, Sekondari 82 na Vyuo vya Ualimu 6;

(b) Kuthibitisha maombi 164 ya Wenye shule na Meneja: Awali 2, Msingi 1, Awali na Msingi 59, Sekondari 96, Vyuo vya Ualimu 5 na Chuo cha Kidini 1;

(c) Kusajili shule za Sekondari 1,084 za Serikali zilizojengwa kwa nguvu za wananchi;

(d) Kutoa leseni 6,319 za kufundisha: Shahada ya Uzamili 44, Shahada ya Kwanza 152, Stashahada 26, Vyeti 22, Kidato cha 6 na Mafunzo ya Muda Mfupi 6,075;

(e) Kuendesha mafunzo kuhusu taratibu za usajili wa shule katika Halmashauri 4;

(f) Kukusanya taarifa za walimu walio kazini kutoka Halmashauri 33; na

(g) Kufanya utafiti wa Kimataifa wa awali kuhusu Ubora wa Elimu ya Msingi katika nchi 15 za Kusini mwa Afrika - "*Southern Africa Consortium for Monitoring Education Quality" (SACMEQ) 'Research Project III*' ambao umesaidia kuboresha zana za kufanyia utafiti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa vibali vya kuanzisha shule za Sekondari za Serikali 500 zinazojengwa kwa nguvu za wananchi na kusajili shule zisizo za Serikali;

(b) Kukusanya takwimu za Walimu walio kazini kwa ajili ya kuwasajili kutoka Halmashauri 47;

(c) Kufanya Utafiti wa Kimataifa kuhusu Ubora wa Elimu ya Msingi katika nchi 15 za Kusini mwa Afrika *'SACMEQ Research Project III';* na

(d) Kutoa ushauri kwa Mameneja na Wenye Shule kuhusu usajili wa shule katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Ruvuma, Morogoro, Arusha na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha elimu ya Msingi, Sekondari, Mafunzo ya Ualimu na Ufundi Stadi, Wizara yangu inatilia mkazo elimu kwa njia ya redio, huduma za Malezi na Ushauri, Elimu ya Mazingira na UKIMWI. Katika mwaka 2006/2007, Wizara ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa na kutangaza vipindi 52 vya Boresha Elimu, 52 vya ufundishaji kwa kutumia mbinu shirikishi na 432 vya masomo ya Kiingereza Maarifa ya Jamii, Kiswahili na Sayansi kwa madarasa ya V, VI na VII pamoja na Historia, Jiografia na Uraia Darasa la III na IV;

(b) Kuchapa na kusambaza nakala 150,000 za Mwongozo wa kufundisha Elimu ya Mazingira katika shule za Msingi na kutoa mafunzo kwa Walimu 164, wakaguzi wa shule 120 wa Kanda ya Mashariki, Kaskazini Magharibi na Magharibi kuhusu utumiaji wa Mwongozo;

(c) Kukamilisha uhariri wa vitini vya kufundishia Elimu ya Mazingira kulingana na Muhtasari wa Stadi za Kazi;

(d) Kuchapa nakala 10,000 za Mwongozo wa Ushauri Nasaha kwa shule za Sekondari na Vyuo vya Ualimu;

(e) Kutafsiri Mwongozo wa Ushauri Nasaha katika Lugha ya Kiswahili;

(f) Kukamilisha Andiko la Elimu Rika la UKIMWI kwa shule za sekondari;

(g) Kununua na kusambaza nakala 86,400 za vitabu vya Uelimishaji Rika, UKIMWI na Magonjwa ya Ngono;

(h) Kuchapa na kusambaza nakala 58,000 za vitabu vya kujikinga na UKIMWI katika shule za Msingi na Sekondari;

(i) Kutoa mafunzo ya Ushauri Nasaha kwa Walimu 520 wa Shule za Sekondari na Wakufunzi 201 wa Vyuo vya Ualimu toka kanda ya Ziwa na Magharibi; na

(j) Kuhakiki Mpango Mkakati wa Elimu ya UKIMWI 2003 - 2007 ili kuwa na Mpango Mkakati wa Elimu ya UKIMWI 2008 - 2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa na kutangaza vipindi 52 vya Boresha Elimu, vipindi 52 vya Ufundishaji kwa kutumia mbinu shirikishi na vipindi 480 vya masomo ya Kiingereza, Sayansi, Kiswahili kwa Darasa la V, VI na VII; Maarifa ya Jamii Darasa la VII na Historia, Jiografia na Uraia kwa Darasa la III, IV na V;

(b) Kuelimisha walimu wa shule za msingi 380 na wakaguzi wa shule za msingi 150 wa kanda za Nyanda za Juu, Kusini na Ziwa kuhusu utumiaji wa Mwongozo wa Elimu ya Mazingira;

(c) Kuchapa na kusambaza: (i) Mwongozo wa kufundishia Elimu ya Mazingira kwa shule za Msingi kulingana na muhtasari wa somo la stadi za kazi; (ii) Mwongozo wa kufundishia Elimu ya Mazingira na Ushauri Nasaha kwa shule za sekondari na Vyuo vya Ualimu; na (iii) Mwongozo wa Elimu Rika katika Shule za Sekondari.

(d) Kutoa mafunzo ya Ushauri Nasaha kwa wawezeshaji 500 wa shule za Msingi na 520 wa shule za Sekondari na Vyuo Vya Ualimu Kanda ya Ziwa na Magharibi;

(e) Kutathmini Mpango Mkakati wa Elimu ya UKIMWI 2003 - 2007 ili kuwa na Mpango Mkakati wa Elimu ya UKIMWI 2008 - 2012 na kukamilisha uandaaji wa Sera ya Elimu ya UKIMWI mahali pa kazi;

(f) Kutoa mafunzo ya ufuatiliaji wa Programu ya UKIMWI kwa Wakaguzi 250 wa Wilaya; na

(g) Kutoa mafunzo ya ufundishaji mada za UKIMWI kwa wawezeshaji 4,000 wa shule za Msingi na 1,000 wa shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya elimu ni muhimu katika kufikia malengo ya kutoa elimu bora. Ili kufikia azma hiyo Wizara yangu imeendelea kutayarisha programu na mipango ya muda mfupi, kati, na mrefu ya *sub*-sekta ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu, Ufundi na Elimu ya Watu Wazima kulingana na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha haya, katika mwaka 2006/2007 Wizara ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea na utafiti wa mwenendo wa mdondoko wa wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari, kukamilisha pendekezo la utafiti wa maendeleo ya taaluma ya uongozi kwa baadhi ya shule za Msingi pamoja na kufanya maandalizi ya awali ya utafiti kuhusu athari ya kutoza ada katika utoaji wa elimu ya Sekondari;

(b) Kufuatilia na kutathmini matumizi ya fedha na utoaji wa huduma za elimu na mafunzo katika shule za sekondari 380;

(c) Kuongeza maeneo ya kukusanya taarifa ili kuhusisha wadau wengi zaidi na kujumuisha Masuala Mtambuka katika kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995;

(d) Kukamilisha andiko la pili la Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II) 2007 - 2011;

(e) Kuandaa Mapitio ya Matumizi ya Fedha za Umma (*Public Expenditure Review* -PER) na Mpango wa Kati wa Matumizi ya Fedha (*Medium Term Expenditure Framework -MTEF*);

(f) Kutoa mafunzo ya matengenezo na utunzaji wa majengo na mazingira kwa walimu 72 kutoka shule 36 za Sekondari;

(g) Kutoa ithibati kwa vitabu 80 na vifaa vingine vya elimu vya kufundishia na kujifunzia;

(h) Kuweka mfumo mpya wa *EMIS - D6* kutoka mfumo wa zamani wa '*Cobol*' ili kuimarisha na kuboresha mfumo wa ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu na kumbukumbu;

(i) Kuchapa na kusambaza vitabu 5,000 vya '*Basic Education Statistics in Tanzania (BEST)* 2007';

(j) Kukarabati majengo ya shule 20 za Sekondari, ofisi za Makao Makuu, Ofisi 3 za kanda za Mpango wa Matengenezo na Vyuo 9 vya Ualimu;

(k) Kununua kompyuta 20 na vifuasi vyake na kufunga mtandao wa intaneti Maktaba Kuu ya Taifa; na

(l) kuandaa Mpango Mkakati wa Muda wa Kati kwa mwaka 2007/2008 - 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Mwaka 2007/2008. Katika mwaka 2007/2008, Wizara itatekeleza yafuatayo: -

(a) Kufanya mapitio ya andiko la MMES (2004 - 2009) linalozingatia upanuzi wa Kidato cha 5 na 6, na Vyuo vya Ualimu ili kukidhi mahitaji ya sasa yanayotokana na mafanikio ya upanuzi wa shule za sekondari hususan ngazi ya Kidato cha 1- 4;

(b) Kuendesha mafunzo ya matengenezo na utunzaji wa majengo na mazingira kwa wakuu wa Shule 30 na Vyuo vya Ualimu 10 ambavyo havikupatiwa mafunzo awamu ya kwanza;

(c) Kufuatilia na kutathmini matumizi ya fedha na utoaji wa huduma za elimu na mafunzo katika shule za sekondari 114, shule moja kutoka kila wilaya;

(d) Kuanzisha matumizi ya TEHAMA katika ofisi za Waratibu wa Elimu ya Sekondari na Maafisaelimu wa Wilaya;

(e) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 na kujumuisha masuala mtambuko;

(f) Kutoa ithibati kwa vitabu 80 vya elimu na zana za kufundishia na kujifunzia;

(g) Kukarabati majengo ya shule 30 za Sekondari za Serikali; Vyuo vya Ualimu Bunda, Butimba, Mtwara, Mandaka na Tarime; ofisi za Makao Makuu; ofisi za kanda ya Mashariki, Kati na Nyanda za Juu Kusini; vituo vya uchapaji vya kanda ya Kati na Mashariki; na ofisi za ukaguzi wa shule za wilaya 20;

(h) Kutathmini majengo ya shule 15 za Sekondari na kutayarisha hati za zabuni kwa ajili ya ukarabati;

(i) Kutoa mafunzo ya matumizi ya Miongozo ya MMES kwa Wakuu wa Shule na Wajumbe wa Bodi za Shule 900 katika shule mpya;

(j) Kufanya mapitio ya Matumizi ya Fedha za Umma na Mpango wa Kati wa Matumizi ya Fedha; na

(k) Kusanifu na kuanza ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa wadau wa Elimu wanapata na kuelewa majukumu ya Wizara ipasavyo, Wizara yangu kwa kupitia vyombo vya habari iliendelea kutoa taarifa ya majukumu, mipango, na programu mbalimbali zinazotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2006/2007, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa na kuratibu utoaji wa taarifa za elimu kwa vyombo vya habari na kutunza kumbukumbu za matukio ya elimu katika picha za video na mnato;

(b) Kutayarisha matangazo 40 ya redio na televisheni ili kuifahamisha jamii kuhusu mikakati, changamoto na mafanikio pamoja na kuhamasisha jamii kushiriki katika kutekeleza mipango ya elimu;

(c) Kuchapa na kusambaza nakala 330,000 za '*Ed-SDP Newsletter*' katika kanda 8 za elimu ili kuwaelimisha wadau na kuwahamasisha kushiriki katika utekelezaji wa mipango ya elimu;

(d) Kuandaa vipindi 50 vya redio na televisheni ili kuelezea Sera ya Elimu ya mwaka 1995 na utekelezaji wa programu za MMEM na MMES; na

(e) Kuandaa na kusambaza nakala 50,000 za kalenda, vipeperushi 20,000, mabango 10,000 na shajara 50,000 zenye taarifa na takwimu za utekelezaji wa programu za MMEM na MMES.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuandaa na kuratibu utoaji wa taarifa za elimu kwa vyombo vya habari ili kuelimisha jamii kuhusu maendeleo ya elimu na kutunza kumbukumbu;

(b) Kutayarisha matangazo 60 na vipindi 26 vya redio na televisheni ili kuelezea sera ya elimu na mafunzo na kuifahamisha jamii kuhusu mikakati, changamoto, mafanikio na kuhamasisha jamii kushiriki katika kutekeleza mipango ya elimu ikiwemo ya MMEM na MMES; na

(c) Kutafiti na kutathmini utoaji wa Habari za Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika vyombo vya Habari (*Communication Environment Scanning*).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake Wizara yangu pia inasimamia ajira na maslahi ya watumishi, sheria, kanuni na taratibu za utumishi. Aidha, Wizara inahusika na utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma, na kutoa elimu ya kuzuia maambukizi na kuandaa utaratibu wa kutoa huduma kwa wafanyakazi wenye Virusi Vya UKIMWI na wenye UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2006/2007. Katika mwaka 2006/2007, Wizara ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Kuajiri Walimu 7,872 wa shule za Sekondari, Vyuo vya Ualimu na watumishi 170 wasio walimu;

(b) Kuidhinisha vibali vya ajira kwa Walimu 330 raia wa kigeni kwa ajili ya shule zisizo za Serikali;

(c) Kushughulikia mafao ya uzeeni kwa watumishi 354 waliostaafu, kupandisha vyeo watumishi 545 na kuthibitisha kazini watumishi 127;

(d) Kuandaa Makisio ya Ikama na Bajeti ya Mishahara ya watumishi kwa mwaka 2007/2008;

(e) Kuratibu mafunzo ya watumishi ya: Shahada ya Uzamili 52, Stashahada ya Uzamili 53, Shahada 1,085, Cheti 8 na muda mfupi 23;

(f) Kuratibu matibabu ya magonjwa ambayo hayapo kwenye orodha ya mafao yatolewayo na Mfuko wa Bima ya Afya;

(g) Kuhakiki idadi ya watumishi kwa lengo la kuboresha kumbukumbu za watumishi;

(h) Kuandaa utaratibu wa jinsi ya kuwahudumia watumishi wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI na wanaougua UKIMWI;
(i) Kutoa mafunzo ya huduma kwa mteja kwa watumishi 360 kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma;

(j) Kuendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika kutoa huduma za usafi, ulinzi na mapokezi; na

(k) Kuandaa na kuratibu ushiriki katika michezo ya SHIMIWI na Bonanza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:

(a) Kuajiri walimu 14,490 na watumishi wasio walimu 397;

(b) Kuidhinisha maombi ya ajira za walimu 600 raia wa kigeni kwa ajili ya shule zisizo za Serikali;

(c) Kuthibitisha kazini watumishi 1,000 na kupandisha vyeo watumishi 10,486 ambao wamekaa katika madaraja waliyonayo kwa muda mrefu;

(d) Kuandaa na kuratibu mpango wa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi 2,110;

(e) Kufanya mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kukusanya maoni kuhusu utoaji wa huduma kwa wateja;

(f) Kuandaa mfumo mpya wa utunzaji wa kumbukumbu za watumishi kwa kutumia kompyuta;

(g) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wakuu wa shule/vyuo, wakaguzi wa shule na waratibu wa elimu ya Sekondari wa kanda za Kusini, Nyanda za Juu Kusini, Ziwa na

Magharibi kuhusu haki na maslahi ya watumishi, sheria, kanuni na taratibu za utumishi; na

(h) Kuratibu mipango ya kuzuia maambukizi na kuweka utaratibu wa kuanza kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI na wenye UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Wakala, Taasisi na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara yangu yanafanikisha utoaji wa elimu bora. Kila Taasisi na Baraza limetekeleza kazi zilizopangwa kwa kuzingatia malengo na mipango ya elimu kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mafunzo ya uongozi wa elimu, Wizara yangu hutoa mafunzo, huduma ya ushauri wa kitaalamu na kufanya utafiti katika masuala ya uongozi na uendeshaji wa taasisi za elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara imetekeleza yafuatayo:

(a) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu (*DEMA*): wanachuo 97 kati ya 100 wamehitimu na 148 kati ya 150 wanaendelea na mafunzo;

(b) Kutoa mafunzo ya uongozi kwa Maafisa Elimu Vifaa na Takwimu na Maafisa Elimu Taaluma 116 kati ya 120 ngazi ya Halmashauri kutoka mikoa ya Tabora, Pwani, Morogoro, Mara na Manyara;

(c) Kutoa mafunzo ya uongozi kwa washiriki 1,351 kati ya 1,400 wa Timu za Menejimenti za Shule za Sekondari katika mikoa ya Pwani, Singida, Rukwa, Lindi na Kigoma;

(d) Kutoa mafunzo ya awali ya Uongozi wa elimu kwa Wakuu wapya 450 wa Shule za Sekondari katika vituo vya kanda za elimu;

(e) Kutoa mafunzo ya mwezi mmoja ya Uongozi wa Elimu kwa Wakuu 120 wa Shule za Sekondari waliokusudiwa;

(f) Kutoa mafunzo ya Uongozi wa Elimu kwa Waratibu Elimu Kata 746 kati ya 2,300 kutoka Halmashauri za Mpwapwa, Singida (V), Singida (M), Nachingwea, Mtwara (V), Mtwara Mikindani, Mbinga, Urambo, Nzega, Kasulu, Shinyanga (V), Shinyanga (M), Kishapu, Sumbawanga (V), Sumbawanga (M), Mbeya (V), Mbeya (J), Njombe, Iringa (V), Iringa (M), Kilolo, Kilombero, Rufiji, Same, Lushoto, Monduli, Arumeru, Karagwe, Musoma (V), Musoma (M), Tarime na Geita;

(g) Kutoa mafunzo ya Uongozi wa Elimu ngazi ya cheti kwa Walimu Wakuu wa shule za Msingi 127 kati ya 1,000 waliokusudiwa;

(h) Kugharimia mafunzo kwa watumishi 16 wa *ADEM:* Shahada na Stashahada ya Uzamili 4 na mafunzo ya muda mfupi 12;

(i) Kuendelea kufanya tafiti 4 za uongozi na uboreshaji wa taasisi za elimu kwa ushirikiano na Malawi, Uganda na Afrika ya Kusini; na

(j) Kukarabati majengo na kuimarisha mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa Viongozi 300 wa ngazi mbalimbali za Elimu; na

(b) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa wakuu wapya 670 wa shule za sekondari, Timu za Menejimenti 1,500 za Shule za Sekondari, Wakaguzi wa shule 114, Waratibu Elimu Kata 1,490, Waratibu wa Elimu ya Sekondari 114 na Maafisaelimu Taaluma na Maafisaelimu Vifaa na Takwimu 180 wa Halmashauri zote kwa kushirikiana na *JICA*.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (*IAE*). Katika jitihada za kufuta ujinga na kujiendeleza katika mfumo usio rasmi, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa vijana nje ya shule, wafanyakazi na watu wazima ambao hawakupata nafasi ya kujiendeleza katika mfumo rasmi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara imetekeleza yafuatayo:

(a) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Juu kwa walengwa 182 na Stashahada ya Kawaida kwa walengwa 261;

(b) Kutoa elimu ya sekondari kwa walioikosa kwa njia ya ana kwa ana na Elimu Masafa kwa walengwa 16,801;

(c) Kuchapa na kusambaza moduli 36 za masomo ya Elimu Masafa Hatua ya II zenye nakala 123,000 za masomo ya Kiingereza, Kiswahili, Jiografia, Historia, Hesabu, Biolojia na Uraia;

(d) Kuchapa majarida ya: *Studies in Adult Education (SAED)* Na. 63, *Journal of Adult Education in Tanzania (JAET)* Na. 15 na *Alumni Newsletter;*

(e) Kutoa mafunzo ya uratibu, usimamizi na menejimenti ya vituo vya MEMKWA na MUKEJA kwa Waratibu Elimu Kata 300 na Walimu Wakuu wa Shule za Msingi 600;

(f) Kutoa mafunzo ya Cheti cha Sheria kwa wanachuo 190;

(g) Kutoa mafunzo ya kujiendeleza kwa wafanyakazi katika ngazi ya Shahada ya Uzamili 3, Stashahada ya juu 3, Stashahada ya Kompyuta na Uongozi 2, Masomo ya Sekondari 21 na Mafunzo ya muda mfupi 85;

(h) Kununua viwanja vya kujenga ofisi katika mikoa ya Mwanza na Manyara;

(i) Kufunga mtandao wa intaneti Makao Makuu (*IAE)*;

(j) Kuajiri watumishi 35; na

(k) Kununua magari kwa mikoa ya Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Ruvuma na Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Juu kwa walengwa 244, Stashahada ya kawaida kwa walengwa 293 na Cheti cha Sheria kwa walengwa 225;

(b) Kutoa elimu ya sekondari kwa wanafunzi 15,000 walioikosa kwa njia ya ana kwa ana na Elimu Masafa na kutathmini maendeleo ya utekelezaji wa programu ya Elimu Masafa katika mikoa yote 21;

(c) Kuandika na kutalii masomo ya utangulizi ya Uraia, Kiingereza, Hesabu na Ufundi na masomo ya English, Kiswahili, Jiografia na Historia Hatua ya III;

(d) Kutoa Elimu ya UKIMWI kwa wafanyakazi wote wa TEWW pamoja na wanafunzi wa Stashahada ya Juu na Kawaida na kuanzisha Kitengo cha Ushauri na Unasihi na huduma kwa wenye VVU na UKIMWI;

(e) Kujenga uwezo wa uratibu, usimamizi na menejimenti ya vituo vya MEMKWA na MUKEJA kwa Waratibu Elimu Kata na Walimu Wakuu wa shule za Msingi kwa walengwa 480;

(f) Kugharimia mafunzo kwa watumishi: Shahada ya Udaktari wa Falsafa 2, Shahada ya Uzamili 4, Elimu ya Sekondari 40 na Mafunzo ya kitaaluma ya muda mfupi 100;

(g) Kununua viwanja na nyumba katika mikoa ya Ruvuma, Mara, Kilimanjaro na kukarabati jengo la Dodoma na Makao Makuu, Dar es salaam;

(h) Kufunga mtandao wa intaneti katika vituo vya Mwanza, Ruvuma, Arusha, Dodoma na Mbeya ili kuboresha mfumo wa kuhifadhi, kutunza na kutumia taarifa na takwimu za elimu; na

(i) Kuajiri wafanyakazi wapya 47 na kununua magari 5 kwa vituo vya Rukwa, Tanga, Singida, Mtwara na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Elimu Tanzania, katika kutoa elimu iliyo bora na inayoendana na wakati, Wizara yangu inaendelea kuimarisha mitaala na mihtasari ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu na Elimu Maalumu. Aidha, Wizara inaendelea kubuni na kufaragua vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea na ukuzaji wa mitaala kwa ngazi mbalimbali kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendesha mikutano 10 ya majopo ya masomo katika elimu ya Msingi, Sekondari na Ualimu;

(b) Kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia zinazoendana na mtaala ulioboreshwa kwa ajili ya shule za elimu ya awali;

(c) Kuandaa mtaala na mihtasari 27 ya ualimu ngazi ya Stashahada ili iendane na mtaala wa Sekondari ulioboreshwa;

(d) Kuandika mwongozo wa uandishi wa moduli 24 za kufundishia masomo ya Sekondari ya Kidato cha I - 4 kulingana na mtaala uliorekebishwa;

(e) Kufuatilia utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Msingi katika kanda zote za elimu ili kupata taarifa kwa ajili ya uboreshaji;

(f) Kuhakiki vitabu 24 vya MEMKWA vya mwaka wa tatu kwa Kundirika la Kwanza na la Pili;

(g) Kutoa mafunzo kwa wawezeshaji 30 kwa ajili ya upanuzi wa shughuli za MEMKWA katika wilaya ya Makete;

(h) Kutoa mafunzo kwa Wakuza mitaala 25 na wafanyakazi waendeshaji 10 wa *TIE* katika maeneo yao ya kitaalamu;

(i) Kuendesha semina tatu za kitaalamu kwa wafanyakazi 85 wa *TIE* kuhusu utumiaji wa TEHAMA;

(j) Kuchapa na kusambaza kalenda ya mwaka 2007 na kuanzisha utumiaji wa tovuti ya *TIE* ili kuelimisha jamii kuhusu kazi za Taasisi;

(k) Kuandika mihtasari ya Historia, Uraia na Jiografia na vitabu vya masomo hayo kwa Darasa la III na kurekebisha mihtasari ya *Physics* na *Chemistry* kwa ajili ya shule za Sekondari Kidato cha 1 - 4;

(l) Kufanya utafiti ili kupata maoni ya wadau kuhusu mihtasari ya masomo ya Sekondari ya Kidato cha 5 na 6 na kuandaa mihtasari ya masomo hayo;

(m) Kukusanya maoni ya wadau na kuandaa mwongozo wa kurekebisha masomo ya michepuo ili kuainisha masomo ya Ufundi, Kilimo, Biashara, Sayansi Kimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi yanayotolewa na VETA;

(n) Kurekebisha mihtasari ya Elimu Maalumu (Ulemavu wa Akili) ngazi ya Elimu ya Msingi ili iendane na mabadiliko ya mtaala wa Elimu ya Msingi ulioboreshwa; na

(o) Kununua gari 1 kwa ajili ya kuimarisha kazi za *TIE.*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kurekebisha mtaala na kuandika mihtasari ya ualimu ngazi ya cheti ili iendane na mabadiliko ya mitaala;

(b) Kubuni na kuandaa mtaala wa mafunzo ya ualimu unaotumia teknolojia ya kisasa (*e-learning*) ili kuwafikia wadau wengi;

(c) Kufanya utafiti kuhusu hali na matumizi ya maabara na ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa vitendo katika shule za sekondari;

(d) Kutayarisha miongozo ya kufundishia elimu ya UKIMWI kwa shule za Sekondari na kufanya majaribio ya miongozo ya elimu ya Awali na elimu ya Msingi;

(e) Kukuza uwezo wa *TIE* kwa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi 20 ili kuinua viwango vyao vya taaluma na kununua gari moja kwa lengo la kuboresha ufanisi;

(f) Kuanza ujenzi wa kituo cha kutolea mafunzo kwa walimu na wadau wa elimu katika kiwanja cha *TIE* Mikocheni;

(g) Kuandaa na kuendesha mafunzo ya wawezeshaji 100 wa Kitaifa wa masomo ya ualimu ngazi ya Stashahada;

(h) Kuanzisha mfumo wa kompyuta katika kitengo cha Rasilimali Watu na Maktaba; na

(i) Kununua vifaa maalumu kwa Wenye Ulemavu kwa ajili ya kuwajengea uwezo walimu wa Elimu Maalumu waweze kutumia miongozo ya kufundishia wenye ulemavu iliyoandaliwa kulingana na mtaala mpya.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina jukumu la kuanzisha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma, Shule, Mashirika na Taasisi nyingine; kutoa mafunzo na kuendesha mitihani ya taaluma; kutoa ushauri wa kuboresha huduma kwa wadau; kuhifadhi machapisho ya Taifa kwa ajili ya kizazi kijacho na kushiriki kikamilifu katika juhudi za kuimarisha programu za Elimu ya Msingi, Sekondari, Ualimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2006/2007. Katika mwaka 2006/2007, Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kuongeza idadi ya machapisho kutoka 796,428 hadi 836,428 katika mikoa 18;

(b) Kutoa Matoleo 2 ya "*Tanzania National Bibliography*", ambapo Toleo la 1999 - 2001 limekamilika na Toleo la 2002 - 2004 linaendelea kuandaliwa;

(c) Kuendeleza ujenzi wa maktaba ya mkoa wa Dodoma ambapo hatua ya kwanza na ya pili imekamilika pamoja na kununua samani;

(d) Kuendeleza ujenzi wa Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka Bagamoyo kwa kujenga madarasa, maabara ya TEHAMA na ofisi za utawala. Awamu ya kwanza imefikia asilimia 97;

(e) Kuendesha vipindi vya watoto vya hadithi, kazi za mikono, usanii, uandishi, uchoraji, utumiaji wa kompyuta na kuandaa vipindi vya maonesho katika televisheni;

(f) Kupata na kumiliki viwanja vya kujenga maktaba katika mikoa ya Singida na Pwani; na

(g) Kusambaza machapisho 440 yanayohusu VVU na UKIMWI na kuendesha semina kuhusu UKIMWI, madawa ya kulevya, pombe na sigara katika mikoa ya Kigoma, Mbeya na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008 Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuongeza idadi ya machapisho kutoka 836,428 hadi 956,428 katika mikoa 18;

(b) Kutoa Matoleo 2 ya "Tanzania *National Bibliography*", Toleo la 2002 - 2004 na Toleo la 2005 - 2006 ili kuwapa wananchi hamasa ya kushiriki katika uandishi wa vitabu;

(c) Kukamilisha michoro ya ujenzi wa ukumbi wa mikutano katika maktaba ya mkoa wa Dodoma, kutayarisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa maktaba ya mkoa wa Singida na kukarabati majengo ya maktaba za mikoa ya Tanga, Mbeya, Ruvuma, Mtwara na Lindi;

(d) Kuendeleza ujenzi wa Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka Bagamoyo;

(e) Kuimarisha huduma za maktaba kwa watoto kwa kuanzisha "*Children Multimedia Resource Centres*" katika mikoa ya Mbeya, Morogoro, Mwanza, Tanga, Iringa na Dodoma;

(f) Kununua magari 2 kwa ajili ya kusaidia kusambaza huduma za maktaba kwenye sehemu zisizo na maktaba;

(g) Kutoa mafunzo ya ukutubi na fani nyingine kwa watumishi 20 wa Bodi na wanafunzi 129 kutoka taasisi na mashirika katika ngazi za Cheti, Stashahada na mafunzo ya muda mfupi;

(h) Kuandaa Mpango Mkakati wa Bodi ya Maktaba wa mwaka 2007 - 2012;

(i) Kuongeza nyenzo za kusomea kwa wasioona katika Maktaba Kuu zikiwemo kompyuta zinazoongea na mashine za kuandikia nukta nundu (*braille*); na

(j) Kuendesha Tamasha la Wiki ya Vitabu na Hema la Kusomea Jumuiya katika vituo 34 vya huduma kwa kushirikiana na wadau ili kuhamasisha tabia ya kupenda kusoma vitabu.

Mheshimiwa Spika, katika kupima maendeleo ya elimu itolewayo nchini Wizara inasimamia na kuendesha Mitihani ya Maarifa, Mitihani ya Kitaifa ya Kumaliza Elimu ya Msingi, Sekondari Kidato cha 4 na 6, Ufundi na Ualimu Daraja A na Stashahada. Aidha, husimamia mitihani inayotolewa na Bodi za Nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara ilitekeleza malengo yafuatayo:

(a) Kuendesha Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi, Ualimu, Ufundi, Kidato cha 4 na 6 na Maarifa;

(b) Kusimamia uendeshaji wa mitihani itolewayo na Bodi za Nje ya Nchi;

(c) Kupanua jengo la kitengo cha chapa na uchapishaji na kununua baadhi ya vifaa kwa ajili ya kitengo hicho;

(d) Kupata kiwanja na hatimiliki kwa ajili ya ofisi za Baraza la Mitihani, Zanzibar;

(e) Kuendelea kujenga kituo cha kusahihishia Mitihani, Mbezi Wani; na

(f) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi yenye lengo la kupunguza maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mtihani wa Kitaifa wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2006, watahiniwa 664,263 walifanya mtihani. Waliofaulu walikuwa 468,279 sawa na asilimia 70.5 ambapo wasichana walikuwa 210,945 sawa na asilimia 45.0 na wavulana walikuwa 257,334 sawa na asilimia 55.0. Ikilinganishwa na mwaka 2005 ambapo watahiniwa 493,946 walifanya mtihani, waliofaulu walikuwa 305,062 sawa na asilimia 61.8, ambapo wasichana walikuwa 131,312 sawa na asilimia 43.0 na wavulana

walikuwa 173,750 sawa na asilimia 57.0. Takwimu zinaonesha kuwa kuanzia mwaka 2000 idadi ya watahiniwa waliofaulu imekuwa ikiongezeka (Kielelezo Na. 3).

Mheshimiwa Spika, katika Mtihani wa Kidato cha 4 mwaka 2006, watahiniwa 141,728 walifanya mtihani. Waliofaulu walikuwa 116,647 sawa na asilimia 82.3 ambapo wasichana walikuwa 52,152 sawa na asilimia 79.4 ya wasichana waliofanya mtihani huo na wavulana walikuwa 64,495 sawa na asilimia 84.8 ya wavulana waliofanya mtihani. Kati ya watahiniwa wote wa mwaka 2006, watahiniwa waliofaulu katika Daraja I - III walikuwa 31,305 sawa na asilimia 22.1 ikilinganishwa na 28,653 sawa na asilimia 23.5 mwaka 2005 (kielelezo Na. 4).

Mheshimiwa Spika, katika Mtihani wa Kidato cha 6 mwaka 2007, kati ya watahiniwa 33,522 waliofanya mtihani, wasichana walikuwa 11,844 sawa na asilimia 35.3 ya watahiniwa wote na wavulana walikuwa 21,678 sawa na asilimia 64.7 ya watahiniwa wote. Waliofaulu mwaka 2007 walikuwa 29,239 sawa na asilimia 87.2 ambapo wasichana waliofaulu walikuwa 10,470 sawa na asilimia 88.4 ya wasichana waliofanya mtihani huo na wavulana waliofaulu walikuwa 18,769 sawa na asilimia 86.6 ya wavulana waliofanya mtihani (kielelezo Na. 5).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, mitihani mingine iliyoendeshwa na Wizara ilikuwa ni pamoja na mitihani ya Ualimu na Ufundi. Katika mitihani ya Ualimu ya mwaka 2006/2007 waliofaulu ni watahiniwa 37,217 kati ya 41,005. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 90.8 ya waliofanya mtihani.

Mwaka 2005/2006 watahiniwa 11,269 walifanya mtihani na kati yao 11,092 sawa na asilimia 98.4 walifaulu. Katika mitihani ya Elimu ya Ufundi ya mwaka 2006 waliofaulu walikuwa 313 kati ya watahiniwa 663 waliofanya mtihani. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 47.2.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara ilisimamia mitihani ya nje kwa niaba ya Taasisi za Uingereza zifuatazo: *'University of London', 'Lincolnshire Institute of Purchasing and Supply', 'Chartered Institute of Marketing', 'The Royal Institute of Chartered Surveyors', 'The Institute of Chartered Secretaries and Administrators', 'Association of Chartered Certified Accountants', 'The Association of International Accountants', 'The Institute of Chartered Shipbrokers'* na *'London Association Board of Royal School of Music'.*

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji huo ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kuanzia mwaka 2005 mitihani yote ya Kitaifa ya Darasa la VII, Kidato cha 4 na 6 iliendeshwa kwa amani na utulivu. Hata hivyo, yalikuwepo matukio ya udanganyifu katika mtihani kwenye baadhi ya vituo na hatua zilichukuliwa kwa wahusika kwa mujibu wa sheria na kanuni za uendeshaji wa mitihani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/08, Wizara itatekeleza yafuatayo:

(a) Kuendesha Mtihani wa Maarifa, Mitihani ya Kumaliza Elimu ya Msingi; Mitihani ya Kidato cha 4 na 6, Mitihani ya Ualimu Daraja A na Stashahada;

(b) Kuboresha mfumo wa usajili na taratibu za uendeshaji mitihani;

(c) Kusimamia Mitihani ya Nje inayofanywa na watahiniwa binafsi hapa nchini;

(d) Kununua Kompyuta 32, samani na kukarabati majengo ya ofisi za Baraza;

(e) Kutayarisha michoro na kufanya tathmini ya gharama za ujenzi wa ofisi ya Zanzibar;

(f) Kuendelea na ujenzi wa kituo cha kusahihishia Mitihani, Mbezi Wani;

(g) Kuongeza wafanyakazi 25 na kuwapatia mafunzo ili kumudu ongezeko kubwa la watahiniwa na kuimarisha shughuli za mitihani; na

(h) Kutoa mafunzo ya elimu ya Virusi Vya UKIMWI pamoja na kuweka utaratibu wa kutoa huduma na kuwahudumia wafanyakazi wenye VVU na wenye UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mahitaji makubwa ya mafunzo ya Ufundi Stadi, Wizara yangu ina mpango wa kupanua na kuimarisha mafunzo hayo ili kutoa stadi za kazi zinazohitajika kuwawezesha vijana kujiajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu imetekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa Mafunzo ya Ufundi Stadi ya muda mfupi na mrefu katika vyuo vya VETA kwa vijana 18,788 ambapo asilimia 27 kati yao ni wasichana. Idadi ya waliopatiwa mafunzo imeongezeka kwa asilimia 14 kulinganisha na wale wa mwaka 2005/2006. Aidha, vijana 54,623 wamepatiwa mafunzo ya stadi za ufundi mbalimbali katika vyuo vya ufundi vya asasi zisizo za serikali na za watu binafsi ambapo asilimia 48 kati yao ni wasichana;

(b) Kutayarisha mkakati wa utekelezaji wa mpango wa uanzishaji wa vyuo vya ufundi stadi katika kila wilaya kwa kuunda kamati maalumu ya kufanya tathmini ya mahitaji ya stadi za kazi katika soko la ajira katika wilaya 24 ambazo hazina vyuo vya Ufundi Stadi;

(c) Kusaini mkataba wa ununuzi wa vifaa kwa ajili ya vyuo vya ufundi stadi vya Mara, Kagera, Songea, Mikumi, Arusha na Dakawa;

(d) Kukarabati na kupanua vyuo vya Ufundi Stadi vya Shinyanga, Mpanda, Tabora, Ulyankulu, Singida na Ujenzi wa Chuo kipya cha Mafunzo ya Hoteli na Utalii Arusha (Njiro);

(e) Kukamilisha taratibu za kupata makandarasi wa kujenga vyuo vya Ufundi Stadi vya Lindi, Manyara, Pwani na Dar es Salaam;

(f) Kutoa ruzuku kwa Vyuo na asasi zisizo za Serikali katika kanda za Dar es Salaam, Ziwa, Magharibi, Kusini Mashariki, Mashariki, Nyanda za Juu, Kaskazini, Kusini Magharibi na Kati;

(g) Kufanya tathmini ya mahitaji ya soko la ajira katika sekta ya ujenzi;

(h) Kuboresha mitaala ya mafunzo kisekta iendane na soko la ajira ambapo mtaala wa sekta ya Hoteli na Utalii umekamilika. Aidha, marekebisho ya mitaala ya sekta ya uzalishaji yameanza;

(i) Kutoa mafunzo ya taaluma kwa walimu 140 wa ufundi stadi;

(j) Kutayarisha Andiko la Awali (*Concept Paper*) la kuwezesha kupata msaada kutoka Benki ya Dunia kwa ajili kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi;

(k) Kuendesha mitihani ya Ufundi Stadi kwa washiriki 34,731 ambapo 26,855 sawa na asilimia 77.3 wamefaulu. Aidha, washiriki 3,241 walifanya mitihani ya Biashara (*NABE*) na 3,032 sawa na asilimia 93.5 walifaulu;

(l) Kuendesha mitihani ya Ufundi Stadi katika mfumo wa mafunzo yanayolenga stadi za kazi ambapo wanafunzi 7,800 walifanya mitihani na wanafunzi 6,312 sawa na asilimia 80.9 walifaulu;

(m) Kutoa mafunzo ya Ufundi Stadi kwa wanafunzi 102 wenye ulemavu ikilinganishwa na wanafunzi 90 wa mwaka 2005/2006; na

(n) Kuimarisha ushirikiano na Zanzibar katika mafunzo ya Ufundi Stadi kwa kuanzisha ushirikiano katika mafunzo ya viwandani kwa Walimu wa Ufundi Stadi kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutayarisha Andiko la Mradi wa Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika kila wilaya na kuaandaa programu ya Kitaifa ya utekelezaji wa mradi;

(b) Kutathmini ajira kwa wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi ili kupima ubora wa mafunzo yanayotolewa;

(c) Kufunga vifaa vipya katika karakana za mafunzo za vyuo vya Kagera, Mara, Songea, Mikumi, Arusha na Dakawa na kuendeleza ukarabati wa vyuo vya Shinyanga, Mpanda, Tabora na Ulyankulu;

(d) Kuanza ujenzi wa vyuo vipya vya Lindi, Pwani, Manyara, Dar es Salaam, Chuo cha Mafunzo ya Hoteli na Utalii cha Arusha (Njiro) na kuendeleza ujenzi wa chuo cha Singida;

(e) Kutoa ruzuku kwa vyuo na asasi zisizo za Serikali ili viongeze ubora na nafasi za mafunzo ya ufundi stadi na kujenga uwezo wa walimu;

(f) Kutoa mafunzo ya taaluma kwa walimu wa Ufundi Stadi, 60 na mafunzo ya ualimu kwa walimu 140 wa Ufundi Stadi, kukuza na kuimarisha mafunzo kwa sekta isiyo rasmi pamoja na kuimarisha mitaala;

(g) Kukamilisha Mwongozo wa Kitaifa na kuanza kutoa motisha kwa waajiri wanaolipa *'Skills and Development Lev*y' kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wao; na

(h) Kuandaa utaratibu utakaowezesha wahitimu wa mafunzo ya Ufundi Stadi kuendelea na elimu na mafunzo ya juu kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE)*.

Mheshimiwa Spika, changamoto - katika kutekeleza malengo, mipango na programu mbalimbali za elimu zilizopangwa, Wizara yangu kwa mwaka 2006/2007 ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(a) Mafanikio makubwa ya ujenzi wa shule za sekondari zinazojengwa kutokana na mwitikio mkubwa wa wananchi yamesababisha mahitaji makubwa ya walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, nyumba za walimu, maabara, maktaba, madarasa na majengo ya utawala;

(b) Baadhi ya wanafunzi kuishi mbali na shule hali inayoweza kusababisha ongezeko la mdondoko wa wanafunzi ikiwa ni pamoja na kupata mimba hivyo kusababisha mahitaji makubwa ya hosteli;

(c) Elimu kwa wenye mahitaji maalumu kutotolewa kikamilifu kutokana na uhaba wa wataalamu, vifaa, nyenzo za kufundishia na kujifunzia na miundombinu;

(d) Uwezo mdogo wa kukidhi mahitaji ya mafunzo ya ufundi kulingana na mahitaji ya soko la ajira;

(e) Kuendelea kuwepo kwa idadi kubwa ya watu wazima wasiojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu;

(f) Mahitaji makubwa ya wataalam, vifaa na miundombinu ya kukidhi matumizi ya TEHAMA katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji fanisi na kutunza kumbukumbu;

(g) Urasimu ndani ya ajira ya walimu kutokana na kuhudumiwa na mamlaka zaidi ya moja na hivyo kuathiri huduma kwa walimu; na

(h) UKIMWI bado ni tishio la maisha ya Watanzania wote ambapo Sekta ya Elimu nayo imeathirika.

Mheshimiwa Spika, maamuzi muhimu - katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa kipaumbele katika ujenzi wa nyumba za walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na mafunzo kazini;

(b) Kuwa na andiko la MMES kwa lengo la kuzingatia upanuzi wa shule za Kidato cha 5 na 6 na Vyuo vya Ualimu ili kukidhi mahitaji ya sasa;

(c) Kuongeza idadi ya walimu na kuanzisha stashahada ya Ualimu ya mwaka mmoja Chuoni na mwaka wa pili kazini;

(d) Kuwa na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa utoaji wa elimu kwa wenye mahitaji maalumu;

(e) Kuimarisha shule za sekondari za kitaifa zilizopo na kuwa na Mpango Mkakati wa ujenzi wa shule mpya za Kitaifa ili kuweka misingi imara ya umoja wa Kitaifa kwa wanafunzi;

(f) Kuimarisha michezo shuleni ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuwa na shule za mchepuo wa michezo na kuendeleza mashindano; *(Makofi)*

(g) Kuanzisha na kuendeleza matumizi ya TEHAMA katika Wizara, Taasisi na asasi zake pamoja na Mikoa na Halmashauri;

(h) Kuangalia uwezekano wa kuwa na chombo kimoja cha ajira na huduma kwa walimu kwa lengo la kuboresha huduma;

(i) Kuandaa utaratibu wa kutoa huduma na faraja kwa watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI;

(j) Kuandaa Mpango Mkakati wa kuendeleza EWW; na

(k) Kuibua mjadala wa Kitaifa kuhusu tatizo la mimba kwa wanafunzi, kukazia sheria ya kuwaadhibu wanaowapa mimba wanafunzi na kuangalia uwezekano wa kuwarejesha shuleni wasichana baada ya kujifungua (*Re-entry Policy*). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wote kwa kuitikia vyema wito wa Serikali wa kuchangia elimu kwa hali na mali. Mwitikio huo unatoa matumaini ya kuleta maendeleo haraka kuliko ilivyotegemewa. Aidha, nawapongeza Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Viongozi wote wa ngazi mbalimbali

wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Madiwani kwa kusimamia vizuri na kushiriki kwao katika kufanikisha upanuzi wa Elimu ya Sekondari. Kipindi hiki cha mafanikio kinastahili kuitwa kipindi cha mageuzi ya Elimu ya Sekondari. Tunawaomba juhudi za ujenzi wa vyumba vya madarasa ziendelee kwa kuwa wanafunzi wanapanda madarasa na kuzidi kuongezeka kwa idadi mwaka hadi mwaka. Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuboresha elimu. Aidha, natoa wito kwa watendaji kuwapanga wanafunzi karibu na nyumbani kadri inavyowezekana ili kupunguza mwendo mrefu kwa wanafunzi kwenda shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za pekee kwa Wahisani mbalimbali kwa kuchangia utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Wahisani hao ni Uswidi, Uingereza, Ufaransa, *Ireland, Japan, Norway, Finland, Canada,* Uholanzi, Ujerumani, China, *Cuba*, Jamhuri ya Watu wa Korea, Ubelgiji na Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*). Aidha, mashirika yaliyochangia ni pamoja na Benki ya Dunia (*WB), WFP, UNICEF, UNESCO, ILO, UNFPA, UNDP,* Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB), NORAD, GTZ, DFID, SIDA (Sweden), CIDA (Canada), JICA, USAID, JOVC, VSO, CELTEL, CBP, OPEC, DANIDA, Barclays Bank, NMB, CRDB, NBC, Peace Corps, Book Aid International, Aga Khan Education Foundation, Plan International, Sight Servers International, UNAIDS,* World *Vision, Irish Aid, Care International, Oxfam* na mashirika mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na misaada hiyo, utekelezaji wa Mipango ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka 2006/2007 haungefanikiwa na kukamilika katika kiwango nilichoelezea bila jitihada, ushirikiano na uongozi wa pamoja katika Wizara yangu. Natoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Wakurugenzi wote wa Idara zote, Viongozi wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi katika ngazi mbalimbali, walimu na wafanyakazi wote wa Wizara yangu kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na katika maandalizi ya Bajeti hii. Pia natoa shukrani zangu pia kwa Wenyeviti, Wakurugenzi Watendaji, Makatibu Watendaji na Wajumbe wa Mabaraza na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara yangu na Wafanyakazi wote katika ngazi mbalimbali kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuimarisha na kuendeleza Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Aidha, natoa shukurani na pongezi kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Elimu la Taifa (*National Education Advisory Council*), Uongozi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Chama cha Mameneja na Wamiliki wa Shule Zisizo za Serikali *(TAMONGSCO*), Chama cha Wachapaji na Asasi za Kiraia (*Civil Society*), kwa ushirikiano wao mzuri na ari yao ya kushirikiana na Wizara katika kutatua matatizo mbalimbali. Napenda kuwashukuru viongozi wa matawi ya *TUGHE* na CWT Makao Makuu ya Wizara kwa ushirikiano na ushauri wao katika kushughulikia masuala ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza yote hayo, naomba sasa Bunge lako lijadili hoja yangu pamoja na kuzingatia Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya shilingi 265,679,865,700 ili kuwezesha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutekeleza mipango ya mwaka 2007/2008. Kati ya fedha hizo: (a) Shilingi 155,447,119,000 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya

Ufundi; na (b) Shilingi 110,232,746,700 zinaombwa kwa ajili ya Mipango ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA**: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, kabla hatujaendelea na shughuli inayofuata ninalo tangazo. Mbunge wa Mkuranga Mheshimiwa Adam Malima na mwenziwe Mhe. Idd Azzan wameniomba eti niwape pole Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Missanga, Mheshimiwa Mudhihir, Mheshimiwa Stanley Kevela, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi na wenzao wengi sana kwa maafa waliyoyapata jana kule Morogoro. (*Makofi)*

Mimi siyaelewi maafa haya lakini kwa kuwa mimi ni kiungo cha kuwasilisha mambo ya Wabunge napenda kuwapa pole pia kwa msiba huo na kuendelea kuwapongeza Mheshimiwa Mbunge Mohamed Dewji wa Singida Mjini na Prof. Juma Kapuya, Waziri wetu wa Ulinzi na Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa *Chief Whip* na Prof. Sarungi na wenzao wote. Niliona nitoe tangazo hilo kwa sababu ni wakati wake. Baada ya hayo Waheshimiwa Wabunge nina udhuru kidogo ningemwomba Mheshimiwa Naibu Spika, aje aendeshe sehemu iliyobaki ya shughuli hizi.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge na mimi naungana mkono na kuwapa pole na hongera wanaohusika. Mimi sijui kitu. Baada ya hapo ninamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' – MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu Utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2006/2007, na malengo ya mwaka wa fedha wa 2007/2008 kwa mujibu wa Kanuni ya 81 (1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwa niaba ya Kamati kutoa pole kwa Wazazi,ndugu, jamaa na marafiki wote, kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi. *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilipata muda wa kutosha kufikiria na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007 na pia kupitia malengo na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 na kutoa maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi 'MMEM' ulilenga kuwapeleka Shule Watoto wote wenye umri wa kwenda Shule ili wapate elimu bora ya Msingi na umeleta mafanikio makubwa katika maeneo yafuatayo:- Kuongeza idadi ya wanafunzi katika shule za Msingi kufikia milioni 7.9 mwaka 2006; Kuongezeka kwa asilimia ya wanaofaulu mtihani wa darasa la saba kila mwaka kufikia asilimia 70.48 mwaka 2006; Kuongezeka kwa asilimia ya wanaochaguliwa kwenda Sekondari kama ilivyo kwenye Taarifa ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafaniko haya yaliyoelezwa na Waziri yanaitaka Serikali na jamii nzima kujipanga upya katika kuendeleza, kufanikisha na kulinda mafanikio haya katika maeneo yafuatayo:- Tunahitaji kujenga majengo yote muhimu ya Madarasa, Ofisi za Walimu, Vyoo na msisitizo wa pekee sasa uende katika kujenga nyumba za Walimu mashuleni; Serikali ielekeze nguvu zake katika kugawa fedha za ujenzi wa nyumba za Walimu katika maeneo na jamii zilizo nyuma katika maendeleo ya Elimu kutokana na sababu mbalimbali za jiografia na historia ya nchi yetu, ili kuleta uwiano mzuri wa upatikanaji wa Elimu; Tunahitaji kuwa na Walimu wenye sifa zinazotakiwa katika kutoa elimu bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza malengo ya elimu, tunaipongeza Serikali kwa maamuzi yake katika maeneo mawili yafuatayo:-

(i) Kwa kukubali ushauri wa Kamati ya Huduma za Jamii, Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla wa kuiweka Sekta ya Elimu kuwa ya kupaumblele namba moja kwenye bajeti ya Serikali ya 2007/2008 kwa kuitengea asilimia 18 ambayo ni kubwa kuliko Sekta zote za kipaumbele Kitaifa kama kielelezo kifuatacho kinavyoonyesha.

| **Sekta** | **Bajeti ya 2007/2008** | **% ya Bajeti** |
|---|---|---|
| Elimu | Trilioni 1.0861 | 18% |
| Barabara | Bilioni 777.2 | 12.8% |
| Afya | Bilioni 589.9 | 10% |
| Kilimo | Bilioni 379 | 6.2% |
| Maji | Bilioni 309.1 | 5.1% |

Tunasema Hongera Serikali kwa kazi nzuri. *(Makofi*)

(ii) Kwa Serikali kutoa kipaumbele namba moja kwa Sekta ya Elimu katika bajeti ya 2007/2008 katika kutoa ajira mpya kwa Sekta ya Elimu ambayo imetengewa nafasi 20,154 ambazo ni sawa na asilimia 49 ya ajira mpya Serikalini ambazo jumla yake ni 41,435. Tunasema vile vile Hongera kwa maamuzi haya.

Aidha, tunatoa Hongera kwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mb., kwa juhudi zake za ziada katika kusukuma ujenzi wa Shule za Sekondari Nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu bora kwa kiasi kikubwa inatokana na mafunzo ya Ualimu na hasa tukizingatia kuwa Walimu ni chimbuko la Uzalendo wa Kitaifa na

Utaifa. Walimu ni wazalishaji pekee wa nguvu kazi ya Taifa katika nyanja zote za kiuchumi na za kijamii, hivyo ili kuboresha taaluma ya Ualimu na kuweza kukabiliana na changamoto za kupata Walimu wenye sifa na taaluma nzuri tunaishauri Serikali kufanya yafuatayo:

(i) Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iandae mpango maalumu wa mafunzo kazini *(In-service Training) na Up-grading Courses* ya Walimu wa ngazi mbali mbali. Mfano: Walimu ngazi ya Daraja la IIIA, asilimia 25 hadi 30 wakipewa mafunzo ya Ualimu ngazi ya Diploma, Serikali itakuwa imetatua sehemu kubwa ya upungufu wa Walimu wenye sifa za kutosha kwenye ngazi ya Shule za Msingi na Sekondari ya kawaida (*O level).*

Vivyo hivyo ukitoa nafasi za kutosha kwa Walimu wenye Diploma kuchukua mafunzo ya Shahada kwenye Vyuo Vikuu utapata Walimu wa kutosha wa Sekondari ya kawaida na ya juu (*A-level*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kuwa lengo la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kudhamini Walimu 1500 kwenye Chuo Kikuu Huria cha Tanzania - *OUT* pamoja na wale wanaosomea Shahada za Ualimu kwenye Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki ni lengo zuri sana na tunashauri idadi hii iongezeke.

Hivyo Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwenye Kasma ya *Inservice Training/ Upgrading Courses* kwa ajili ya kupata Walimu wa kutosha wenye sifa. Pia Serikali iendelee kuimarisha Vyuo vya Walimu ili kuongeza idadi ya Walimu daraja IIIA ambao ni muhimu sana kwa ngazi za madarasa ya awali na Elimu ya Msingi.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itekeleze maombi ya muda mrefu ya kuwaondolea walimu urasimu na usumbufu mkubwa wa matatizo yanayotokana na mfumo wa ajira yao, kwa kuzingatia kuwa Walimu idadi yao ni karibu asilimia 50 ya watumishi wote wa Serikali. Kundi hili ni kubwa na hivyo linahitaji kuwa chini ya Idara au chombo kimoja cha ajira.

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika**,** motisha kwa ajira ya Ualimu na kufanya kazi ya Ualimu yenye ujira au mshahara mzuri na kutambua wale watakaofanya kazi katika mazingira magumu ndiyo njia muafaka ya kuifanya kazi ya Ualimu kuwa na mvuto kwa wale watakaopenda kusomea kazi ya Ualimu.

(iv) Mheshimiwa Naibu Spika, mrundikano wa madaraja ni kero na hivyo hatua za makusudi zichukuliwe kurekebisha hali hiyo.

(v) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke msukumo wa kipekee katika kujenga nyumba za Walimu mashuleni na hasa vijijni. Hiki nacho ni kivutio na motisha muhimu kwa Walimu, kwa sababu katika mazingira ya ukosefu wa vyumba vya madarasa, hatua zozote za kuwa na aina mbadala ya vyumba inaweza kufanywa kwa muda. Lakini

haiwezekani Mwalimu akaishi kwenye mazingira mengine yoyote zaidi ya kuwa na nyumba.

(vi) Mheshimiwa Naibu Spika**,** fedha zinazotengwa kwa ajili ya kuendesha shule kama vile '*Capitation grant'* zinatakiwa zifikishwe kwenye akaunti za Shule kwa wakati na kwa usahihi. Ni vema Serikali itimize ahadi yake ya kutoa Dola 10 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kwani kwa sasa zoezi hili linaziweka shule kwenye matatizo ya uendeshaji na hili linaweza kushusha ari ya Walimu na watoa huduma kwa ujumla, na hata kuathiri taaluma kutokana na ukosefu wa vifaa vya kufundishia.

(vii) Mheshimiwa Naibu Spika, malimbikizo ya madai ya Walimu yalipwe yote na mianya inayoruhusu hali hiyo iondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio ya kutekeleza MMEM kwa kujenga madarasa, kuandikisha wanafunzi wengi darasa la kwanza na kuwepo Kanuni na Waraka wa Elimu Na. 25 ya uandikishaji na mahudhurio shuleni ya lazima ya mwaka 2002 *(The Primary School Compulsory Enrollment and Attendance Rules)* kumekuwepo vitendo vya utoro wa wanafunzi katika Shule za Msingi kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na watoto kwenda kufanya biashara ndogondogo, kupata mimba na baadhi yao kuolewa au kuoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili limekuwa kubwa kiasi cha kumfanya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kufikia hatua ya kukemea tatizo la utoro shuleni. Aidha, Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya mwaka 2007/2008 ukurasa 32 ilionyesha wazi kwa takwimu kuwa tatizo hili limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka. Mfano, mwaka 2002 wanafunzi waliokatishwa masomo walikuwa 36,680 ikilinganishwa na wanafunzi 48,221 mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuchukua hatua madhubuti na kali dhidi ya wazazi, wananchi na wanafunzi wanaoendekeza tabia hii ambayo inazidisha ongezeko la wajinga katika jamii.

Ni muhimu Serikali ifahamu ni nani anazembea katika eneo hili wakati utawala wa Serikali unaanzia katika ngazi za msingi za Vitongoji na Mitaa. Aidha, tunashauri kuwa agenda ya utoro wa watoto shuleni, sasa iwe ya kudumu kwenye Kamati za Elimu za Halmashauri ambako taarifa ya kila shule inaweza kujadiliwa ili tatizo la utoro lipungue au liishe kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuwa na Mpango Mkakati utakaofanikisha wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari kusoma, kuelewa na kufaulu masomo ya lugha hasa Kiingereza na Kiswahili kwani lugha hufanikisha kuwepo na mawasiliano ya uhakika kati ya mwalimu na wanafunzi, na kwa kuwa masomo mengi katika Shule za Sekondari hufundishwa kwa lugha ya Kiingereza, wanafunzi wengi hushindwa kufaulu mitihani kwa sababu ya kutoelewa vema wanachofundishwa na namna ya kujieleza kwa yale wanayotahiniwa. Lugha ni ufunguo wa masomo mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Hisabati bado matokeo ya elimu ya Msingi na Sekondari yanaonyesha udhaifu katika kufaulu somo la Hisabati. Somo hili ni muhimu kwa sababu ndilo linalojenga msingi wa mwanafunzi kuwa na uwezo wa kufikiri, kurahisisha na hatimaye uwezo wa kumfanya awe na maarifa ya kukabiliana na maisha yake katika harakati za kupambana na umaskini na kupata maisha bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa matumizi ya fedha za utekelezaji wa mpango wa MMES zinazotolewa na Serikali Kuu yasimamiwe kwa karibu na Wakurugenzi wa Halmashauri na Bodi za Shule, Kamati za Elimu za Halmashauri husika na Wananchi wapewe taarifa ya miradi inayojengwa kupitia MMES. Ushauri huu unatokana na usimamizi mbaya wa matumizi ya fedha za MMES unaoshuhudiwa na Kamati inapotembelea Shule za Sekondari kwenye Mikoa na Wilaya mbali mbali.

Aidha, Waratibu wa Sekondari walioteuliwa hivi karibuni sasa washirikishwe kikamilifu. Tunashauri kuwa Waheshimiwa Wabunge wawe wakipewa taarifa ya kina kila wanapotembelea Shule za Sekondari kwenye majimbo yao, ili nao watekeleze wajibu wao wa kusimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kamati inashauri Serikali kwamba kwa kuwa kumekuwapo na mafanikio katika ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata zilizofunguliwa mwaka huu (2007); na kwa kuwa kiwango cha kufaulu katika Shule za Sekondari kimekuwa kinaongezeka kila mwaka, ni vema Serikali na jamii kwa ujumla ikaanza mikakati ya jinsi ya kuweka miundombinu ya kidato cha tano watakapomaliza kidato cha nne mwaka 2010, na watakaoingia Sekondari mwaka 2008 watakuwa wengi zaidi na hivyo baada ya mwaka 2010 ni lazima tuwe na Shule za kutosha za kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Taasisi ya Elimu ni chombo mahususi chenye wataalamu waliondaliwa kutafiti, kuandaa na kukuza mitaala ya Elimu kuanzia ngazi ya Shule za awali, Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu, kudhibiti ubora wa zana zinazotumika kuendeleza mitaala, kutunga na kuchapisha mihtasari, kuunda na kusambaza zana za kufundishia mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa kazi ya Taasisi hii ni ya kitaalamu inayohitaji maandalizi maalumu, hivyo ipewe uwezo ili iweze kuandaa mitaala kwa kuzingatia mahitaji na matazamio ya jamii na ulimwengu wa utandawazi. Aidha, Kamati inashauri kuwa kuwepo muda maalumu wa kufanya maandalizi ya mabadiliko ya mitaala ya elimu katika ngazi zote kwa kuzingatia maoni ya wadau na mahitaji ya Soko la ajira badala ya kufanya maamuzi yasiyofanyiwa utafiti wa kutosha.

Kwa mfano, kuanzishwa kwa somo la Stadi za Kazi katika Elimu ya Msingi miaka mitano iliyopita bila kuwa na maandalizi ya kukidhi kufundishwa kwa somo ambalo moduli za kufundisha somo hilo zimechelewa kusambazwa kwenye shule. Pia kufutwa kwa mikondo ya biashara na kilimo katika shule za Sekondari miaka michache iliyopita na mikondo hiyo kurejeshwa tena mwaka jana. Tujifunze kutokana na upungufu wa aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mitihani ni chombo nyeti na ni jicho la Taifa kinachoipatia nchi uhalali wa viwango vya elimu wanayopata watu wake. Kamati inaona kuwa Serikali haijatoa umuhimu unaostahili hasa katika kuboresha miundombinu na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa Serikali huchukulia Baraza la Mitihani kuwa sawa na Taasisi nyingine za kawaida na hivyo kutolipa uzito unaostahili hasa katika masuala ya bajeti na hivyo kuwa na upungufu mkubwa wa vitendea kazi na kuathiri ufanisi wa shughuli zake.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kamati inaelewa upungufu mkubwa katika Taasisi hii nyeti ni pamoja na kuchakaa na kupitwa na wakati kwa mfumo wake wa kompyuta aina ya *WANG Vs* 65 ulioanza kutumika mwaka 1983, umechakaa na programu zake kupitwa na wakati na umekuwa ukiharibika mara kwa mara na kusababisha msongamano wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Baraza lipewe fedha za kutosha kuboresha vitendea kazi vyake ikiwa ni pamoja na kuweka mfumo mpya wa kompyuta, kuboresha sehemu ya uchapaji wa Mitihani na Vyeti na kununua magari ya kusafirishia Mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kamati iliwahi kutembelea ujenzi wa Kituo cha kusahihisha mitihani Mbezi ambacho kipo katika hatua za mwisho za ujenzi. Pamoja ma mafanikio ya ujenzi wa kituo hicho, Baraza linadaiwa kiasi cha Shilingi bilioni 13.2. Makandarasi wamefikia hatua ya kutaka kulifikisha suala hili kwenye vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka wa fedha wa 2007/2008 Serikali imetenga kiasi cha Shs. 300,000,000/= kama sehemu ya kulipa deni hilo. Kamati inaona kuwa fedha hizo ni kidogo sana, sawa na asilimia 2.27 ukilinganisha na ukubwa wa deni zima la Makandarasi. Hivyo Kamati inashauri kuwa Serikali itafute fedha au njia nyingine za kulipa deni la Makandarasi hao kabla ya Baraza kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kamati inaipongeza Serikali kwa mpango wa kuendeleza Elimu ya Ufundi Stadi chini ya VETA nchini kote. Kamati inashauri Serikali kutoa maelezo ya maendeleo ya ujenzi wa Vyuo vya VETA na lini ujenzi utakamilika kwa Mikoa ya Pwani, Lindi na Manyara ambayo ndiyo Mikoa pekee isiyokuwa na Vyuo vya VETA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inashauri Serikali kuwa utaratibu wa kuwa na vyuo vya Ufundi kwa kila wilaya ukamilishwe kutokana na wingi wa vijana wanaomaliza elimu ya Msingi ambao hawapati nafasi ya Elimu ya Sekondari, na wale wanaomaliza Elimu ya Sekondari ambao hawapati nafasi ya kuendelea katika fani nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati inashauri kuwa ili kuleta maendeleo na mafanikio ya haraka katika kupanua Elimu ya Ufundi Stadi, Serikali ibakize asilimia 4

kwa VETA badala ya asilimia 2 ya kodi inayopata kutokana na kodi iitwayo 'VETA *Skills and Development Levy'*, ili zitumike kuendeleza na kuboresha vifaa vya kufundishia kuongeza idadi ya Vyuo hivyo, kujenga mazingira mazuri zaidi ya wahitimu wa Elimu ya Msingi na Sekondari kujifunza fani mbali mbali za kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuhamasisha wasichana kujiunga na Elimu ya Ufundi kwa kuweka mikakati zaidi ili kulinda mafanikio ya asilimia 48 ya Wasichana ambayo imefikiwa mwaka 2007. Hii ni hatua njema ya kupongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** naomba kuchukua fursa hii kukupongeza wewe kwa jinsi unavyoendesha Vikao vya Bunge kwa umahiri na busara kubwa. Aidha, nampongeza Naibu Spika na Wenyeviti wanaokusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Pia nawapongeza Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa jinsi tulivyoshirikiana katika kujadili na kwa ushauri mbali mbali wakati wa shughuli za Kamati yangu na Kamati nyingine. Hongereni sana Wenyeviti wa Kamati za Kudumu kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati nimamshukuru Mheshimiwa Margareth S.Sitta (Mb), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi akisaidiwa na Manaibu wake Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza (Mb) na Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila (Mb) pamoja na watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, Profesa Hamis Dihenga kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati kutoa majibu ya hoja za Wabunge kuhusu utekelezaji wa Wizara kwa mwaka 2006/2007, na Bajeti ya mwaka wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho namshukuru Katibu wa Bunge, Bwana Damian S.L. Foka na Ofisi yake kwa kutuhudumia vema kipindi chote Kamati ilipokuwa kazini. Nampongeza Katibu wa Kamati hii Ndugu Theonest K. Ruhilabake, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi Taarifa hii kutoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuwashukuru na kuwapa hongera kwa kazi nzuri Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kwa kuishauri Serikali kuboresha Sekta ya Elimu na kuipa kipaumbele namba moja, kwani kila mwaka Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa Sekta ya Elimu, kazi ambayo sasa Serikali imefanya. Hongera sana Serikali na tutaendelea kuishauri Serikali kuwa iendelee kuipa Sekta ya Elimu kipaumbele. Elimu ndiyo silaha kubwa katika kupambana na umaskini, ujinga na maradhi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** na sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 87(4) ya Kanuni za Bunge, na naomba niwatambue wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kama ifuatavyo: Mheshimiwa Omari S.Kwaangw', Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mheshimiwa Nuru A. Bafadhili, Mheshimiwa Prof. Feetham F. Banyikwa, Mheshimiwa Hasnain G. Dewji, Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Hemed M. Hemed, Mhe.shimiwa Phares K. Kabuye, Mheshimiwa Janeth B. Kahama, Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mheshimiwa Sameer I. Lotto, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Margreth A. Mkanga, Mheshimiwa Martha M.

Mlata, Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Omari A. Mzee, Mheshimiwa Khadija S. Ngozi, Mheshimiwa Sijapata F. Nkayamba, Mheshimiwa Usi Amme Pandu, Mheshimiwa Faustine K. Rwilomba, Mheshimiwa Mwanakhamisi K. Said, na Mheshimiwa Fatma Abdulla Tamim.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ili Serikali itekeleze yale yaliyopangwa kwa mwaka 2007/2008 na kuufanyia kazi ushauri wa Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Said Amour Arfi.

Mheshimiwa Arfi kabla hujasoma hotuba yako ili kufanya usirudie ama tusikukatishe fungua ukurasa wa 4 wa hotuba yako, ubora wa elimu msitari wa 3 mkono wako wa kulia inasomeka "Kambi ya Vyama vya Ushindani". Mmeona maneno hayo! Yaondoe hayo yape jina lake vizuri.

Namshahihisha Mheshimiwa Arfi kwa mujibu wa kanuni zetu. Kanuni zetu hazitambui Kambi ya Ushindani zinatambua Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa Kanuni ya 11. Kanuni ya 12(1) inatambua kuwepo kwako Mheshimiwa Arfi kama umeteuliwa na Kiongozi wa Upinzani. Kwa hiyo, yafute maneno hayo, utakaposoma usome inavyostahili. Kwa hiyo, hotuba yako itakubalika. (*Makofi)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika.

**MHE. SAID AMOUR ARFI – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa Bungeni tukiwa hai na wazima. Pili,naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuchangia kwa mujibu wa kanuni za Bunge, Kanuni za 43(5)(c) na 81(1) kwa kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi nichukue nafasi hii kutoa shukrani na pongezi za kipekee kwa viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wao imara na madhubuti wenye kuiwezesha Kambi ifanye kazi zake kulingana na Kanuni zetu za Bunge.

Bila kusahau, nitoe pia pongezi kwa Wabunge wote wa Upinzani kwa umoja walionao, wakishirikiana na wale wote wawekao mbele maslahi ya nchi hii, kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kwa maslahi ya Taifa na Watanzani wote. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani pamoja na Naibu wake kwa kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Napenda kuahidi kuwa nitajitahidi kwa hali na mali na kuonyesha kuwa hawakukosea katika uteuzi huu. Vilevile nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Mpanda Kati kwa ushirikiano wanaonipatia katika kufanya kazi yangu vizuri, nawaahidi kuwa nitakuwa nao na sitapoteza imani yao kwangu, Mungu aendelee kutupa uzima wote. Amin!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuwapa pole wale wote waliopatwa na maafa na majanga mbali mbali ambayo yote ni miongoni mwa mitihani yake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tuwaombee wenzetu wote waliokwishatangulia kwenye makazi mema peponi, na wale waliopatwa na maumivu waweze kupona haraka. *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** aidha, nichukue nafasi hii kutoa pole kwa familia ya hayati Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, aliyetutoka hivi karibuni. Marehemu alikuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya vijana wa Kitanzania. Mwenyezi Mungu ampe makazi mema. *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kabla sijaanza kutoa Maoni ya Kambi ya Upinzani, naomba niweke kitu kimoja bayana. Hapo zamani Elimu ilikuwa ni huduma lakini kwa sasa kulingana na matakwa ya viongozi wetu elimu imekuwa ni bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema haya kwa kuwa wakati ilipokuwa huduma "UBORA" kwa shule zote Tanzania ulikuwa katika kiwango kimoja kuanzia kwa walimu hadi mgawanyo wa vifaa vya kufundishia katika shule zote.

Kwa sasa imekuwa bidhaa kwa maana kuwa kila mtu ana hiari ya kununua bidhaa kulingana na ubora anaouhitaji yeye na ubora huo ndio utakaotoa bei ya kununulia, na hili limepelekea kuwa na shule za madaraja kulingana na ubora wa bidhaa hizo. Na hii ni hatari sana kwetu. Wazazi wasiokuwa na fedha hawawezi tena kuwanunulia watoto wao elimu bora, maana yake ni kuwa watoto wao wasipate nafasi za uongozi katika nchi hii.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi ya Kenya imejitahidi sana kuendelea kuifanya elimu kuwa ni huduma, yaani viwango vya elimu kwa shule zote za Serikali ni sawa, shule ziwe mjini ama vijijini. Jambo hili ni la kuwapongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuongelea machache ambayo Kambi ya Upinzani inaona kuwa yatafaa katika kurekebisha na kuiwezesha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iweze kutoa elimu iliyo bora kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiweka mkazo katika kuangalia uwingi wa wanaokwenda shule za msingi na sekondari bila kuzingatia kikamilifu ubora. Msimamo wa Serikali wakati wote umekuwa kwamba cha muhimu ni kujenga kwanza madarasa, suala la ubora litafuata. Hata Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete amerudia tena msimamo huu alipokuwa akijibu maswali ya waandishi wa habari baada ya hotuba yake ya mwisho wa mwezi uliopita. Kambi ya Upinzani inadhani suala la ubora na uwingi ni lazima viende sambamba bila kutenganishwa. Tukitaka na tukiwa na dhamira inawezekana.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya upinzani haikubaliani kabisa na msimamo huu wa Serikali. Ni vyema Serikali ikakumbuka uzoefu katika Mpango wa Elimu kwa Wote (*UPE*) ambapo yapo maeneo ambayo Taifa lilipata madhara kwa kuangalia zaidi uwingi na kusahau ubora. Maisha bora kwa kila mtanzania hayawezi kutokea kama wanafunzi watapata ‘Bora Elimu’ badala ya ‘Elimu Bora’. Sasa Serikali imeanza kupeleka nguvu zaidi katika elimu ya Sekondari kupitia MMES wakati huo huo bado suala la ubora wa elimu halijashughulikiwa katika elimu ya msingi kupitia MMEM.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni ishara baada ya muda tutahama tena MMES bila kushughulikia suala la ubora. Ubora utaendelea kuachwa nyuma huku suala la uwingi likiendelea kukimbizwa mstari wa mbele. Kambi ya upinzani inaitaka Serikali kueleza wazi kiwango cha ubora wa elimu ambacho kila mwanafunzi anapaswa kupata *(minimum standard package)* ili kila shule iweze kuzingatia. Suala hili limetolewa maelekezo pia na Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Elimu (*UNESCO*).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwahakikishia Watanzania kuwa kambi ya upinzani kwa ushirikiano na Serikali kupitia Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kuunga mkono jitihada zote zenye lengo la kuwapatia Watanzania wote Elimu Bora itakayo wawezesha kupambana na adui mkubwa ujinga na umasikini na hasa katika dunia hii ambayo bila Elimu bora Serikali itaendelea kubeba mzigo mkubwa ambao kadiri elimu bora itakavyokuwa inatolewa utapungua sana kwa vile wananchi wenye elimu watakuwa wakijihudumia kwa mambo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya elimu ni mojawapo ya sekta muhimu sana ambayo imekuwa ikipewa kipaumbele kwa maendeleo ya jamii yoyote na historia inaonyesha kuwa hakuna nchi duniani iliyoendelea bila kutoa kipaumbele kwenye Elimu na; au kuwekeza vya kutosha kabisa kwenye Elimu, ngazi zote toka awali hadi elimu ya juu.Tanzania kama nchi inayoendelea inahitaji kuwa makini na vipaumbele inavyotoa. Kwa kiwango fulani bajeti ya mwaka huu, iwapo fedha hizi zitatolewa zote na kusimamiwa vizuri, inayoashiria mwanzo wa msingi mzuri.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Elimu ya Msingi Kwa Waliokosa (MEMKWA), ili kukabiliana na wimbi la kuondoa ujinga miongoni mwa watanzania, Wizara ya Elimu iliamua kuanzisha mpango maalumu ili kuwawezesha wale wote walioikosa Elimu ya msingi kwa wakati waweze kuipata kwa kupitia mpango huu. Huu ni uamuzi wa Jumuia ya Kimataifa uliopitishwa *Jomtien Thailand,* mwaka 1990 maarufu

kama “*EFA*”, japo neno hili halijatumika sana Tanzania. Mpango huu ulikuwa ukamilike mwaka 2000, lakini kwa kuwa nchi nyingi hazikufikia malengo umepangwa sasa ukamilike mwaka 2015. Toka kuanzishwa kwa mpango huu nchini kwetu umeonesha kiwango fulani cha mafanikio kwa Watanzania, pamoja na kuwa pia umekumbwa na matatizo mengi. Mpango huu ulikuwa umelenga vijana wa kike na kiume kuanzia rika lengwa kuanzia miaka 13 na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tafiti mbali mbali zilizofanywa na vyombo vya habari imebainika kuwa pamoja na matatizo mengi yaliyoukumba mpango huu, baadhi ya wanafunzi wa kike walioko kwenye MEMKWA ni wafanyakazi wa kazi za nyumbani, pia imebainika kuwa wanafunzi hao hupewa kazi nyingi ambazo huwafanya kukosa muda wa kujisomea. Kutokana na hali hiyo wanafunzi hao hulazimika kucheza katika maeneo yaliyo karibu na shule ili kupoteza muda wa kurudi nyumbani na hivyo kuepuka kufanyishwa kazi nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kuleta taarifa hii katika Bunge lako Tukufu ili Wizara iweze kuandaa utaratibu ambao utaweza kuwasaidia wanafunzi hao na waweze kupata Elimu bora, kwa manufaa yao na Taifa kwa ujumla. Pia Serikali kwa ujumla wake isimamie vizuri zaidi sheria inayokataza watoto wadogo kufanyishwa kazi. Kupitia mpango huu pia imebainika kuwa mpaka sasa kuna baadhi ya shule za msingi zenye madarasa ya MEMKWA, kuna wanafunzi walioolewa na kuachika, na wengine wamekwishazaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swala hili sio baya, kwani na wao ni Watanzania na wana haki ya kupata Elimu chini ya mpango huu. Hivyo basi, ingekuwa vizuri utaratibu bora zaidi ungeandaliwa ikiwa ni pamoja na kuwa na madarasa tofauti na wanafunzi wenye umri mdogo ambao kimsingi wanatofautiana sana kwa uelewa, mitazamo na mahitaji. Tunachotafuta ni utoaji wa Elimu wenye Tija, badala ya kuwalundika pamoja, na hivyo kutokugusa mahitaji maalumu kwa kadiri ya uwezo na vipawa vya kila mmoja wa watoto hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matatizo ya lengo la kila aliyefaulu Kujiunga na Shule, Serikali imehamasisha wananchi kujenga shule katika kila Kata ili watoto wote waliofaulu wasome. Tatizo ni kuwa shule hizo zina michango mingi nje ya ile inayojulikana rasmi kiasi cha kufanya baadhi ya watoto ambao wazazi wao wana hali duni kuacha kujiunga na masomo kwa ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoto huwa wanachangishwa madawati, kuendeleza ujenzi wa madarasa na kadhalika, gharama ambazo inabidi mzazi alipie takriban shilingi 150,000/- wakati uwezo huo haupo. Je, Serikali haioni hii inachangia kuwakosesha walalahoi masomo? Ni vema Serikali ikatoa mwongozo unaojulikana na ulio wazi kwa nchi nzima ili wazazi wajue kabisa wanatakiwa kuchangia nini hasa kwa elimu ya watoto wao na hivyo wapate nafasi pia ya kujiandaa kikamilifu. Sasa hivi Serikali inazungumzia ada ya shilingi 20,000 kwa Shule ya kutwa, lakini hali halisi ni tofauti kabisa na maelekezo hayo ya Serikali. Kambi ya Upinzania inaitaka Serikali itoe Tamko rasmi na

mwongozo uliowazi kuhusu jambo hili ili watekelezaji waweze kufahamu nini hasa kinaruhusiwa na nini hakiruhusiwi katika kuchangisha wazazi.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wanaodaiwa ada hurudishwa nyumbani japokuwa kosa sio la watoto. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa badala ya kuwarudisha watoto na kuwanyima nafasi ya kusoma, Wazazi waitwe mashuleni na kuwekeana Mikataba ya ulipaji ada badala ya kuwarudisha wanafunzi nyumbani. Hali hii ni hatari zaidi kwa wasichana kwani ndio chanzo cha kufanya maasi badala ya kurudi nyumbani. Anaelekea sehemu zisizostahili na watu wasio na nia njema hutumia nafasi hiyo kuwatia kwenye vishawishi watoto hao. Utaratibu huu si salama kabisa kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa sana kwa Wanafunzi ambao wanaishi umbali mrefu sana kutoka shule zinapojengwa kwa kutilia maanani jiografia ya kata zetu. Hivyo basi litakuwa jambo la busara kama kila shule ya Kata ingelikuwa pia na Hosteli angalau kwa wanafunzi wa kike ili kuepuka kukaa nyumba za kupanga, maarufu kama '*gheto'* ambazo nazo ni chanzo kikubwa kwa watoto wetu kupata mimba wakiwa shuleni.
Hosteli hizo pia zitapunguza adha ya usafiri kwenda na kurudi kutoka sehemu wanazoishi ambapo kwa wengine ni zaidi ya kilomita 5 njia moja. Hali hii humpunguzia mwanafunzi tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, shule nyingi za sekondari zilizojengwa kila Kata zinafikia tu kidato cha nne. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa sambaba na shule hizo kuwe na mkakati kabambe wa kujenga pia Kidato cha Tano, kwani kulingana na wingi wa shule zinazoishia kidato cha nne shule za vidato vya 5 na 6 hazitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi wote watakaofaulu. Tusije tukashtukizwa tena wakati hatujajiaandaa kwa ujenzi wa vidato vya 5 na 6. Kambi ya Upinzani inataka kujua, Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na changamoto hilo, na mkakati gani hasa umeandaliwa kwa ujenzi huo wa Vidato vya Tano na Sita.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tunadhani Serikali itakubali ushauri uliotolewa na Kambi ya Upinzani kuhusu jinsi ya kuwa na walimu wa kutosha na wenye sifa sahihi watakaoweza kukabiliana na ongezeko hilo la wanafunzi katika ngazi zote za elimu ya Sekondari hapa nchini. Tunaamini kabisa kwa kufuata ushauri huo wa kukodisha kwa mkataba wa muda maalumu walimu toka nchi jirani katika ngazi mbali mbali kutatoa mwanya kwa Serikali kufundisha walimu wake kwa utaratibu uliokuwa ukitumika hapo zamani. Kuna tatizo gani kuwa na utaratibu wa waalimu toka nchi jirani, mbona Majaji tuliwachukua kutoka Nigeria kwa mkataba maalumu?(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa imani yetu, kiini cha elimu bora sio darasa jipya, bali ni mwalimu aliyeelimishwa kikamilifu, mwenye nyenzo zote za kufundishia, na mwenye mazingira safi, salama na ya kumwezesha kufanyia kazi yake. Darasa jipya peke yake haliwezi kufanya elimu yetu kuwa bora.

Mwalimu aliyekamilika anaweza. Hivyo Kambi ya vyama vya Ushindani inadhani Walimu wanapaswa kupewa kipaumbele kwa kila hali ili kuboresha elimu.

Utaratibu wa *Crash programme*, uwe utaratibu wa mpito tu na kuwe na mkakati wa muda mrefu wa kuwaanda Waalimu na kuwaandalia waalimu mazingira mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msingi ni kuwa bila ya walimu kupewa kipaumbele na kuwa na walimu makini wanaongalia vyema mazingira ya ufundishaji kwa wanafunzi, mabadiliko yote katika sekta ya elimu ni kazi bure. Tunaamini kuwa walimu ndio roho ya elimu, hivyo basi ni lazima walimu wawe ndio roho katika sera yetu ya elimu na utekelezaji wake. Hii itaondoa na kumaliza mtindo wa zima moto katika uandaaji walimu katika ngazi mbali mbali elimu ya Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ruzuku kwa Ajili ya Elimu *(Capitation Grant),* kwa mujibu wa MMEM kiwango ambacho kinatakiwa kutumika kwa kila mwanafunzi ni dola 10 ambazo ni sawa na takriban shilingi 12,500 kwa mwanafunzi. Kwa mujibu wa MMES kiwango ambacho kinatakiwa kutumika kwa kila mwanafunzi ni kati ya shilingi elfu 20 mpaka 30 kwa mwanafunzi.

Tatizo la Msingi lililopo hapa ni fedha kutotumwa kamili na kutotumwa kwa wakati. Taarifa na tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa kiwango hicho hakijawahi kutumwa kikamilifu tangu uamuzi huo ufanyike. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe kauli juu ya usahihi wa Taarifa hizi, na kama kweli fedha hizi zinafika na kutumika inavyotakiwa kwenye Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iweke utaratibu wa wazi wa kila mdau wakiwemo wanafunzi na walimu wa kueleza Serikali itatoa shilingi ngapi na fedha hizo zinatolewa lini. Kwa uzoefu wa nchi mbalimbali ni vyema serikali ikaweka utaratibu wa kutoa fedha katika tarehe zinazojulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo sasa, pamoja na ruzuku kwa kila mwanafunzi kujulikana wazi, viwango vinavyomfikia mwanafunzi vinatofautiana katika Wilaya mbalimbali. Mathalani zipo Wilaya ambazo wanafunzi wanapata shilingi elfu mbili mia tano, zingine shilingi elfu tano na kadhalika.

Kwa utaratibu huu viwango vya elimu vitatofautiana pia wilaya hadi wilaya. Serikali itoe ufafanuzi ni kwa nini viwango vya fedha vinavyomfikia mwanafunzi moja kwa moja vinakuwa vikitofautiana na pia ieleze ni hatua zipi zitachuliwa kuzuia hali hii isiendelee kujitokeza.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti za Ukaguzi wa Mahesabu ya MMEM, tangu mwaka 2002 mahesabu ya matumizi ya fedha za MMEM yamekuwa yakikaguliwa kwa utaratibu tofauti na mahesabu ya kawaida ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Ripoti za fedha za MMEM zimekuwa zikikaguliwa na makampuni binafsi hususan kwa baraka za Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa ripoti za Ukaguzi *(audited reports)* za matumizi mengine ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI zimekuwa zikiwekwa wazi; ripoti za ukaguzi wa mahesabu ya MMEM zimekuwa hazitolewi kwa umma. Hata katika tovuti za Wizara ya Elimu na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*CAG*) ambapo ripoti zingine zinapatikana, ripoti za ukaguzi wa matumizi ya fedha za MMEM hazipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kinyume kabisa na dhana ya uwazi, uwajibikaji na utawala bora! Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuweka wazi ripoti hizi kwa umma kama ambavyo *CAG* anavyofanya kwa ripoti za matumizi mengine ya kasma za serikali.

(ii) Tujibiwe katika kikao hiki, nini masuala ya msingi yaliyojitokeza katika ripoti hizo na mapendekezo yaliyotolewa;

(iii) Toka ripoti hizo zianze kutolewa ni hatua gani zimechukuliwa kutokana na mapendekezo yaliyomo kwenye ripoti hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni muhimu sana kwa sababu MMEM ni mpango wa mageuzi makubwa katika elimu. Ni mpango wenye kutumia fedha nyingi, takriban shilingi bilioni 300 kwa mwaka ambazo ni wastani wa shilingi milioni elfu moja kwa siku.

Hizi ni fedha nyingi za umma na umma wa watanzania unapaswa kuelezwa ukaguzi wa matumizi yake kwa uwazi. Tunalisema hili kwa vile karibu kila mahali kuna malalamiko kuhusu matumizi mabaya ya fedha za MMEM katika ngazi za shule na kamati za shule, lakini hakuna utaratibu ulio wazi wa kupata taarifa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, japo utaratibu ni kuwa Kamati za Shule zinapaswa kutoa taarifa mara kwa mara kwa Serikali za Vijiji na hatimaye Mkutano Mkuu wa Kijiji, lakini utaratibu huu hautumiki karibu sehemu zote. Ni vema Serikali ikatolea Kauli jambo hili kabla mambo hayajaharibika, hasa tukizingatia Mkataba uliowekwa saini kati ya *IDA* na Serikali yetu kuhusu utaratibu wa kutunza fedha na wa Utoaji Taarifa wa fedha za MMEM.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia inaitaka Serikali kuweka wazi matumizi ya MMEM na hata MMES katika hatua zote zinazofuata kama ilivyo kwa matumizi mengine ya Serikali ili upungufu ambao umejitokeza usijirudie tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari, Kambi ya Upinzani imebaini tofauti baina ya maelezo yaliyomo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) na maelekezo ya utekelezaji yanayotolewa na serikali. Mathalani, Waziri Mkuu ametoa maelezo ya ujenzi wa sekondari moja kwa kila kata wakati MMEM inatoa maelezo tofauti. Serikali ni vyema ikatoa ufafanuzi: Mosi; je, tofauti hii iko kwa kiasi gani, kwa nini na athari zake ni nini? Pili; je, mpango wa sasa wa sekondari kata unazingatia masuala kadhaa yaliyotolewa maelezo katika MMEM

mathalani ukubwa wa kata, idadi ya watu na tofati za hatua ambazo maeneo mbalimbali yamefikia katika ujenzi wa sekondari?

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Wizara kwa Ujumla, Wizara ya Elimu ya Mafunzo na Ufundi katika kila mwaka wa Bajeti, imekuwa ikitegemea fungu kubwa la pesa kutoka nje. Kwa mfano, Matumizi ya Kawaida ya Wizara 2006/2007, fedha zilizoidhinishwa ni shilingi 133,964,077,900. Fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo zilikuwa sh.105,686,632,100. Katika matumizi ya Wizara 2007/2008, fedha zinazoombwa kwa matumizi ya kawaida ni shilingi 155,447,119,000. Matumizi ya miradi ya maendeleo ni shilingi 110, 232,746,700 kati ya hizo shilingi 95,856,764,700, ni fedha za utegemezi kutoka kwa wahisani mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika,tunaipongeza Serikali kwa kuweka mkazo katika kupanua elimu ikiwemo elimu ya msingi na sekondari. Na hapa Kambi ya Upinzani inapenda kusisitiza kwamba sisi Kambi ya Upinzani hatupingi elimu kuwa kipaumbele muhimu kama baadhi ya watu wanavyotaka kupotosha. Ndio maana wakati bajeti ya nchi iliyopitishwa Serikali imetenga asilimia 17.8 kwa ajili ya elimu. Kambi ya Upinzani mapendekezo yake ni kutenga asilimia 20 ya bajeti kwa ajili ya elimu na kuonyesha mahali ambapo fedha hizi zingelipatikana. Kinyume cha mawazo hayo, Kambi ya Upinzani inadhani bado kabisa Elimu haijapewa kipaumbele kinachostahili kama inavyoonyeshwa na mapendekezo yetu ya asilimia ambayo tungeliwekeza kwenye Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hiyo, imekuwa desturi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuwa na utegemezi kutoka nje ili iweze kuendesha shughuli zake. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali katika jambo zito kama la elimu, katika mipango ijayo ipunguze kwa kiwango kikubwa utegemezi huu ili kuwe na uhakika kabisa wa kutekeleza malengo yaliyopangwa. Serikali inafahamu kabisa majengo yaliyobaki magofu, baada ya kuwahamasisha wananchi wajenge maboma ya shule hadi lenta na fedha za wafadhili zingelimalizia. Maboma hayo yako hadi leo. Jambo hili siyo tu la hatari bali pia linawakatisha tamaa wananchi waliohamasika.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vyanzo vingine vingi vimekuwa vikichangia fedha katika sekta hii ya elimu, na fedha hizo hazionekani katika bajeti kuu ya wizara. Hii yote ni kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwa mfano,*Tanzania Social Action Fund* (*TASAF*), *PMO-RALG* ,*MoF*, *DONOR/NGO PROJECTS* na taasisi nyingine lakini cha ajabu ni kwamba fedha hizo zimekuwa hazionyeshwi kwenye Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, au bila kuonyesha fedha hizo zimefanya kazi zipi au kuelekezwa kwenye miradi ipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla fedha zinazochangiwa kwenye sekta ya elimu kutoka katika vyanzo vyote ni nyingi kiasi kwamba watendaji wanashindwa kuelewa ni nini kinatakiwa kufanyika. Japokuwa fedha zinazowekwa ni nyingi lakini lengo lake halionekani kwa jamii, kwani walengwa na matokeo yake ndio tunavyoona, ubora wa elimu unazidi kwenda chini.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Utaratibu wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, umekuwa ukipitia njia za aina mbili. Kwanza, Wizara imekuwa ikitumia njia ya *bottom-up planning*, ambapo muundo wa uandaaji wa Makadirio ya matumizi unaanzia katika ngazi ya vijiji na kuwa '*approved'* katika ngazi ya wilaya. Hii ni hatua nzuri na ya kupongezwa kwa sababu inawashirikisha wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia ya pili ni ile ya '*top-down planning'* (yaani mipango inaanzia juu), ambapo muundo wa Makadirio ya Matumizi unaanzia katika ngazi ya Serikali Kuu na kuandaliwa na Wizara ya Fedha na kuwa '*approved'* na Bunge. Hivyo basi ukiangalia kwa undani hizi njia mbili hazikufungamanishwa (*connected)* kwani njia ya pili inaonekana kuwa na nguvu zaidi kuliko ya kwanza ambayo matumzi yanapangwa kutoka ngazi ya kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kutumika sana kwa njia hii ya *top-down planning,* Wilaya pamoja na vijiji vimekuwa vikipata fedha na vitendea kazi kwa ajili ya maendeleo katika sekta ya Elimu kwa masharti na maelekezo ya jinsi ya kutumia fedha na vifaa hivyo. Wilaya pamoja na vijiji wamekuwa wakipangiwa ni kiasi gani cha fedha kitumike kwenye kununua madawati, kiasi gani kitumike kununulia *science kit* na vingine vingi kwa maendeleo ya Elimu hapo kijijini kwao tofauti kabisa na vipaumbele vilivyowekwa katika ngazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo inaonesha dhahiri kuwa ngazi za vijiji na wilaya zimenyimwa madaraka ama uwezo wa kukaa chini na kupanga mambo ambayo wao wanaona yanafaa na yatafaa katika kuendeleza sekta ya Elimu kwa manufaa ya wanakijiji na taifa kwa ujmla. Isitoshe mipango waliyopanga wakati Hazina na Bunge wanapoamua ukomo *(ceilings)* hupanga bila kuzingatia *ceilings* zilipendekezwa kutoka chini na hivyo kufanya utaratibu wetu wa Bajeti kuwa a*rbitrary* yaani usiozingatia vipaumbele vya walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango mingi inayokuwa ikipangwa na ngazi za vijiji inakuwa haitekelezwi. Utaratibu huu huziweka Halmashauri za Wilaya katika hali ngumu, kwani wakati fedha zinapelekwa huwa hazina uwiano na mipango ya awali hivyo huwajibika kupanga upya matumizi ya fedha hizo bila utaratibu maalumu. Hatua hii ndiyo inaingiza ubadhirifu mkubwa kwani kamati mbali mbali husika huwa hazihusishwi. Hii ni hali ya hatari sana. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kurekebisha hali hii kwa kutafuta uwiano unaofaa wa mipango na hasa kuhusisha ngazi za chini katika uwekaji wa *ceiling* ili bajeti na mipango yao iweze kutekelezeka kama walivyopanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanzishwa kwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), uwiano kati ya mwalimu na mwanafunzi umekuwa ukiongezeka na kupungua kwa kiasi kidogo kwa miaka tofauti sasa. Kwa mfano, kuanzia mwaka 2001 uwiano wa mwalimu na wanafunzi ulikuwa kama ifuatavyo:2001(1:46), 2002(1:53), 2003(1:57), 2004(1:59), 2005(1:56) na 2006(1:52).

Bado uwiano huu hautoshi na bado ni vigumu kwa mwalimu kufanya *consultation* na mwanafunzi mmoja mmoja na kuweza kugundua matatizo yao na kuweza kuwasaidia. Hivyo basi kuna umuhimu wa kufanywa jitihada za kuongeza walimu walio na ujuzi hasa kule vijijini, na hatimae kufikisha uwiano wa mwalimu mmoja na wanafunzi 40 (1:40),kwa kila darasa kama ilivyo katika viwango vya kimataifa. Kama tukifanikiwa kufikia uwiano huu nina hakika kwamba hii itaweka wepesi kwa mwalimu na kumrahisishia ufundishaji, pia uwiano huu una uwezo mkubwa sana wa kuondoa msongamano wa wanafunzi katika madarasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa fedha imekuwa ni tatizo kubwa linaloikibili Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, na hii limekuwa kikwazo kikubwa katika kutekeleza malengo mbalimbali ya programu za (MMEM na MMES) ,kwa mfano, ujenzi wa vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na maabara na hivyo kuathiri utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya upinzani inapenda kujua kama tulivyoonyesha hapo mwanzo kuwa kuna fungu kubwa la utegemezi kutoka kwa wahisani mbali mbali,na mashirika mengi yamekuwa yakichangia fedha kwa ajili ya maendeleo ya Elimu; je, fedha hizo hazitoshi kumalizia miradi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Shule zenye Mazingira yanayomjali Mtoto *(child friendly school project*), Wizara kwa kushirikiana na *UNICEF* imeendesha mradi wa uhamasishaji jamii juu ya shule inayo mjali mtoto. Mradi huu unatarajiwa kumalizika mwaka 2009, na kwa kupitia mradi huu ni jumla ya shule 622 katika wilaya sita nazo ni Kisarawe, Masasi, Songea, Musoma, Ngara na Makete. Kambi ya Upinzani inapenda kujua mambo matatu muhimu, katika mradi huu. (i) Ni mafanikio gani yamepatikana mpaka sasa tangu mradi huu uanzishwe hasa katika wilaya hizo? (ii) Ni vigezo vipi vinatumika kuichagua wilaya kuanzishiwa au kupelekewa mradi huo? (iii) Kama mradi una mafanikio katika kutengeneza mazingira yanayomjali mtoto, ni hatua zipi Wizara inachukua ili kuhakikisha kuwa mradi huu unazifikia wilaya zingine zote kabla ya mradi kwisha ili manufaa ya mradi yaweze kupatikana kwa nchi nzima?

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo ya stashahada ya kawaida ya Elimu ya watu wazima na kutoa stashahada ya juu. Taasisi hii pia ina lengo la kutoa mafunzo ya kuendeleza wafanyakazi wa taasisi katika mafunzo ya shahada ya udaktari wa falsafa, shahada ya uzamili, Elimu ya sekondari, na mafunzo ya muda mfupi.

Taasisi hii imekuwa ikijitahidi kwa hali na mali ili kufikia malengo yake kama ilivyojipangia. Hata hivyo, Taasisi hii imekuwa ikikabiliwa na matatizo mbalimbali ambayo yamekuwa yakipelekea athari nyingi na kusababisha kutokutekelezwa kwa malengo iliyojipangia, kama:-

(i) Taasisi imekuwa ikiingia gharama kubwa za kukodi majengo mfano, kukodi vyumba vya madarasa ya kufundishia masomo ya ana kwa ana. Na hii ni kutokana na

upungufu wa majengo ya ofisi na madarasa katika vituo vya kuendeshea shughuli za TEWW.

(ii) TEWW imeshindwa kutekeleza majukumu yake kama ilivyo kwenye mpango wa utekelezaji kutokana na kutokupatiwa fedha za kutosha.

(iii) Pia TEWW imeshindwa kufuatilia na kusimamia utekelezaji katika vituo vya TEWW mikoani kutokana na ukosefu wa fedha. Hata hivyo, Taasisi hi imekuwa ikijitahidi kwa hali na mali ili kukabiliana na matatizo hayo, kama kutoa mafunzo kwa wafanyakazi ili kuongeza maarifa na ujuzi kwa lengo la kuongeza tija. Na vilevile Taasisi imekuwa ikiandika michanganuo mbalimbali ya kuombea fedha kutoka kwa wabia mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni nafasi muhimu na ya pekee kwa Serikali kuona kwamba taasisi hii ina juhudi zake binafsi ili iweze kufikia malengo iliyojipangia, hivyo basi Serikali haina budi kuchukua hatua mbalimbali ambazo zitaisaidia taasisi kukabiliana na matatizo hayo na hatimae kufanikiwa kufikia malengo iliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili watoto wa kitanzania waweze kupata Elimu iliyo bora kwa manufaa yao ni lazima na mazingira ya upatikanaji wa Elimu hiyo yawe bora. Moja ya mazingira hayo ni maktaba zenye vitabu vya kiada vya kutosha ambapo mwanafunzi anaweza kujijengea desturi ya kujisomea kwa muda wake wa ziada.

Ujenzi na ukarabati wa maktaba ni mojawapo ya miongoni mwa miradi ya Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi kwa miaka miwili sasa. Mpaka sasa Wizara haijatoa ripoti yake au kuonesha ni maktaba ngapi zimekwishajengwa au kukarabatiwa, au zimefikia kiwango gani, na ni mikoa mingapi mpaka sasa mradi huu umeanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu dunia nzima wanakubaliana kuwa mwanafunzi anaelewa vizuri pale anapotumia lugha anayoifahamu. Kwa njia hii ni ukweli kuwa elimu tunayoitoa hapa kwetu inashindwa kukubaliana na ukweli wa tafiti zilizofanywa na wataalamu mbalimbali duniani kuhusiana na mchango wa lugha katika uelewa wa wanafunzi. Aidha, kujifunza masomo kwa kutumia lugha wanayoielewa hakumwondolei mwanafunzi uwezo wa kujifunza lugha nyingine ya kigeni kama kingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa mapendekezo yafuatayo ambayo kwa kiasi kikubwa yatasaidia katika kuendeleza na kuimarisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, na hivyo kumwezesha mwanafunzi wa kitanzania aweze kupata Elimu lliyo bora, kwa manufaa yake na taifa kwa ujumla. Katika utengenezaji wa Bajeti, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa njia bora ya kuweza kutumika ni ile ya *bottom-up planning*, kwani njia hii itatoa fursa kwa wanainchi kujadili na kupanga bajeti kulingana na mahitaji yao katika Elimu. Kambi ya Upinzani inaamini kwa asilimia mia kuwa wananchi ndio hasa wanayoyajua matatizo na mahitaji yao kielimu. Hivyo basi wapewe uhuru huo na yale yatakayopangwa yafanyiwe kazi. Wizara

ishughulike na utoaji wa mipango na mwelekeo wa jumla, kulinda Sera na ubora wa elimu (*quality*).

Kuwepo na uwazi katika ngazi zote kuanzia ngazi ya kijiji, ngazi ya wilaya na hata mashuleni juu ya utendaji kazi wao na matumizi ya fedha pamoja na vifaa vilivyotolewa na serikali na hata wabia mbalimbali. Kuanzishwe kwa mbinu shirikishi kwa kila Halmashauri ambapo wananchi wataweza kushirikishwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali. Kwa mfano, katika mradi wa ujenzi wa nyumba za walimu tuna uhakika iwapo wananchi watashirikishwa katika zoezi hili jambo hili litafanikiwa kwa kiasi kikubwa na kuokoa fedha kwa kazi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru tena. Aidha, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa hotuba yako. Sasa tunao wachangiaji na tunaanza na wale ambao hawajapata nafasi ya kuchangia katika Wizara zilizotangulia.

Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Rosemary Kirigini na Mheshimiwa Magreth Mkanga nadhani kwa asubuhi hii watakuwa wanatosha. Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kwa kuwa mtu wa kwanza kuchangia katika siku ya leo. Naomba pia niipongeze Simba kwa ushindi wao wa jana.(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nimekuona umekuwa Simba.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu, ni kweli mimi ni Simba damu.

Mheshimiwa Spika naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa ulinzi wake mpaka siku hii ya leo. Kwanza kabisa naomba nitoe pole kwa wazazi wa marehemu Amina Chifupa Mpakanjia pamoja na Wabunge na Vijana wote nchi nzima kwa kumpoteza mwenzetu. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

Pili, naomba nitoe salamu za rambirambi na pole kwa ajali zote zilizotokea katika sehemu mbalimbali. Kuna ambao waliofariki na kuna wengine wapo hospitali. Vilevile kwa hao waliofariki Mwenyezi mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri ambayo aliyoifanya kuhamasisha Naibu Mawaziri kwenda Mikoani ili kuweza kuhamasisha Elimu na kweli jitihada hizo zilizofanyika zimefanikiwa kwa kiwango kikubwa sana

Naomba nimpongeze Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi pamoja na Manaibu wake kwa kazi nzuri na ushirikiano wao wanaoufanya kwa kuhakikisha elimu yetu iweze kupaa. Naomba pia nimpongeze Mkuu wetu wa Mkoa wa Rukwa kwa juhudi ambazo anazifanya kwa ajili ya elimu na kwa kusema kweli anafanya juhudi ambazo zinatupa matumaini kwa Mkoa wetu wa Rukwa. Anajitahidi sana na naomba nimpongeze kwa juhudi zake hizo anazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nianze kwa ujenzi wa madarasa, nyumba na maabara. Kuna nyumba ambazo zimejengwa huko vijijini kwenye shule za Kata. Wale makandarasi hawakujenga vizuri. Kwa kuwa tuna Jeshi la Kujenga Taifa na kwa kuwa Jeshi letu sasa hivi lipo katika hali ya utulivu, halina kazi nyingi kwa sababu ya nchi yetu kuwa na amani, wanajenga majengo, madaraja kila sehemu kwa ufanisi mkubwa sana, napendekeza kuwa Serikali ilitumie Jeshi letu ili liweze kujenga nyumba za Walimu, madarasa pamoja na maabara. Jeshi la Kujenga Taifa ni la Serikali kwa hiyo, zile pesa zitakazotolewa zitaingia ndani ya Serikali na watajenga kwa ufanisi mzuri zaidi kwa sababu wanajua hiki ni chombo cha Serikali.(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza Serikali ione umuhimu wa kulitumia Jeshi hili ili malalamiko kuhusu Walimu kuwa wanatumia hela vibaya, wanakwenda, *sub-treasury* kule wanahangaika, usumbufu huo sasa uweze kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta muda mwingi walimu wakuu wanaenda *Sub-Treasury*. Kama sisi kwetu Mpanda, inabidi watoke Mpanda waende Sumbawanga kwa ajili ya kufuatilia fedha za ujenzi. Sasa muda mwingi wanatumia kule, utakuta *Sub-Treasury* yenyewe inasumbua na nini, huku watoto wanakosa masomo na usimamizi unakuwa mdogo kwa wanafunzi. Napendekeza Jeshi la Kujenga Taifa liweze kusimamia ujenzi wa shule za sekondari hizi za Kata ili ufanisi wa majengo uwe mzuri kwa sababu ni kitu ambacho tunajua Jeshi haliwezi kutuangusha kwa kuwa ni watu makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo ya walimu, mimi nashauri Serikali itoe ada kwa walimu hawa ambao wanaenda kusomea ualimu maana yake sasa hivi ada ya chuo ni shilingi 150,000/=. Ili tuweze kupata walimu wengi na waweze kujiunga katika chuo, maana kuna wengine hawana uwezo na wana nia ya kwenda vyuo vya ualimu, shilingi 150,000/= hawana!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iweze kuwasaidia hawa watu ambao hawana uwezo na wana nia kweli ya kwenda kujiunga na vyuo vyetu vya ualimu. Ili na sisi tuweze kupata walimu wengi, hii ada itolewe. Kwa mfano, tuone kama Polisi, Chuo cha Polisi kile cha Moshi wanasoma bure, Uhamiaji wanasoma bure, mafunzo yao ni bure! Sasa, je, kwa nini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, isiwafundishe walimu bure? Tunapendekeza, ili walimu waweze kuwa wengi na sasa hivi tunasema tunajenga shule nyingi za walimu, basi tutoe ada za walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wanaofaulu vizuri kutoka sekondari wale ambao tunawapangia kwenda vyuo vya ualimu tuwaondolee ada hii ya shilingi150,000/=

ili na wenyewe waweze kujikimu mambo madogo madogo. Naomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, iweze kuwafikiria hawa watu wanaotaka kujiunga na vyuo vya ualimu wasamehewe ada, maana yake shilingi 150,000/= ni nyingi, unakuta wazazi wengine hawana uwezo, amejitahidi kumsomesha mtoto kwenye shule ya Kata kuanzia *form one* mpaka *form four,* lakini kwa kuwa kule ada ni ndogo, shilingi 20,000/= ameweza, ameimudu, lakini, shilingi 150,000/= atashindwa. Sasa naomba Serikali iweze kuangalia, je, hawa walimu wanaoingia katika vyuo, wanaweza kuwapunguzia hiyo shilingi 150,000? Naomba Serikali mfikirie kiwango hicho cha shilingi 150,000/=, aidha, mkipunguze kidogo au muwasamehe kabisa kama wanavyofanya Polisi pamoja Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu wanahangaika sana kule Wizarani kufuatilia madai yao, posho zao, likizo, mapunjo ya mishahara, matibabu na uhamisho, pesa zao hawapati kwa urahisi. Sasa sijui Wizarani kuna matatizo gani? Unakuta mwalimu anakaa mwaka mmoja anadai madai yake ya likizo au mapunjo ya mishahara na unakuta huyo mtu anakaa mbali, Mkoa wa Rukwa, mbali mpaka afike Dar es Salaam kuja kufuatilia posho. Ule muda anaopoteza kuja labda Dar es Salaam kufuatilia au anakaa vijijini kwenda Wilayani kufuatilia mapunjo ya mishahara au posho, unakuwa usumbufu, watoto wanashindwa kupata mafunzo yao kwa wakati. Muda mwingi walimu wanafuatilia Wilayani mapunjo ya mishahara yao, likizo, matibabu, hawapati mapema. Naomba Serikali iweze kufuatilia jambo hili ili wale walimu wanaokaa vijijini waweze kupata huduma hiyo kwa wepesi zaidi kuliko kuwaacha wanafunzi wakiwa wanahangaika huko, wenyewe wanakuja Wilayani au Mikoani kuja kufutilia madai yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ijenge shule nyingi za mabweni kutokana na hali halisi ya watoto wa kike wanavyohangaika. Watoto wa kike wanapata vishawishi kutokana na shule za *day* au unakuta katika shule hizi za Kata tulizozijenga, kutoka shule hadi kijiji ni mbali na shule nyingi za Kata zimejengwa hivyo, wanatembea muda mrefu, wanachoka. Akitoka kijijini mpaka afike shule ya Kata, amechoka. Hatakuwa makini au kuwa msikivu, anashidwa kutokana na zile maili alizotembea, akili inakuwa imeshachoka na njaa vile vile. Nashauri Serikali ijaribu kutujengea mabweni ili wanafunzi, mabinti zetu wasipate vishawishi maana huko njiani, wanaweza wakapata vishawishi mbalimbali, masomo yanaweza kuwa hafifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani sisi tulipokuwa tunasoma, tulikuwa tukienda shuleni, tunakaa *assembly*, tunakaguliwa vizuri sana. Lakini sasa hivi naona shule za *primary* walimu wamekuwa hawawakagui hawa watoto, unakuta mtoto wa *primary* anapaka wanja na *lipstick* anaenda shuleni. Mtoto mdogo kweli, ina maana hakuna kukaguliwa ile asubuhi, maana asubuhi lazima wanafunzi wakae *assembly* waweze kukaguliwa. Lakini hiyo haipo! Unakuta mtoto kapaka wanja, ina maana mwalimu hakumwona yule mtoto! Yale maadili yaliyokuwepo wakati sisi tunasoma, naona sasa hivi yamepungua kidogo.

Naomba Serikali ifuatilie kuwahimiza walimu wa shule za *primary* kufanya ukaguzi. Zamani tulikuwa tunakaguliwa Jumatatu na Jumatano. Mzazi wa pili ni mwalimu, lazima wanafunzi wakaguliwe shuleni. Sasa hivi shuleni unakuta kengele ikigongwa, moja kwa moja wanaingia madarasani. Naomba Serikali ikumbuke

kuwafuatilia walimu wa shule za msingi ili wanafunzi wetu waweze kukaguliwa ili maadili ya watoto wetu yawe mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Sumbawanga tuna chuo, kile chuo, naomba Serikali ikipandishe gredi ili tuweze kupata walimu wa *primary* pamoja na walimu wa shule za sekondari.

**NAIBU SPIKA:** Chuo gani hicho?

**MHE. ANNA. R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Sumbawanga cha Ualimu! Naiomba Serikali ikipandishe gredi ili tuweze kupata walimu wa shule za msingi pamoja na sekondari kutokana na hali halisi ya Mkoa wa Rukwa kuwa na walimu wachache.

Vile vile tunaomba tupongeze, kuna walimu waliojiunga kundi ambao wanatafuta walimu katika vyuo mbalimbali kuwaleta Mkoa wa Rukwa na tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa. Lakini vile vile, ingawa tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa, naomba Serikali ikiongezee gredi hiki Chuo cha Sumbawanga ili tuweze kupata walimu wa shule za msingi pamoja na walimu wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo mimi naomba niishie hapa hapa. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaunga mkono hoja! *(Makofi)*

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii nyeti ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. *(Makofi)*

Kabla sijaanza kuchangia, ningependa nianze kwa kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Namwomba Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nitoe salaam za rambirambi pia kwa wale wafanyakazi wa *Nyanza Cooperative Union* waliopata ajali walipokuwa wakienda kazini Singida, nao pia Mungu awaweke mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru wananchi wangu wa Mkoa wa Mara hususan Mkuu wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya zote tano, viongozi wote wa Chama na Serikali kwa ushirikiano mzuri wanaonipa ili niweze kutekeleza vizuri kazi yangu ya Kibunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze sasa kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Napenda kuipongeza Serikali kwa kuifikiria Wizara hii kwa kuipa kipaumbele kwa asilimia 18 ya Bajeti nzima kwa mwaka huu wa fedha. Kwa kweli jambo hili ni jambo la kujivunia sana kwani sote tunaamini kwamba hakuna Taifa au nchi ambayo inaweza kuendelea bila watu wake kujikomboa kutoka kwenye ujinga.

Changamoto tuliyonayo au waliyonayo wafanyakazi na watendaji wa Wizara hii ni namna tu wanavyoweza kuitumia Bajeti hii vizuri kwa kuendeleza kwa kasi na kwa umakini mkubwa mipango yote ya maendeleo iliyopangwa na Wizara hii na pia kuhakikisha kunakuwepo na uwiano mzuri kati ya matumizi ya ndani na yale ya mipango ya maendeleo iliyojipangia Wizara hii, isije mwisho wa mwaka tukauta kwamba matumizi ya ndani yamekuwa makubwa kuliko pesa zilizowekwa kwa mipango ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba moja kwa moja nijielekeze kwenye mkakati wa kimaendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) na pia MMES. Napenda kuchukua fursa hii, kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyofanya hususan kupitia kwa Waziri Mkuu kwa kuwahimiza Naibu Mawaziri wote katika kutekeleza mpango mzima wa ujenzi wa shule za msingi na pia shule za sekondari. Lakini katika kila kilicho kizuri, hakikosi kuwa na kasoro, mpango huu, umekuwa na kasoro kidogo kwani haukuzingatia kabisa hali zote za wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wanafunzi wenye ulemavu, lakini shule hizi zimejengwa kwa kutumia ramani za kawaida na kuwaacha wale wanafunzi wenye ulemavu washindwe hata kutumia haya madarasa. Madarasa haya yamejengwa, zimewekwa ngazi, lakini Serikali au Wizara haikufikiria kama ndani ya yale madarasa watapatikana watoto ambao wana ulemavu, kwa hiyo waweze kuweka *slopes* ambazo zitawawezesha watoto hawa hata kama wanatumia *wheel chairs* waweze kuingia darasani na kutoka darasani na kuwaondolea adha ambayo ipo sasa hivi ya kubebwa na wanafunzi wenzao mara wanapotaka kuingia na kutoka darasani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu Waziri wakati anafanya majumuisho, atueleze ni kwa nini mpango huu haukuzingatia ramani zilizopo katika kujenga madarasa ambayo yatakidhi aina zote za wanafunzi. Vile vile, mpango huu umeacha wazi na umelipiga teke suala la kujenga vyoo na hasa vyoo kwa ajili ya wanafunzi ambao wana ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanikiwa kufanya ziara katika Wilaya yangu ya Musoma Vijijini. Kule nilisikitishwa sana kwa sababu nilikuta…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, una hakika unasema wamepiga teke au unataka kusema vinginevyo! Kupiga teke! Tafuta neno lingine zaidi!

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda nisahihishe, wamesahau, hawakuzingatia kwamba kuna watoto walemavu ambao watatakiwa kutumia aina fulani ya vyoo. Kwa hiyo, niliomba suala hili liingizwe katika mpango mzima wa MMEM na MMES, vyoo vijengwe kwa kuzingatia aina zote za watoto waliopo shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ningependa kuongelea katika mpango huo huo wa MMEM na MMES, uhafifu wa ujenzi wa Maabara. Wasiwasi wangu ni kwamba katika siku zijazo, wataalamu kama madaktari, wahandisi, wafamasia na

wataalamu wengine wote wanaotokana na masomo ya sayansi watatoweka kabisa na kusababisha nchi kuagiza wataalamu hawa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuongelea ni suala la shule maalumu kwa maana ya kwamba shule za watoto wenye ulemavu. Hapa nazungumzia zile shule ambazo zinashughulika na hawa watoto wenye ulemavu wa akili, ulemavu wa masikio na vile vile ulemavu wa kuona yaani vipofu. Katika shule hizi kumekuwa na upungufu wa vifaa vya kufundishia na vile vya kujifundisha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba wakati Waziri anapofanya majumuisho, atueleze ni mkakati gani basi Wizara hii imeandaa kwa ajili ya kuhakikisha kunakuwepo uwiano kati ya mtoto na vitu vya kujifundishia, kwa sababu unakuta kunakuwepo na kifaa kimoja au vifaa vichache vinakuwa haviharakishi ule ufundishaji au ufundishwaji. Kwa hiyo, naomba Waziri atueleze mikakati mizima kuhusiana na shule hizi za watoto wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuongelea suala la shule binafsi. Sote tunafurahi kwamba shule hizi ni nyingi na zinatoa huduma nzuri kweli, tunafurahi. Lakini mimi nina wasiwasi kidogo hapa, katika shule hizi kumekuwepo na walimu wengi sana ambao ni wageni kutoka Kenya na kutoka Uganda.

Mheshimiwa Spika, tunaelewa kwamba kweli nchi yetu ina upungufu wa walimu, lakini tatizo langu ni kwamba, je, tuna hakika gani kwamba walimu hao wanaokuja kufundisha shule hizi kweli wana sifa zile za kuwa walimu au ni basi tu mtu ametoka Kenya amekuja hapa, anajua Kiingereza, basi anaajiriwa kwenye hizi shule za watu binafsi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, ijaribu kuhakiki walimu hawa ili tuweze kujua je, wana uhalali wa kuishi na kufanya kazi hapa nchini na vyeti vyao. Kuwepo na chombo maalumu ambacho kitaweza kuthibitisha vyeti vyao na mimi vile vile nashauri, kama inawezekana, basi walimu wetu Watanzania waajiriwe kwa wingi kwenye shule hizi kwani wao ndio tuna uhakika kabisa wa vyeti vyao kwani tunaweza tukavihakikisha na kujua kwamba kweli hawa ni walimu halali na wanaweza kufundisha kwenye shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu hapa Wizara itueleze na chombo cha walimu kiko hapa, naona watu wote wanaohusika wako hapa ndani. Ningependa tu watueleze ni kwa nini hakuna chombo cha kuzingatia suala hili na kulinda ajira za walimu wetu, kwa sababu mimi nina imani, tunasema kwamba walimu ni wachache, lakini kuna walimu wengine wako mitaani hawana kazi. Kwa hiyo, kama kutakuwepo na chombo cha kulinda ajira za walimu, basi walimu hao wanaweza kuajiriwa na wahakikishe walimu hao wanaajiriwa kwenye shule hizi za watu binafsi. Kama kutakuwa na upungufu, basi waweze kufikiria kuajiri hawa walimu wa kutoka Kenya na Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchangia kwenye hotuba hii mpango mzima wa elimu kwa watu wazima. Kwa kweli kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake nikirejea kitabu, ukurasa namba 24, naona Wizara ina mikakati mingi sana juu ya mpango huu mzima. Kwa kweli mpango huu umekuwepo kuanzia muda mrefu sana kuanzia mwaka 1971, kumekuwepo na mpango huu wa kuendeleza watu wazima. Lakini ni dhahiri na ni lazima tukubali kwamba mpango huu utekelezaji wake umekuwa ni hafifu sana. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri anapofanya majumuisho, atueleze ni kwa nini mpango huu umekuwa ni hafifu sana, kwa sababu tunajua watu wengi wanaoishi vijijini, hawajui kusoma wala kuandika na kama hawajui kusoma wala kuandika, basi vipato vyao na maisha yao siku zote yatakuwa duni.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba je, tangu mkakati huu umeanza, wameandaa mazingira gani na ni sehemu gani ambazo wameziandaa ambazo zinafundisha watu hao wazima? Basi atueleze! Amesema kwamba watu 16,000 wamepatiwa elimu hii, ukilinganisha na idadi ya watu katika nchi yetu, bado hao watu 16,000 ni wachache sana na ningeomba tu watueleze wana mkakati gani wa kuongeza idadi hiyo kutoka 16,000 ili iendane na maisha ya sasa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo napenda kuongelea ni hili wimbi ambalo limejitokeza hivi sasa la watoto wa kike kupata mimba na kuolewa wakiwa wadogo sana. Tatizo hili, ukiachilia mikoa mingine, kwa kweli katika Mkoa wangu wa Mara, tatizo hili limekuwa kubwa mno hususan Wilaya ya Tarime. Kumekuwepo na tatizo la walimu kuwapatia mimba wanafunzi. Sasa mimi hapa najiuliza, wanafunzi tunawapeleka shule kusoma, kule shuleni walimu wanaacha kazi yao ya ualimu wanafanya kazi tofauti kabisa ya kuwapa mimba wanafunzi, kweli, uhalali uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Wizara ichukue kwa umakini kabisa suala hili, kwa kweli imekuwa ni tatizo sugu na ile adhabu ambayo walimu wanapewa, kuna baadhi ya Wilaya, walimu wameonekana kuhamishwa. Mwalimu anayetoa mimba sana, basi anahamishwa kutoka Wilaya hii, anapelekwa Wilaya nyingine. Kwa kweli mimi naomba hapa isitumike hiyo adhabu au ile adhabu ya kulipa shilingi 10,000/=, adhabu hii imepitwa na wakati. Naomba watu hawa wachukuliwe kama wabakaji! Kwa hiyo, ile adhabu, wanayopewa wabakaji kwa kufungwa miaka 30, basi ielekezwe kwa walimu hawa ambao wanawapa mimba watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kumetokea tatizo kwa wanafunzi kuachishwa masomo, wanaolewa. Unakuta mzee mzima kabisa na akili zake anaenda kuoa kitoto kidogo cha darasa la tano, eti kwa sababu ana ng'ombe wengi. Hili tatizo ni sugu kabisa hasa katika Wilaya yangu ya Musoma Vijijini, watoto wameolewa wadogo sana, inasikitisha. Watoto wanapofika darasa la saba, unakuta idadi ya wasichana ni wachache, ukiuliza wako wapi, unaambiwa wote wameshaolewa!

Kwa hiyo, naomba Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, aunde mkakati maalumu ambao utawasimamia watoto hawa. Wakati mwingine unakuta mtoto hapendi kuolewa, lakini baba ameshachukua ng'ombe, labda mtu akiwa mweupe kama mimi, ng'ombe 50. Basi unakuta yule mzee anaingia tamaa, mtoto akishaingia tu darasa la tano,

anachukua ng'ombe 50. Hapa usawa uko wapi na haki ya binadamu hapa iko wapi? Je, Wizara wanalijua hili kama kuna vijiji ambavyo watoto wanaolewa wakiwa darasa la tano? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tufikirie mtoto wa darasa la tano, anaweza kumtunza mume? Anaweza kuzaa mtoto? Matokeo yake, ndio maana tunajikuta kwamba kunakuwa na vifo vingi sana vya mama wajawazito kwa sababu mama wajawazito wengi wanazaa chini ya umri unaokubalika. Kwa hiyo, naomba Wizara ishirikiane na Mheshimiwa Rais. Hili suala pia linamkera sana Mheshimiwa Rais, lakini, je, Wizara mmejipanga vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba wakati mnafanya majumuisho, suala hili ni la muhimu sana mtueleze mikakati ambayo mmeipanga katika suala zima la watoto kupata mimba hasa wale wanaopewa mimba na walimu na wale watoto wanaoolewa wakiwa darasa la tano na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja hii kwa aslimia mia moja! Ahsante sana! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Kabla sijamwita Mheshimwa Magreth Mkanga, nimepokea ujumbe kutoka kwa Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, anasema; "Mheshimiwa Naibu Spika, sahihisho, salaam! Naomba sana Waheshimiwa Wabunge wapende kutumia neno la wasioona badala ya vipofu, hii ni sababu ya kuepusha unyanyapaaji." *(Makofi)*

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kabla sijaendelea, naomba niungane na salaam zilizotoka kwa mwenzangu, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji kwamba….

Naomba tu nitoe tu msamiati kidogo tu basi ambao wenzenu utatufanya tujisikie vizuri. Vipofu hawaitwi vipofu, wanaitwa wasioona, wasiosikia, hawaitwi wasiosikia, kwa sababu wasiosikia ni watukutu, wanaitwa viziwi, kwamba kuna matatizo nta imekwishaingia mtu hawezi hata kupenyeza sauti. Hatuiti wasiosikia kwa sababu wasiosikia ni watukutu. Viwete hatuitwi viwete kama Mkanga hapa, mimi ukiniita hivyo kwa vile nina gongo naweza nikakupiga. *(Makofi)*

Mimi nina ulemavu wa viungo na ni vya aina nyingi, kama ni mkono, kama ni mguu, kama ni nini, ni ulemavu wa viungo. Wenzetu wenye matatizo ya vichwa, hawaitwi vichaa, kuna vichaa wanaojitakia kwa bangi, lakini kuna mtoto alizaliwa ubongo kidogo ukawa na matatizo au tu kwa ajali, wale wanaitwa walemavu wa akili na siyo vichaa kwa sababu vichaa kwa kweli ni kitu tofauti kabisa. Kwa hiyo, ningeomba kidogo kuweza kusahihisha hayo ili kweli kama alivyosema mwenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninaomba nafasi hii iwe tu ni kwamba nilikuwa natoa elimu, lakini siyo kuchangia. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Basi umevunja Kanuni! Hatutahesabu hivyo! *(Kicheko)*

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru! Baada ya ufafanuzi huo mdogo, ningependa kwanza kutoa rambirambi za dhati kabisa kwa wengi tu ambao wameshatangulia mbele ya haki akiwemo mwenzetu aliyekuwa Mbunge, Mheshimiwa Amina Chifupa, mwanangu ambaye ni hivi majuzi tu amekwisha kwenda kwa Mungu. Pamoja na yeye kuna wengi, kwa jumla niseme tu, Mungu awasaidie, awarehemu, awalaze mahali pema peponi na sisi tuliobaki, basi tuendelee kuyaenzi yale ambayo waliyafanya kwa nia njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya rambirambi hizo ningependa kutoa pongezi za jumla kwa Wizara husika ambayo leo ndiyo tunaizungumzia nikinzia na kazi nzuri inayofanywa na Waziri, Mheshimiwa Margareth Sitta, Naibu Mawaziri wake wawili, watendaji na Katibu Mkuu. Lakini hawa wakielekezwa zaidi na kusimamiwa kabisa na jitihada na msukumo wa ziada wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimwa Waziri Mkuu ambaye katika ujenzi wa shule ambao baadaye umeleta hata usemi ambao Mheshimiwa Waziri leo ameuleta kwamba sasa tuseme ni karne ya kurekebisha au sijui kuboresha elimu, kwa kweli amefanya kazi nzuri sana kwa upande wa suala la elimu hasa kuhimiza ujenzi wa shule za sekondari. Pongezi zao ni nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza wewe, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wenu, mmekuwa mkituongoza kwa busara humu ndani. Wakati mwingine unaona mambo, unasema sijui yatakuwaje! Lakini kwa busara na kwamba mmeshafahamu na Kanuni, tunapigwa Kanuni mpaka tunajirekebisha na kuelewa la kufanya.

Pamoja na pongezi hizo ningependa kuchangia machache au mengi ndani ya hotuba hii. La kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Rosemary Kirigini aliyekaa. Imekuwa kama amenifilisi, lakini kwa kweli nimefarijika kwamba sasa Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo yetu tunafanya kazi hata na kuangalia masuala ya watu wenye ulemavu wakiwemo wanafunzi wetu na maeneo wanayosomea. Hilo mimi nimelifurahia sana sana! Amezungumzia sana kuhusu kutozingatiwa kwa mazingira rafiki ya majengo ya madarasa, vyoo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nimelisemea katika miaka yangu yote mitano ya nyuma na bado nitaendelea kusema. Hata mimi nasikitika katika Wizara mpaka leo hivi hakuna kinachozingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwishauliza na kujibiwa kwamba ramani husika zimeishatolewa kwenye Halmashauri, lakini inashangaza kwamba mimi sijaona mabadiliko ya mazingira ya majengo haya kutegemeana na hizo ramani ambazo naambiwa zimekwishakabidhiwa kwenye Halmashauri zetu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachoomba, nadhani katika kuhitimisha hapa, mwenzangu ameshasema kabisa, tatizo la *accessibility* ni kubwa. Kulikuwa na maonyesho hapa ya *NGOs* walikuja, nilibahatika kwenda kwenye *NGO* moja inayoshughulikia kutoa huduma kwa watu wenye ulemavu, nilikuta watoto wawili walemavu wa viungo, nikawauliza matatizo yenu ni nini katika shule, maana kuyasema

mimi inawezekana siyo. Kwa midomo yao walidhihirisha kwamba wana matatizo ya kuwa na majengo na vyoo visivyo rafiki kwao kiasi kwamba wanatumia kubebwa ama inabidi wajiburute na kushika uchafu tu katika maeneo ya maliwato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa karne hii na ulimwengu wa leo, bado hata hawa watoto wachache wanaoweza kusoma huko kwenye mazingira magumu ya namna hiyo, hali inakuwa mbaya kama hiyo! Naiomba Wizara inapomalizia inisaidie basi kunifafanulia, hivi nani huyu anaweka hizo ramani tunazosema zipo mwafaka kwa wao? Nani huyu katika Halmashauri? Nashauri basi kwamba shule kabla hazijafunguliwa, hazijaruhusiwa zifanye kazi, basi labda Wizara ichukue nafasi ya kuhakikisha kwamba hazifunguliwi mpaka majengo hayo yakidhi haja ya watoto wenye ulemavu, kwa sababu vinginevyo inakuwa ni wimbo wa kila siku na hakuna kinachotekelezwa. Kwa hiyo, naomba hilo nijibiwe tutakapokuwa tunamalizia yale yanayotuhusu kumalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiongeza baada ya hapo, mimi naona kama suala la *accessibility* halitajaliwa sana, tukawa tu na lugha ya kuendelea kulisemea, suala la elimu kwa wote wala hatutalifikia kimatendo, itakuwa ni nadharia tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nashauri kwa sababu Wizara imesema inaendelea kudurusu kupitia upya sera na sheria ya elimu, basi hili labda lizingatiwe kwamba labda pawepo na mkazo wa kisheria maalumu kwamba suala hili liweze kuzingatiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana na Wizara wametueleza kwamba wataongeza uandikishaji wa watoto shule za awali na shule za msingi. Mimi hilo nalipongeza sana, lakini pamoja na pongezi hizo nilikuwa naomba kufahamu Wizara imeweka mikakati gani madhubuti ya kuhakikisha kwamba watoto wenye ulemavu wanaopaswa kuingia shule za awali na msingi wataandikishwa wote hasa kwa kutoa maelekezo kwa watendaji wao. Kwa sababu ninalolifahamu mpaka sasa kuna walezi/wazazi ambao bado wanawaficha watoto wenye ulemavu kwenda shuleni. Tuangalie picha ya Kapeto, mimi ile inaniuma sana kwa sababu ndiyo hali halisi ya watoto wenye ulemavu walio wengi, baba anakataa au hata Wizara yenyewe imetoa maoni fulani, anasema kaka yuko humo ndani, yuko wapi, yeye amefichwa kwa sababu ni mlemavu. Sasa mna mikakati gani ya kuhakikisha kwamba akina Kapeto hawaendelee kukosa elimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kwenye upande wa elimu ya sekondari. Nimefurahishwa kwamba kuna shule ambazo zitarekebishiwa miundombinu yake ili iweze kukidhi haja ya mazingira ya watoto wenye ulemavu. Lakini nilikuwa naendelea kushauri hivi kwa nini katika hizi shule tunazozijenga sasa hivi hayo maboresho yasiendelee kuwemo kwa sababu hii hali ya kuwa na shule maalumu tu kwa ajili ya watoto wenye ulemavu za sekondari wakasome kule imekuwa ni tatizo, masafa ya kusafiri kwenda kwenye shule hizo wakishachaguliwa ni marefu, nauli na ghasia zote na watu kama sisi kutembea hivi ni matatizo. *(Makofi)*

Sasa kwa nini isiwe katika shule zetu hizi ili tukidhi haja hizi kusudi watoto hawa pia wasome kwenye maeneo yaliyo karibu kama wenzao. Serikali sasa hivi inajikita

kwenye dhana ya kuwa na elimu jumuishi. Sasa hapa ujumuishi utatoka wapi? Kama wale itabidi wasafiri kwenda mbali kwa sababu ni kiziwi akafuate shule Tabora, Ruvu. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri kwamba badala ya kupoteza muda na wakati hizi hizi shule tunazozijenga hebu tujaribu kupunguza adha za hawa watoto kwa kuzingatia mazingira yao muafaka kwenye hizi hizi shule tunazozijenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana na jitihada za Wizara kwamba wametuambia watahimiza ujenzi wa *hostels* kwenye shule zetu na hili limesemwa kwamba itajaribu kusaidia kupunguza mdondoko wa wasichana wanaoweza kupata mimba, mengi yamesemwa hapa.

Mimi nasema hivi naungana na Wizara kwamba jamani wakati umefika wa kuweza kuweka mikakati ya jinsi gani kuwasaidia wasichana wanaopata mimba baada ya kujifungua warudie masomo. Tusipofanya hivyo kwanza wengi wa hawa wanaokwama kwenye vishawishi ni watoto wanaotoka kwenye familia maskini. Sasa anapata mimba anaacha shule anakwenda kwenye umaskini wake ule ule wa baba yake na mama yake, akiongeza na mjukuu juu. Bado ile hali ya usawa wa wanawake na wanaume kupata elimu mimi siioni kwa misingi hii kwamba tutaifikia lini. Tuweke utaratibu maalumu kwa kweli hawa wanaoanguka kwenye majaribu na sababu tunazijua hapa kuozwa bila kutaka, kubakwa na kadhalika, adhabu inamuwia sasa mtoto wa kike. Yule wa kiume awe mtoto mwenzie, awe baba, baba ndiyo kabisa anaruka vihunzi 60 huko usiniambie kwamba mimi ndiye niliyekupa mimba anayeadhibika ni mtoto wa kike, usawa uko wapi hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kweli hili tulifanyie mkakati maalumu tuone vipi watoto wetu hawa waweze kusoma. Wala sipendezwi wala si-*encourage* kwamba wapate mimba, lakini wengi wanapata kwa bahati mbaya. Wengi wa hawa wangeweza kuwa watalaamu wazuri, wangeweza kuwa viongozi wazuri, lakini mimba tu hizo ndio zimewatia mkosi na kuwafanya waendelee kuwa wajinga na umaskini uweze kuendelea. Kwa hiyo, huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu kwamba wakati umefika wala hatutachekwa, tujaribu kuokoa watoto wetu wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niseme chochote kwenye sehemu ya elimu ya ualimu, nashukuru kuna mafunzo ambayo yataendelezwa na hasa ya kuwa na walimu wengi wa kutosha wa elimu maalumu waweze kuwasaidia watoto wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninachokiomba walimu wenye ulemavu kwa sasa hivi ni shule moja tu ya Patandi ndiyo ambayo wanafundisha nadhani. Lakini kumekuwa na malalamiko kwamba na wao wanajiunga wengi wakiwa wameshakuwa walimu, wanakwenda kujiendeleza, kumetokea malalamiko kwamba hawa wanaopenda kwenda kujiendeleza wakachukua sehemu hiyo ya elimu maalumu wanapata vikwazo. Kwanza wakimaliza hawapandishwi madaraja, wanasema wewe bado ni *certificate* sasa utakuwa na *certificate* mbili ile yako na hii kwa nini pasiwe na utaratibu wa kuwapa motisha kwa sababu hii ni kazi ya ziada ya kujitolea kwenda kusomea jinsi ya kuhangaika na mtoto mwenye ulemavu. Hawa wafikiriwe wapangiwe madaraja yao, *promotions* kama wengine ambavyo wanapangiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la elimu kwa ujumla ningependa nizungumzie licha ya vikwazo vya *accessibility,* vikwazo vya nyenzo za kufundishia na kujifunzia ambavyo Wizara imejitahidi kuanza kuviongeza, nipongeze sana shule za viziwi nilizotembelea Morogoro nimekuta kwa kweli wana vifaa vipya kabisa. Lakini sina hakika na maeneo mengine. Tatizo kubwa kwa watoto wenye ulemavu, viziwi wanaendelea kudai na kuhimiza Serikali umuhimu wa kutumia lugha ya alama. Bila ya lugha ya alama *(sign language)* kiziwi inakuwa ni tatizo kuelewa. Hili nalo Serikali kwa kweli hebu ilione kwa sababu kwa kweli kwa hawa tunajidanganya kwamba tunawasomesha kumbe la maana hakuna. Wanakuwepo darasani kama vile hawapo. Kwa hiyo, ningeomba *sign language* iweze kuhimizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukubaliana na Kamati yangu ya Huduma za Jamii ambayo imetoa mapendekezo kuwa na uwezekano wa kuwa na chombo cha ajira ya walimu wote nchini. Hawa ni kundi kubwa, wana matatizo mengi na usumbufu na urasimu mkubwa kwa sababu wanakuwa waajiriwa wengine chini ya Wizara ya Afya, wengine sijui chini ya Wizara ya nini, inapobidi kuomba marekebisho ya mishahara kwa kweli inakuwa ni tatizo.

Kwa hiyo, ningeomba sana suala hili liweze kuzingatiwa tuwe na chombo chao maalumu cha kuwaajiri, kusimamia maadili yao, kuwaadhibu wanapokosa na hata kuwalipa na kuwapandisha madaraja. Hiyo hata wa *private school* itabidi wakapate ruhusa ya kuajiri mtu huyo ambaye amekwisha kamilishwa kama chombo hicho kitakavyokuwa kinataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kusahau masuala ya madeni ya walimu na malimbikizo. Huu ni wimbo tangu miaka miwili/mitatu/minne. Hivi tatizo ni nini kwa nini tunaendelea kulimbikiza madeni haya ya walimu na ni lini yataweza kulipwa kabisa tukamaliza kabisa tatizo hili, kwa nini watendaji wanapopata zile *documents* hawawezi kuanza kuweka rekodi mapema ili malipo yaweze kufanyika mapema? Kimekuwa ni kilio cha siku nyingi na imekuwa kama vile sijui tunajisahau, suala la madeni ya walimu kwa kweli lishughulikiwe ili *agenda* hii iwe inafikia mwisho wake kwamba kila deni jipya linalipwa kuliko kuendelea kuwalimbikizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi nishukuru Wizara kwamba imeanza kuonyesha labda kuna maendeleo kwa upande wa elimu ya watu wenye ulemavu lakini bado jitihada ni kubwa, kuna asasi zingine zinaendesha mambo haya zenyewe naomba ruzuku kwa mfano za misheni zinazojitolea kuwahudumia watoto wenye ulemavu waweze kupewa kwa wakati na angalau ziwe za kutosha.

Mheshimiwa Naib Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na niwatakie heri nitataka kufahamu hivyo vifaa wanavyonunulia ni vipi na wanapeleka katika shule zipi watakapokuwa wanamalizia hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, badilisha *microphone* hatukusikii.

**MHE. PROF. FEETHAM F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu nichangie hoja ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwanza napenda kutoa rambirambi kwa wazazi wa Mbunge Mheshimiwa Amina Chifupa ambaye alifariki hivi karibuni. Kwa kuwa alikuwa Mbunge mwenzetu kwa kweli wote tuna majonzi makubwa na tunaomba rambirambi zetu ziwafikie wazazi na ndugu na marafiki wa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa pongezi kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kutoa hotuba nzuri. Mimi nitajikita katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ni mpango wa MMEM au ujenzi wa shule za msingi, sehemu ya pili itahusu ujenzi wa shule za sekondari na nitamalizia kwa kuzungumzia matatizo fulani yanayoikabili Wilaya ya Ngara. Elimu ya msingi MMEM, kwanza niishukuru Serikali kwa kuanzisha huu mpango wa MMEM. Kusema kweli huu mpango umekuwa wa mafanikio makubwa. Kama kuna *revolution* katika sekta ya elimu ni mafanikio ya Mpango wa Elimu ya Shule za Msingi (MMEM). Tukikumbuka mwaka wa 1974 wakati *UPE* ilipoanzishwa au ilipokuwa *declared* ya kwamba tupate *Universal Primary Education* tunajua kwamba hii programu ni kama ilishindikana na ilishindikana kwa sababu dhamira ya *international community* walikuwa hawataki sisi tupate *Universal Primary Education*.

Mheshimiwa Naibu Spika, imechukua karibu miaka 20 kuweza kufanikisha mpango wa *Universal Primary Education* na hii imetokana na mpango wa MMEM. Tukiangalia katika Wilaya ya Ngara karibu kila kijiji kina shule ya msingi. *Enrolment* (udahili) ni asilimia mia kwa mia kila mtoto aliopo mwenye umri wa miaka 7 mpaka 13 yuko katika shule ya msingi katika Wilaya ya Ngara. Matatizo ni kwamba walimu hawatoshi katika hizi shule. Tunajua ya kwamba kila unapopanua *service* ya aina fulani lazima kutajitokeza matatizo.

Kwa hiyo, wapigakura wa Wilaya ya Ngara wameniomba niiombe Serikali iongeze jitihada za kupeleka walimu watakaokwenda kufundisha katika shule za msingi. Kuna shule nyingi hazina walimu wa kutosha hasa shule zilizoko kwenye Tarafa ya Rulenge na Murusagamba ambazo ziko mbali kidogo na Makao Makuu ya Wilaya. Shule hizi zina matatizo makubwa ya walimu na mazingira ya kufundishia kwa kweli siyo mazuri.Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke jitihada za kupeleka walimu katika shule hizi za msingi hasa zile za Murusagamba, Muganza shule za Kata za Bugarama na shule za Nyakisasa zina *shortage* kubwa sana za walimu. Vile vile labda nizungumzie mishahara ya walimu, wakati mwingine mishahara inachelewa na walimu hasa wale wanaofundisha katika shule ambazo ziko mbali na Makao Makuu ya Wilaya, kusema kweli wanapata adha kubwa kuja kupata mishahara. Kwa hiyo, ningeomba Wizara ijitahidi katika kuleta mishahara mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimaliza hilo, nichangie elimu ya sekondari. Ngara shule za sekondari zimejengwa kila kata. Sasa hivi tuna shule za sekondari karibu 20 katika Wilaya, hakuna kata ambayo haina sekondari. Kilichofanya tufanikiwe katika mradi mzima wa ujenzi wa sekondari ni kwa kutumia fedha za mfuko wa *TASAF.* Katika mfuko huu Wilaya ya Ngara imepangiwa *1.2 billion shillings* na katika kuzungumza pale

Halmashauri na kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya na Mkoa, Kanali Mfulu tumefanikiwa ku-*allocate 50%* ya hizi fedha ambazo ni shilingi milioni 600 katika ujenzi wa sekondari. Kila kata imekuwa *allocated* shilingi milioni 50. Hizi shilingi milioni 50 zimeleta *revolution* katika ujenzi wa sekondari baada ya wananchi kuchangia. Serikali kuchangia shilingi milioni 50 kila kata, sekondari zilijengwa katika miezi mitatu, Januari mpaka Machi shule zote zilishajengwa.

Naishukuru Serikali kwanza kwa ku-*allocate* fedha za *TASAF* kwa sababu kila Wilaya imepata fedha za *TASAF*. Namshukuru Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi na Halmashauri nzima ya Ngara hasa Madiwani, kwa ushirikiano wao katika kufanikisha zoezi zima la ujenzi wa sekondari za kata. Hapa kuna tatizo. Tumejenga sekondari, lakini kuna *shortage* ya walimu. Sasa naiomba Serikali ituletee walimu wa kutosha kila shule iwe na walimu wa kutosha ili tubadilishe *level* ya *education* katika Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekondari, Ngara hatuna sekondari za *high school*. Kuna sekondari ya *high school* moja ambayo ni ya misheni. Sasa shule za misheni kusema ukweli zina matatizo yake. Kwanza lazima ulipe *fees* kubwa, sasa kuna sekondari mbili katika Wilaya ya Ngara, kuna sekondari ya Kabanga ambayo ni ya Serikali na kuna Sekondari ya Ngara Mjini ambayo ni ya Serikali. Tunaomba Serikali izi-*upgrade* hizi sekondari za kawaida ziweze kuwa *high school*. Tatizo ni kwamba tunahitaji *support* ya Serikali. Sisi kama Halmashauri na mimi kama Diwani tumeshaelekeza nguvu kidogo katika kujenga madarasa katika hizi sekondari. Lakini tunahitaji msaada wa Serikali ili kuzi-*convert* hizi sekondari za kawaida ziwe na *high school* ili tuweze ku-*absolve* wanafunzi wanaomaliza *form four* waingie *form five* hii itakuwa ni msaada mkubwa kwa Wilaya ya Ngara.

Sasa nijielekeze katika *Vocation Education (VETA)*. Wilaya ya Ngara hatuna shule ya ufundi. Tuna shule moja ambayo ni Chuo cha Maendeleo ya Jamii. Kwa sasa hivi hicho chuo cha Lemela kusema kweli hakitumiki, ni kama kimesahaulika. Hamna walimu, hakuna *training* yoyote inayofanyika pale. Sasa nichukue nafasi hii kuiomba Serikali ikigeuze hiki chuo kiwe Chuo cha *VETA* cha Wilaya. Kwa sababu kwenye *speech* ya Waziri amesema kila Wilaya itapata chuo cha *VETA*. Itakuwa ni rahisi sana kugeuza hiki chuo kuwa chuo cha *VETA* kwa sababu kina mashine *basic* za kupiga randa, mashine za umeme, mashine za *welding* zipo pale, lakini hazitumiki kwa sababu chuo hakipati *allocation* ya fedha ya kutosha. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kukigeuza hiki Chuo cha Lemela kiwe Chuo cha *VETA* na kitaleta faraja kubwa sana kwa wananchi wa Ngara ambao wanahitaji kusomea ufundi lakini hawana chuo cha kusomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nizungumzie elimu ya walimu. Mimi naweza kuzungumzia hili kwa sababu nimefaidika. Wako wanaobeza programu ya sekondari ya kuchukua vijana waliomaliza *form six* kuwapeleka shuleni katika mafunzo ya ualimu kwa mwezi mmoja kisha wakawapeleka shule waanze kufundisha kwamba siyo walimu wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikubaliani nao kwa sababu nilipokuwa *form one* mwaka 1963 nilifundishwa somo la hisabati na mwalimu aliyekuwa amemaliza *form four* na mimi nimekuwa Profesa. Mwalimu aliyenifundisha *physics form one* na *form two* alikuwa ni mwalimu aliyefika *form four* na hapa mimi nili-*pass high school physics*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sikubaliani nao kabisa kwamba ukimchukua kijana aliyemaliza *high school* ukimwelekeza namna ya kufundisha kwa mwezi mmoja huyo ni mwalimu kamili na anaweza kutuletea *revolution* katika *process* nzima ya *education*. Vile vile naweza kutoa mfano wa *pearce corps, pearce corps* walionifundisha mimi Kiingereza walinifundisha na wengine walikuwa hawajaingia hata siku moja katika shule za kufundisha. Lakini wametufundisha na mimi nili-*pass* lakini walitufundisha na mimi nili-*pass* Kiingereza *form six*. Kwa hiyo, watu wanaobeza programu ya Serikali hii *crash program* ya kuwapeleka vijana waliomaliza *form six* katika *training* fupi ya mwezi mmoja wakapelekwa shuleni hawa hawatutakii mema na inabidi tuwapuuze kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunahitaji kufanya *revolution* katika *education* ni lazima tuwe wabunifu katika ku-*implement program* nzima, tusiwasikilize watu ambao hawatutakii mema, wanasema mwalimu ni lazima akae darasani miaka miwili/mitatu.

Mimi sikubaliani nao na ninamsukuma Mheshimiwa Margaret Sitta, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, asiwasikilize wanaobeza programu nzima, programu hii ni nzuri na ndiyo itatuletea maendeleo katika kupambana na ujinga na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niseme naunga mkono hoja asilimia mia moja na hotuba ilikuwa nzuri na tumtakie maisha marefu Mheshimiwa Waziri, ili aweze kurekebisha matatizo yaliyojitokeza katika sekta ya elimu katika miaka iliyopita. Nashukuru sana. Ahsanteni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki hauwezi kutosha msemaji kwa dakika 15. Tutakapoingia mchana tutawaita Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji na Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili na wengine wajiandae. *(Makofi)*

*(Saa 6.53 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na majadiliano, nitamwita Mheshimiwa Benito Malangalila, nadhani hayupo, Mheshimiwa Job Ndugai, atafuatiwa na Mheshimiwa na Mheshimiwa Janeth Massaburi na Mheshimiwa Zuleikha Yusus Haji naye ajiandaye.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:**Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ili niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ninaanza kwa kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa hongera nyingi kwa Mheshimiwa Waziri wa Elimu ya Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Margaret Sitta, kwa hotuba nzuri. Pia nawapongeza Naibu Mawaziri wake wote wawili Mheshimiwa Mwantumu Mahiza na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, kwa kazi nzuri. Tukija pale Wizarani, Waheshimiwa Naibu Mawaziri hawa wawili mnatupokea vizuri na mnatujali sana. Muendelee na utaribu huo. *(Makofi)*

Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu moja kubwa kwanza, kwenye hotuba yako ukurasa wa 62, fungu 62(a) umezungumzia ahadi ya kutayarisha andiko la mradi wa ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika kila Wilaya na mnaandaa programu ya Kitaifa ya utekelezaji wa mradi huo. Hilo nawapongezeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kwa kweli kila Wilaya ipate vyuo vya aina hii. Ni muhimu mno tunasikia habari njema kwamba mnaandaa mradi na mnatengeneza andiko la programu. Lakini katika eneo hilo la elimu nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, Waziri wa Elimu mwenyewe, Mkuu wangu wa Mkoa wa Dodoma, Mkuu wangu wa Wilaya ya Kongwa, Ndugu Lemrisi Kipuyo kwa suala zima la ujenzi wa shule za sekondari, kazi kubwa sana imefanyika na bado kazi kubwa iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu wangu wa Wilaya, Mheshimiwa Kipuyo, mwaka jana katika kuhimiza hizi sekondari, alizolewa na maji kwenye mto wa msimu, karibu apoteze maisha yake. Ile gari ikawa *right off* haiko barabarani mpaka leo. Wakaponea na *DAS* kwa kutokea dirishani, iko kazi kubwa sana imefanyika. Kwa kweli nawapongeza nyote kabisa. *(Makofi)*

Lakini pia nazipongeza Halmashauri zote nchini na hasa Halmashauri yangu ya Kongwa kwa kazi nzuri waliyofanya katika kusimamia kazi hii ya ujenzi wa sekondari. Sikuona tu katika kitabu chetu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri mahali akiwataja Halmashauri. Wamefanya kazi kubwa sana. Wamekuwa ni viungo muhimu sana. Bila wao sidhani kama tungeweza kufika pale tulipoweza kufika. Kwa sababu sehemu kubwa ya kazi hii imefanywa kwa uchangiaji wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niupongeze Mkoa wa Dodoma kwa kuwa wa kwanza safari hii katika matokeo ya mtihani wa darasa saba uliopita Kitaifa maana haijapata kutoka huko nyuma, kumbe mambo haya yanawezekana. Watu wakishaamka maana yake wameamka, sasa hata Wagogo tumeamka sasa tunakuwa wa kwanza Kitaifa, mtu yeyote asitegemee tutarudi nyuma. Sasa kazi ni moja tu kwenda mbele. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2000 Wilaya ya Kongwa ilikuwa na sekondari tatu tu. Sekondari hizo tatu zilikuwa haziwezi kujaza sekondari moja wanafunzi wake. Lakini leo hii shule za binafsi na za Serikali itakapofika mwezi Januari 2008, tunatarajia kuwa na shule za sekondari 30 kutoka tatu hadi 30 katika kipindi hiki kifupi sana. Katika idadi hiyo karibu 15 zimejengwa katika kipindi hiki cha mwaka mmoja na nusu ya Awamu ya Nne ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nikaanza na kutoa pongezi nyingi sana. Tumejenga mashule mpaka kule ambako ilikuwa si rahisi kutarajia kwamba pangeweza kuwa na shule. Kule Nyumbi leo kuna shule sekondari, vijana wako shuleni. Kule Ibwaga, kule Chiwe, Songambele, Norini, Makawa na kwingine ambako ungefikiria kwa akili ya kawaida ingechukua miaka 20, 25 ijayo. Lakini leo sekondari zimeanzishwa na vijana wako shuleni hivi sasa wanasoma kidato cha kwanza na kidato cha pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kuchukua kwa miaka miwili mfululizo wanafunzi wote waliofanya mtihani wa darasa la saba, mwaka juzi na mwaka jana tumechukua wote kabisa. Ndiyo maana nikasema naipongeza Serikali, nampongeza sana kipekee Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kulisimamia hili na ningeliomba liendelee kusimamiwa hili la sekondari. Huo ni mwanzo mzuri kwetu sisi. Itatusaidia sana huko tunakoenda.

Mheshimiwa Waziri, amezungumza kwenye kitabu chake ukurasa wa 13 kwamba mwaka 2005 Kitaifa kulikuwa na shule 1202 Kitaifa na mwaka 2007 ziko shule 2274. Hii imewezesha asilimia 85.6 ya watoto wote nchi hii waliofanya mtihani wa darasa la saba kwenda sekondari kutoka asilimia 48.6 ya mwaka 2006. Tusipopongeza, tutakuwa watu wa ajabu sana. Ni kazi nzuri imefanyika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi tunakupongezeni sana na wananchi wa Tanzania kwa ujumla tuendelee na utaratibu huu utatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inathibitisha maneno ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaweka katika ukurasa wa kwanza katika kitabu chake, aliyoyanukulu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ambapo aliwaambia Oktoba 11, 2006 kwamba nawahakikishia kuwa mnayo Serikali inayosikia, inayosikiliza, inayojali na iliyo tayari kuchukua hatua. Tunayo dhamira ya dhati ya kuboresha elimu kwa kuboresha huduma kwa walimu, kwa kuongeza walimu, pamoja na mazingira yao ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya niyaseme mwanzo yanathibitisha usemi huo muhimu. Tungependa kwa niaba ya watu wa Kongwa, tushukuru sana Serikali kwa utaratibu huu vinginevyo sisi wengine tungebakia kuwa wa mwisho daima. Lakini sasa tunapeleka watoto wote sekondari, wakifika *form four* hata kama nusu itaenda *form five* au robo itaenda *form five* nina hakika Chuo Kikuu kinachojengwa Dodoma hapa miaka michache ijayo, watoto wa Kongwa watakuwepo kwa mamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwendo huu hata Wilaya nyingine ziko hivyo hivyo kiasi kwamba matarajio yangu ni kwamba ndani ya miaka 10 ijayo kutakuwa na

uwiano kielimu nchi nzima hii. Kwa maana ya elimu ya Chuo Kikuu na wanaomaliza Chuo Kikuu. Naomba tu kwamba madarasa mapya yatakayojengwa nchi nzima, *form one* mpaka *form four* mgao pia Kongwa tupate wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamekuwa na migao mara sijui walioko pembezoni, mara walioko wapi, hebu tutoe tu kama tulivyofanya kwenye MMES na kwenye MMEM, tujaribu kutoa kwa haki, kwa idadi ya watoto waliopo ili iondoe manung'uniko madogo madogo. Lakini vile vile kidato cha tano na sita kuna madarasa ambayo mmeyatengea Bajeti. Tungeliomba zile Wilaya ambazo hatuna kidato cha tano na sita kama Kongwa na sisi mtutengee tuanze maandalizi ya kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnapofanya hivyo hamuanzi ninyi, sisi tumeshaanza tayari kuchangishana na kutumia nguvu zetu kuhakikisha kwamba hicho kidogo mtakachotupatia tutapiga maili kubwa zaidi. Matarajio yetu ni kuanzisha shule tatu za sekondari za kidato cha tano na sita kule Mkoka, Mlali na Kongwa Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo tatizo kwa shule zetu za msingi na shule za sekondari kubwa sana kwa walimu wa masomo ya Kiingereza, somo la Hesabu na Sayansi kwa ujumla. Kila walimu wakikaa mwanzo wa muhula, *staff room* kugawana masomo, walio wengi wanayakimbia masomo hayo ama kwa kutoyaweza, kutoyamudu au vingevyo. Sasa ningependa kushauri hebu Wizara iangalie namna ya kumotisha walimu wa masomo ya sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kitabu kinasema mwaka jana walimu wanafunzi chuo kile cha Iringa walikuwa 97 tu wa Hesabu. Hata ukiwagawa kwa mkoa wa Dodoma mmoja mmoja kila shule bado hawatoshi, maana yake liko tatizo la hakika hapa. Hesabu siyo kitu rahisi, *Physics, Chemistry, Biology.* Mtu kusoma *PCB, PCM* siyo jambo rahisi. Kwa hiyo, wanapomaliza watu wa namna hii ambao tunawahitaji kweli kweli tunataka dunia ya sayansi na teknolojia basi hata *package* yao itazamwe ili watiwe moyo walimu wengi zaidi kufundisha masomo haya ya sayansi, vinginevyo tutazungumza tu kwamba dunia ya sayansi na teknolojia lakini itakuwa vigumu kuwapata walimu watakaofundisha mambo haya. Lakini pili, ili tupate uboresho katika masuala ya sayansi na teknolojia hata wanafunzi wanapomaliza basi mishahara yao itazamwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anamaliza Uhandisi, mshahara anaopata sitaki kulinganisha na taaluma zingine. Tutazame tu utaratibu wake ukoje. Hivi pale Mlimani kweli *Engineering* ni sawa sawa na mambo mengine au kama kule *Faculty of Science* wanaumia kweli. Enzi zetu sisi *Faculty of Science* unaanza *first year* mko 70 mnaingia *second year* mko 30 na mnamaliza 20, ukija kwenye mshahara hamna kitu cha maana. Ukija huku duniani wanaotawala sio wale walioumia sana. Lakini hatukatai sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji *administrators* na kadhalika, hawa ma-*scientists* wamesahauliwa, nchi za wenzetu zilizoinuka ziliwatazama kipekee hawa. Hatuwezi kusema kwamba tuwawezeshe vijana, wasome *science and technology* wakati

wakimaliza masomo yao wakija mtaani, hakuna anayewajali na kujaliwa siku hizi watu wanaangalia *package* bwana. Huwezi kusema tu sayansi na teknolojia ukaumia huko *PGM, PCM* halafu ukimaliza hakuna *package* ya maana unazidiwa na mtu aliyesoma Kiswahili tunachokijua wote.

Kwa hiyo, mambo haya yatazamwe hata kwenye mishahara, hata kwenye taratibu zingine ili yaweze kuwatia moyo vijana wajisikie kweli wawe wanasoma sayansi kwamba wanahitajika na ni sehemu muhimu ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niseme neno moja dogo kuhusiana na matangazo ya kwenye televisheni ya Haki Elimu. Kama nilivyo-*declare interest* yangu mapema mimi nimesoma sayansi, sikusoma usanii. Kwa hiyo, wakati mwingine naweza nikakosea kidogo lakini matangazo yale nia yake nini hasa, yaliyo mengi, yanatuletea picha ambayo sina hakika nayo sana. Niiambie tu Serikali kwamba kule Zambia wakati ule Rais Mzee Keneth Kaunda na *UNIP* yake wanaanguka kwa sababu ya matangazo ya rejareja kama haya, yana-*potray UNIP* gari bovu, linakwenda katika barabara za mashimo, gari linaporomoka poromoka hivi, halafu yana-*protray MMB* barabara ya lami na gari nzuri zinapita, yupo wapi Mzee keneth Kaunda leo?

Sasa kama wenzetu hawa nao ni chama cha siasa wangejiandikisha vizuri wakaeleweka. Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi utakapokuwa unaainisha masuala hapa mwishoni, utueleze mbona hatuelewi elewi haya maneno yakoje ya Haki Elimu. Hapa unaweza kuwa na matangazo mazuri zaidi yanayosaidia zaidi juhudi hizi zote ya kuboresha elimu, lakini matangazo yanayotoka ni ya ajabu kidogo. Tusaidiane, kama yako sawa sawa atatueleza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, lakini mimi nina shaka nayo kidogo. *(Makofi)*

Namalizia kwa kuwashukuru sana wananchi wa Kongwa, kwa maendeleo makubwa ya elimu ambayo tumeyafanya. Mimi naamini ngwe iliyo mbele yetu bado ni kubwa tukishirikiana na *DC* wetu kama nilivyosema mwanzo na nampongeza sana Mheshimiwa Lembulisi Kivuyo, pamoja na watumishi wengi wa Halmashauri na wananchi kwa ujumla tutapiga hatua kubwa mbele. Matumaini yangu ni kwamba Chuo Kikuu cha Dodoma kinachojengwa hapa hapa Dodoma na vyuo vingine vikuu nchini katika miaka mitano, sita, saba ijayo, nina hakika tutakuwa na mamia ya wanafunzi wakitokea Kongwa.Tukifanya kwa pamoja tunaweza kuibadilisha kabisa Kongwa kutoka Wilaya maskini ya mwisho mwisho inayochekwa na kila mtu isiyo kuwa na hata Katibu Tarafa mmoja nchi nzima ya Tanzania, haina mtu katika utawala wa maana, wa cheo cha maana *DC* hakuna, Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya hakuna nchi nzima anayetoka Kongwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewaambia watu wa Kongwa hatubaguliwi kwa sababu ya anwani yetu tunatoka Kongwa, ni kwa sababu hatukusoma. Lakini sasa kwa mipango ambayo tumeiweka na juhudi tunazofanya nina hakika katika miaka sita, saba, kumi mwisho tuko katika maeneo yote kama wenzetu wanavyoshiriki katika ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza tena Mheshimiwa Waziri na ninaomba kusema naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Lakini bwana nyama yupo bwana, yeye mwenyewe ni bwana nyama, kwa hiyo yupo. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii niwe mchangiaji wa pili katika jioni hii ya leo. Kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema mpaka siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitume rambirambi zangu kwa familia ya Mzee Chifupa, kwa kuondokewa na binti yake mpendwa, Marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa. Sisi tulimpenda sana lakini Mwenyezi Mungu alimpenda zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa kwa kazi nzuri anayofanya na pia ameonyesha moyo wa uzalendo wa hali ya juu kwa nchi yake. Moyo huu ni mfano wa kuigwa kwa sisi sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze Makamu wa Rais kwa kazi nzuri anayofanya siku hadi siku. Napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu si tu kwa ufuatiliaji wake wa karibu wa kero mbalimbali za wananchi, bali pia alihakikisha ujenzi wa shule za sekondari zinakamilika kwa muda uliopangwa. Vile vile nichukue fursa hii kuwapongeza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, Naibu Mawaziri wake na Naibu Mawaziri wote kwa jitihada walizozifanya kwa kutembea nchi nzima kuhakikisha shule zinajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa niwashukuru ninyi Waheshimiwa Wabunge wote Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumchagua Dr. Didas Massaburi kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Nalisema hili toka sakafu ya moyo wangu. Naomba Mwenyezi Mungu awaongeze katika kazi zenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naomba nichangie machache kwa kuwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri imegusa kila pembe. Kwa hiyo, naona ametufilisi kusema kweli, ilikuwa ni jambo jema kama tungefunga mjadala. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwanza kuhusu mabweni kwa wasichana, ingawa wenzangu wameshachangia, lakini naomba nitie msisitizo kwamba mabweni kwa wasichana ni jambo la msingi sana. Mabweni haya yatachangia kuepusha vishawishi kwa watoto wetu wa kike mara waendapo shuleni na kurudi. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie suala hili kwa upana zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu kuwapa uwezo watoto. Ingefaa watoto wadogo wajengewe uwezo na hasa wajengewe uzalendo wakiwa chekechea. Tujaribu kuiga kwa wenzetu, kwa mfano, Wachina huwafunza watoto wao wakiwa chekechea jinsi ya kuelewa nchi yao na kuipenda nchi yao ili wanapomaliza

shule wawe na uelewa na kujiamini na huwa hawezi kubabaishwa na Mataifa mengine kwa kutumiwa au kwa njia moja au nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani, hivi punde Mheshimiwa Mbunge aliyekaa amechangia kuhusu suala la HakiElimu. HakiElimu sawa, kwa upande mwingine kuna mambo mazuri wanaelezea, lakini kwa asilimia kubwa mimi binafsi na hata watoto wangu, kwa kweli hawafurahishwi na kitendo cha HakiElimu. Maana yake inajenga chuki, unawajenga watoto wadogo ukiwafundisha kama kuna tabaka la mtoto wa tajiri anakula, kuna mtoto wa maskini yeye anahangaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukumbuke Serikali inajitahidi sana kuwajengea uwezo wananchi wetu ndiyo maana inahamasisha watu wajiunge na *SACCOS*. Inapanga mipango mbalimbali juu ya kuwawezesha wajasiriamali na ukiangalia yule mama, Mama Kayumba yeye ni mama mzuri tu pale, naona amependeza amepaka wanja vizuri, ana uwezo wa kufanya kazi. Lakini anashindwa kumsaidia mtoto wake.
Sasa naomba hizi taasisi kusema kweli hii nchi ni huru, imetoka mbali, kuna watu wamepigania nchi hii. Hii nchi inaangaliwa na Mataifa mengi. Kuna watu hawatuangalii kwa jicho jema. Kwa hiyo, tuiangalie kama alivyosema Mheshimiwa Job Ndugai, kama hawa Haki Elimu ni chama cha siasa, wangeenda kujiandikisha kwa Msajili wa Vyama. Tunawakaribisha wawe miongoni mwa vyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli sisi tuna dhamana ya kuwatetea wananchi wetu na ndiyo maana hatuogopi kuchangia kitu ambacho tunaona kinafaa au hakifai na hatuna maana kwamba hatutaki kukosolewa. Tuko hapa kwa ajili ya kuielekeza Serikali na pia kuikosoa. Lakini tunaomba taasisi hizi zielewe kwa kweli, hii nchi ina wenyewe. Kwa kweli hatupendi ichezewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ishirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii ili waandae vijarida ambavyo vitaweza kuwaelimisha watoto wetu wakiwa wadogo mpaka wanapohitimu waielewe nchi hii. Kwa mfano, mtoto ukimwuliza *Katavi National Park* iko eneo gani la nchi au ina idadi gani ya wanyama, hawawezi kukuelewa, kwa sababu hawajaelimishwa. Hivi juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alielezea mzunguko wa nyumbu katika Mbuga ya Serengeti. Wengi wetu tulikuwa hatuelewi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii itatusaidia pia kuwajengea uwezo watoto wetu na vile vile wanapomaliza darasa la saba wengine, ni sehemu ya ajira. Tunakaribisha watalii waje wengi nchini, lakini uelewa ni mdogo. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie suala hili kwa undani zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona sina mengi ya kuelezea, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. NURU AWADH BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kufikia hapa kwa muda huu wa sasa hivi. Pili, kwa niaba ya wananchi wa Tanga na mimi naungana na wenzangu katika kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa, tunasema Mwenyezi Mungu amweke mahali pema na Mwenyezi Mungu ajalie wazazi wake wapate moyo wa subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza napenda kuzungumzia kuhusu maadili. Kuna mwenzangu asubuhi alizungumzia kuhusu maadili ya wanafunzi. Wanafunzi zamani walikuwa wanawekwa *assembly* wanakaguliwa na wanakuwa wako *smart* kila wakati, siku za Jumatatu na Alhamisi, lakini pia napenda kuchangia kuhusu na walimu wenyewe wanaofundisha.Sasa hivi kuna baadhi ya shule utakwenda kumkuta mwalimu utafikiri labda wanakwenda kwenye *kitchen party* au anaenda wapi, jinsi alivyojipamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli sasa hivi ni sayansi na teknolojia, tunakwenda na mageuzi, lakini mageuzi hayo yanazidi mno, mwalimu anajipamba kiasi cha kumfanya mwanafunzi hamsikilizi mwalimu anachofundisha, anamwangalia mwalimu amevaa vipi. Kwa hiyo, tunaomba hilo tuliangalie ili kuweza kukuza maadili ya walimu. Utakuta kuna mwalimu ni mlevi pengine kwa mfano mwalimu wa kiume analewa anakwenda baa analewa, akirudi anapigiwa makofi na watoto, wanamwimbia kidedea kidedea na yeye mwenyewe anacheza, unaona! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwalimu yule atakapokwenda asubuhi shuleni kila atakachomwambia mwanafunzi, mwanafunzi atakuwa amemdharau. Kwa hiyo, naomba walimu turudi kama zamani, tuonyeshe kuwa tunakwenda na maadili yetu ya kiualimu. Halafu kuna suala la *tuition* kwa ajili ya wanafunzi. Kuna baadhi ya walimu kila shule wameandaa *tuition,* wanafunzi wanaingia asubuhi kabla ya kuingia darasani, halafu na baada ya masomo ya jioni wanakwenda *tuition.(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo linajitokeza *tuition* hiyo asubuhi lazima mtoto achangie shilingi 30 au shilingi 50 wengine mpaka shilingi100 asubuhi na jioni hali kadhalika. Kwa hiyo, mzazi atakapokuwa amekosa pesa ya kumpa mwanae mtoto yule hataingia kule kwenye *tuition* na matokeo yake atakuwa anaruka ruka kwa sababu anaona wenzake wanaingia, yeye hasomi anakuwa ni mtoro. Kwa hiyo, chanzo cha utoro pia unatokana na hapo. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iliangalie hili na pia iwaweze vizuri walimu ili hiyo *tuition* isiwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu sisi tumesoma wakati wetu hatukuwa tukienda *tuition.* Lakini mwalimu anatufundisha darasani tunaelewa na tunafanya

mitihani na tunafaulu bila ya *tuition.* Kwa hiyo, walimu tuwawezeshe ili waweze kukabiliana na hali hii ngumu. Ni hali ngumu ya maisha ndiyo inayofanya pia ikawa wanahangaika hangaika walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu nikirudi kwa upande wa wazazi, kuna wazazi hawajengi tabia ya kufuatilia mienendo ya watoto wao. Mzazi akishampeleka mtoto shule basi ameshamwachia mwalimu mtoto yule, akirudi shule akimwambia nimetoka shule haamini kuwa anatoka shuleni. Lakini kumbe mtoto yule hatoki shuleni. Kwa hiyo na wazazi mlioko majumbani tunaomba jamani mhakikishe mnasaidiana na walimu pia katika kuwalea watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mzazi ni mlezi wa kwanza, mwalimu ndiyo mlezi wa pili ambaye ana muda mrefu wa kushinda na mtoto wakiwa shuleni. Kwa hiyo, watoto wetu wanaharibika kutokana na wazazi wengine kutokufuatilia mienendo mizima ya watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kuna baadhi ya walimu hususan vijijini, mjini hakuna hilo, lakini baadhi ya walimu wa vijijini wanakuwa hawana wasaidizi wa kuwasaidia. Basi watoto wengine wanachukuliwa wanashinda shuleni na wale watoto wadogo wa walimu na wakati huo huo wakati mwingine anatolewa mwanafunzi darasani aende akampikie mwalimu au akamfulie.

Kwa hiyo, hii kwa kweli inarudisha nyuma maendeleo ya mtoto na wakati mwingine hivyo hivyo mtoto mwanafunzi wa kike anatumiwa na mwalimu wa kiume aende akampikie. Je, wajua matokeo ya kupika mtoto wa kike akimpikia mwalimu wa kiume matokeo yake nadhani yanaweza yakawa mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia kuhusu ubora wa majengo. Kwa kweli sisi tulisoma katika shule ambazo zilijengwa karibu miaka 50 iliyopita. Lakini shule hizo mpaka leo bado ni nzuri. Sasa hivi huu utaratibu wa MMES na MMEM wa kujenga shule imekuwa wakandarasi wanalipua lipua tu yaani hawana uchungu wa pesa za Watanzania wenzao. Wao wanalipua lipua tu majengo, unakuta shule imejengwa baada ya mwaka shule tayari imeshapata ufa, haifai kabisa kuwa shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani, hebu tujengeni shule ambazo zitawafanya hata wajukuu zetu watakaokuja kusomea, zionekane ni shule ambazo ziko madhubuti. Halafu pia hawa wakandarasi tunaomba pia wasichukuliwe sana, kuna wazazi humu wana taaluma mbalimbali, kuna mafundi mwashi, kuna seremala, kuna fundi *welding* na kadhalika. Kwa hiyo, Kamati za Shule ziwatumie wazazi wale, ziwawekee tangazo ili

washiriki katika ujenzi wa shule. Nina hakika kwa vile wana uchungu wa fedha zao watajenga shule ambazo ni nzuri na imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tulipokuwa tukisoma sisi, kulikuwa kuna *mobile clinics* kila baada ya miezi miwili au mitatu zinapita shuleni kule kwa hiyo, wasichana wale wakubwa wakubwa wale wote kunakuwa na *medical check up* wanaingizwa ndani, wanachekiwa vizuri, ana ugonjwa gani, kwa hiyo, matatizo yale ya upataji ujauzito yalipungua kwa kiasi fulani kwa sababu walikuwa watoto wanaogopa kuonekana kuwa mimi nisije nikawa ni mjamzito na ilikuwa ni aibu kuonekana ni mjamzito wenzake wakajua kuwa huyu mtu ni mjamzito. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ianzishe tena zile *mobile clinics* ili wanafunzi wawe wanachekiwa afya zao na pia itapunguza safari za wanafunzi kwenda hospitalini. Maana yake kwa kule Tanga Mjini utakuta mwanafunzi anaenda hospitali, akitoka hospitali kuna daladala maalumu zina muziki, basi atapanda mwanzo wa daladala mpaka mwisho atarudi haendi nyumbani wala haendi shuleni, anakuwa kazi yake ni kufuata hizo daladala na muziki na mpaka wakati fulani, kuna wanafunzi kwa ushahidi waliwahi kutoroka majumbani kwao akatafutwa wiki nzima haonekani kumbe yuko kwa kondakta wa daladala. Kwa hiyo, hiyo inatia uchungu kutokana na hali hiyo jinsi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Waheshimiwa Madiwani, kuna baadhi ya madiwani wanachukulia itikadi zao za kisiasa kuwanyanyasa baadhi ya walimu. Kama sisi Wabunge tukiwa hapa sote ni ndugu kwa hiyo, hakuna Mbunge wa *CUF*, CCM, CHADEMA, *TLP* wala chama chochote, sote sisi ni ndugu tunazungumza kwa pamoja. Lakini cha kushangaza, mwalimu atakapokuwa amezungumza labda na mtu wa upinzani, anaonekana na yeye vilevile ni mpinzani, kwa hiyo, anapewa adhabu ya kuhamishwa shule ya mbali ili iwe ni adhabu kwake, sasa namna ile mnamkatisha mwalimu tamaa. Mwalimu huyo utamkuta kapelekwa kwenye shule ambayo ilikuwa haijakamilika lakini ameiendeleza shule mpaka imekuwa nzuri. Sasa anahamishwa eti tu kwa sababu alikutwa kasimama na mtu wa upinzani. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya 50 inasema kwamba, kama kweli Mheshimiwa Mbunge ana uhakika wa jambo analolisema, tunaomba athibitishe ama afute kauli yake. Kwa sababu sidhani kama Serikali haiwezi ikamhamisha mtu kwa ajili tu ya kuongea na mpinzani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, hebu kaa chini. Unaweza ukathibitisha kuwa kuna mwalimu aliyehamishwa kwa sababu hiyo?

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nifute usemi ili tusilumbane. *(Makofi)*

Halafu kingine ninachotaka kuchangia hasa ni kuhusu Tanga. Sisi watu wa Tanga tuna eneo ambalo lilikuwa linaitwa kijiji cha miaka 21 ya uhuru, mjenzi wa nyumba hizo alikuwa ni Marehemu Somahia na nyumba zile zimetolewa zimekabidhiwa kwa Halmashauri ya Jiji la Tanga. Sasa ninachoomba hivi sasa hatuko kwenye mchakato wa

kisiasa wala kampeni, sisi tunachotafuta ni maendeleo ya Tanga. Sisi Tanga tuna tatizo la shule ya sekondari kwa kidato cha tano na cha sita. Nadhani watu Tanga wananisikia pamoja na Waheshimiwa Madiwani wenzangu, tushirikiane tuungane, lile eneo la kijiji cha miaka 21, tuchangishane tuweze kujenga shule ya kidato cha tano na sita. Tusishabikie siasa tukachukua ile sehemu ya eneo tukaiachia tukajenga vitu ambavyo havina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michezo ni afya na michezo ni ajira. Tunajua sasa hivi Waziri wa Elimu, imeandaa mkakati mzuri kuhusu michezo, lakini tunachoomba labda maafisa mipango miji na wengine, yale maeneo ambayo yana viwanja vya shule, yasiuzwe kwa watu binafsi wakaweza kujenga nyumba zao. Kuna watu wanaingia mpaka kwenye maeneo ya shule wanapewa wanajenga nyumba, kwa hiyo watoto wanakuwa hawana sehemu ambayo wanaweza wakafanya michezo. Kwa hiyo, zile sehemu ambazo ni viwanja vya shule vibaki kuwa viwanja vya shule kwa ajili ya wanafunzi wafanye michezo.

Kwa sababu kuwekeza kwenye michezo pia kunasaidia. Wenzetu Nigeria tumewapa akina Kanu kutokana na kuwekeza katika michezo. Kwa hiyo na sisi tujitahidi tuweze kuwekeza katika michezo kama tulivyoanza sasa hivi na jitihada za Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikweke za kuendeleza michezo mpaka tumeweza kupata Timu ya Taifa iliyo imara. *(Makofi)*

Mwisho wa yote, napenda kuipongeza timu ya simba kwa kupata ushindi, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza, naomba nianze kwa salamu za pole. Napenda nitumie nafasi hii kwa niaba ya wapiga kura wangu na mimi binafsi, kutoa pole kwa wafiwa wenzetu mbalimbali ambao wamepoteza maisha karibuni, akiwemo Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, Marehemu Stephen Kazi, ambaye alikuwa rafiki yangu kipenzi, pamoja na wengine waliopata vifo mbalimbali, kutokana na ajali za magari katika sehemu mbalimbali za nchi yetu. Mwenyezi Mungu, azipokee roho za marehemu na aziweke mahali pema peponi, *amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu za pole hizo, naomba sasa nitumie nafasi hii kutoa salamu za pongezi. Kwanza, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri sana. Hotuba hii imeandikwa kielimu, hotuba hii imeandikwa kiufundi, ni rahisi kuisoma na ni rahisi kufuatilia, ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Lakini vilevile nawapongeza Manaibu Mawaziri wako, pamoja na wataalam wako wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kazi nzuri waliyoifanya si kwa hotuba tu bali kwa mambo yote ambayo wamekuwa wakiyafanya katika Sekta ya Elimu. Kazi mnayofanya ni nzuri sana, nawapongeza sana. Lakini naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kusimamia zoezi hasa la kuongeza shule za sekondari katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasahau kabisa kwanza, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kuipa pongezi Serikali, kwa kuipatia elimu kipaumbele cha kwanza. Hii inaonesha kwamba, kweli tumeamua kubadilika, nawapongeza sana na nazidi kuomba tena mwaka unaofuata kama nilivyosoma katika michango yangu ya nyuma, elimu iendelee kupewa kipaumbele angalau kwa mwaka mmoja zaidi. Baada ya salamu hizo, sasa naomba kusema machache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shule zetu zinahitaji walimu. Naishukuru sana sana Wizara kwa kuliona hilo na walimu kwenda kuwapeleka mahali inakuwa ni kukaa wanahitaji nyumba. Naipongeza sana Wizara kwa kuona kwamba sasa imelivalia njuga suala la nyumba za walimu.

Mimi naamini kwamba, wananchi wataiunga mkono Serikali yetu kuhakikisha kwamba nyumba za walimu zimepatikana, kazi ambayo wananchi wameshaianza ni nzuri sana nawapongeza sana kwa kazi nzuri. Lakini vilevile inafaa kuwakumbuka Waheshimiwa Madiwani nao wamesimamia kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya nyumba mimi napenda kuishauri Wizara, ili mradi imefanikisha katika Mradi wa MMEM inaelekea kufanikisha katika Mradi wa MMES, kwa sasa imeanza kuboresha shule hizi, naomba sana sana ianze kufikiria juu ya kupeleka umeme katika shule hizi. Maana yake ni nini? Shule zetu hizi zitakuwa na maana zaidi kama zitatoa wataalam wazuri sana, najua wataalam ni pamoja na wataalam wa kompyuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kupeleka kompyuta mahali ambapo hakuna umeme. Inawezekana sana kwa kweli ni kazi nzito sana, fedha zitakazo hitajika ni nyingi sana, lakini naamini kwamba kwa wataalam walioko Wizara ya Elimu na walivyobobea katika kuuza miradi mbalimbali, inawezekana kabisa fedha hiyo ikapatikana, angalau tu katika shule ambazo zitakuwa karibu na *Greed* ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nielekee kwenye jambo moja, naomba Serikali iwakubalie walimu ombi lao, wanahitaji iwe bayana hasa anayeshughulikia na ajira yao ni nani? Inawezekana kabisa kwamba muda ulikuwa bado haujafika, lakini sasa hivi muda ni muafaka kabisa. Shule za sekondari walimu wake walikuwa wanashughulikiwa moja kwa moja na Katibu Mku, vipindi vya nyuma shule za sekondari zilikuwa chache, leo tuna shule zaidi ya 1,000, hebu jaribu kuzidisha 1,000 x 24, Katibu Mkuu tunampatia kazi kubwa mno.

Tunaomba sana sana Wizara pamoja na Serikali kwa ujumla, ziangalie sasa umuhimu wa kuwa na chombo kimoja kinachoshughulikia ajira na nidhamu ya mwalimu. Kwa ushauri wangu ili mradi tumeamua kupeleka madaraka kwa wananchi, Halmashauri zetu tuzipatie kazi hiyo, kila Halmashauri iweze kusimamia walimu wake. Kwa mantiki hiyo sasa ningeomba Idara ya Elimu ngazi ya Wilaya iimarishwe, kuwe na maafisa

taaluma wawili wa sekondari na wa msingi, hivyo hivyo katika ngazi ya mkoa. Mimi naamini kwamba, walimu wetu watapungukiwa kero nyingi sana ambazo zinawasumbua sana sasa hivi hasa walimu wa sekondari. Naomba sana Serikali iliangalie hilo iliwekee uzito wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yanayofuata sasa ni masuala ya ufafanuzi tu. Tunavyofahamu, shule zetu tuna viwango vya mikondo, shule moja inatakiwa kuwa na mikondo minne, kwa kila darasa. Lakini tunasikia kwamba kuna uwezekano Wizara ikafungua badala ya kuwa na mikondo minne, tunaweza kwenda kwenye mikondo sita ni jambo jema. Kama itafika basi naiomba Wizara tutangaze mapema kwa sababu kuna kata ambazo zimeanza shule ya pili, ya tatu na nne. Kama mlivyosema kwamba kila shule inaweza kuwa na mikondo minne au sita, haitakuwa lazima kwa wananchi kuchangia kujenga madarasa zaidi kuanza kujenga shule nyingine, wanaweza kuongeza kwenye shule ambazo tayari zipo. Naomba taarifa itolewe mapema, iweze kueleweka kwa nchi ili wasije wakaweka nguvu mahali ambapo hazitatakiwa baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo naomba Wizara itusaidie ni suala la *capitation grand*. Tulisema kwamba, wazazi watatoa ada ya shilingi 20,000 sehemu nyingine italipwa na Serikali. Inawezakana kunaweza kuwa na matatizo kidogo katika kupata pesa hizo, lakini ni vizuri ikaeleweka kwa sababu tatizo ambalo shule zetu inapata ni kwamba, wanaopona wanashindwa kufanya mipango kwa sababu pesa haijulikani itafika lini na itafika kiasi gani? Kwa hiyo, naomba sana hilo lingewekwa wazi tufanyaje ili shule zetu ziweze kufanya mipango yao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tayari nimeshasema, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu juu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa jioni hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, naomba nianze na pongezi. Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kazi nzuri aliyoifanya katika kujenga shule za sekondari kwa kipindi kifupi kwa nchi nzima, bila kumsahau Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri mwenye dhamana, Manaibu Waziri na wote walioshiriki katika kazi hii yenye mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza Mkuu wa Mkoa wa Singida, Ndugu Parseko Kone, kwa kazi kubwa aliyofanya ya ksimamia na kuhamasisha ujenzi wa shule za sekondari Mkoani Singida. *(Makofi)*

Mkoa wa Singida tulikotoka tulikuwa na shule za sekondari 33, kwa maana ya shule mbili zilikuwa za *mission* zikataifishwa na Serikali na moja bado ni ya *mission* mpaka hivi sasa. Shule 30 zilijengwa kwa nguvu za wananchi huko nyuma katika awamu iliyopita. Lakini kwa awamu hii ya mwaka mmoja aliyokaa, Mkuu wa Mkoa wa

Singida ameweza kujenga shule 70, hili ni jambo la kumpongeza kwa ujasiri na ushujaa alioufanya wa kuisaidia Singida katika kuboresha elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kumpongeza Mkuu wa Mkoa, vilevile ameshirikiana na *DCs,* watendaji wote na wananchi kwa ujumla na Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Singida, kwa kufanya kazi hii nzuri, wote nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi sasa naomba nitumie nafasi hii kujadili kidogo ama kushauri kidogo juu ya bajeti hii iliyo mbele yetu. Naomba nizungumzie kuhusu chombo kinachosimamia ajira kwa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu ni kati ya watumishi walioko katika nchi yetu, lakini walimu ni zaidi ya asilimia 50 watumishi wa Serikali. Cha kushangaza walimu hawa tunawatangisha tangisha kwa nini? Ukienda Menejimenti ya Utumishi wa Umma walimu wanahudumiwa, ukienda Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI walimu wanahudumiwa, ukienda Wizara ya Elimu ndio hapo tena walimu wapo, Wizara ya Fedha walimu wapo. Ninaomba sana kundi hili kubwa tuhakikishe tunasimamia haki na maslahi yao kwa kuwapa chombo kimoja, kwa nini wasiwe chini ya Wizara moja ili haki zao za msingi ziweze kutunzwa vizuri?

Walimu wana mambo mengi, wana kero nyingi, ukilinganisha na kazi nzito waliyokuwa nayo. Lakini unakuta mwalimu anakuwa na tatizo, faili linatembea Wizara nne, mwalimu hata kama alikuwa na nia ya kushughulikia tatizo lake anaweza akaishia njiani. Ninaomba sana, madhali Serikali ilishalisikia hili, hebu tufike mahali tusikie kilio cha walimu tuwape chombo kimoja kitakachosimamia ajira zao, haki zao na maslahi yao. Kufanya hivyo tutakuwa tumewasaidia sana walimu kuboresha ufanisi wa kazi zao na kupata haki zao na maslahi yao kwa njia ya mkato, kuliko mlolongo huu mrefu ambao wanaupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba nizungumzie juu ya uhakiki wa madeni ya walimu. Toka Januari, 2007, Serikali ilikuwa na inahakiki madeni ya watumishi pamoja na walimu. Lakini sielewi mpaka sasa hivi Serikali imeshahakiki madeni kiasi gani, jumla ya shilingi ngapi walimu wanadai na ni walimu wangapi basi wameshalipwa madeni yao? Ni vizuri sana Waziri atakapokuwa anatoa majumuisho ya bajeti yake, akawaeleza walimu kupitia Bunge hili wakasikia kwamba, uhakiki wa madeni ni shilingi ngapi na wangapi mpaka sasa hivi wamelipwa na wamebakia wangapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ndani ya madeni hayo hayo, kwa nini bado malimbikizo yanakuwepo? Ifike mahali basi haya sasa hivi mwalimu anapokuwa na madai yake alipwe papo hapo. Kama tutaendelea kulipa madeni huku tunalimbikiza madeni, hatutamaliza madeni, itakuwa tumewatendea haki sana walimu endapo tutamaliza madeni. Ni bora tukaendelea kuomba madeni ya nyuma lakini sasa hivi basi madeni yaende na wakati, mtu afanye kazi yake alipwe ujira wake mbona sisi humu ndani hatukopeshwi? Ni Mbunge gani anakopeshwa hapa, sisi tunafanya kazi papo hapo na walimu wafanyiwe hivyo, tutakuwa tumewatia moyo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nizungumzie suala la kupandishwa vyeo walimu. Mwaka 2006, mfumo wa kutathmini madeni ya walimu ulisimamishwa baada ya kuona kwamba, mfumo wa *OPRAS* ulikuwa na mapungufu kidogo, lakini mpaka sasa hivi hatujui kama baada ya kuhakiki huu mfumo walimu wameshaanza kupanda madaraja. Kwa sababu mfumo huu ulionekana una mapungufu, walimu wengi ilionekana wanacheleweshwa kupanda madaraja yao.

Mwalimu anakaa katika daraja moja mpaka miaka kumi, wako walimu wa namna hii. Nina hakika kwa kuwa Serikali ilishaliona hili, ndani ya uhakiki wao na kuangalia mfumo huu wa *OPRAS*, sasa walimu watakuwa wameaanza kupanda madaraja. Sasa ninaamini Mheshimiwa Waziri kwa kuwa ni mwalimu mwenzetu, atatuambia basi baada ya uhakiki wa mfumo huu ni walimu kiasi gani wameanza kupanda madaraja na walimu wangapi bado hawajapandishwa madaraja.

Walimu ni tofauti na watumishi wengine jamani tusijilinganishe, kila watu wana ugumu na kazi yao, hao wenzetu inatakiwa tuwachukue jinsi kazi yao ama uzito wa kazi yao ulivyo. Tukiwapa haki zao kwa kuwapandisha madaraja, wakati muafaka tutakuwa tumewatia moyo sana walimu na watafanya kazi yao vizuri mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulizungumzia hilo, naomba nizungumzie jambo ambalo wenzangu wameshalizungumza lakini ninatakiwa nirudie kwa sababu lina umuhimu na uzito wake, ni suala la hosteli. Wanafunzi tunaowapeleka shule sasa ni wengi wa kutosha na inapendeza sana, lakini wengi wao elimu wanayoipata hailingani na stahili hii ya elimu hiyo. Kwa sababu unakuta mwanafunzi anakaa maili tano kutoka shule ya sekondari ilipo, ama kumi au mwanafunzi anapanga kwa mtu tu, huduma anayopata pale ni shida na si hivyo tu watoto wa kike wana matatizo jamani, ni tofauti na watoto wa kiume.

Vishawishi ni vingi, ndio maana watoto wa kike wengi hawamalizi shule kwa sababu ya shule hizi za kutwa. Ninaomba sana sana, pamoja na Serikali kuona umuhimu wa kujenga hosteli, naomba sana kipaumbele wapewe wasichana wa kike katika hosteli ambazo zitakuwa zinamalizika halafu baadaye ndio tuwafikirie watoto wa kiume. Tukifanya hivyo tutakuwa tumewasaidia wanafunzi wetu kumaliza elimu na kupata elimu inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu Mfuko wa *Capitation.* Naipongeza sana Serikali kwa kweli inafanya kazi nzuri, inawajali wanafunzi mambo mengi ya msingi yanapelekwa. Kwa mfano, kila mwanafunzi nchini anapewa shilingi 10,000 kwa ajili ya mahitaji yake ya lazima kupitia Mfuko huu wa *Capitation* lakini si shule zote ambazo zinatoa kiwango hiki. Mimi niko kwenye Kamati ya Mahesabu ya Serikali za Mitaa, nina ushahidi wa kutosha, ziko shule zinatoa shilingi 2,000 na ziko shule zinatoa shilingi 5,000 badala ya shilingi 10,000. Kuna sababu gani za msingi wanafunzi wasipate stahili yao waliyopangiwa na Serikali yao? Je, mgao huu wa *capitation* kwa ajili ya watoto hawa ni tofauti kati ya shule na shule? Kama sio tofauti, ninaomba wanafunzi wote wapate kiwango kinacholingana. Tukifanya hivyo tutakuwa

tumewasaidia hawa watoto kupata mahitaji yao muhimu ili waweze kuyamudu masomo yao bila matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu matatizo yanayozikabili shule zetu za sekondari zilizojengwa vijijini. Tunashukuru sana sekondari mpaka vijijini zipo, lakini sekondari hizi zina matatizo mengi, tatizo mojawapo ni uhaba wa walimu. Walimu wengi wanakataa kwenda kufundisha vijijini, kwa sababu shule hizi hazina huduma muhimu. Shule ya sekondari nzuri ya kisasa imejengwa haina nyumba za walimu, hakuna maji safi na salama, hakuna barabara, hakuna hata maduka ya mahitaji muhimu, hakuna zahanati; hivi unafikiria mwalimu ukimpeleka huko atakaa, hakai, ataenda kuchungulia tu atageuka. Kwa sababu mahitaji muhimu hatayapata na sasa hivi mambo kisasa watu wanahitaji huduma muhimu.

Ninaiomba Serikali kwa sababu ya mapungufu haya, tutazame uwezekano wa kuwasaidia walimu wanaopangiwa shule za vijijini, namna ya kuwapa motisha ili waweze kuishi kwenye mazingira haya. Bila kutoa kifuta jasho ama posho ya aina yoyote kwa walimu hawa, shule za vijijini hazitapata walimu sambamba na shule za mijini. Kwa maana hiyo basi, taaluma zitakazokuwa zinatolewa huko hazitalingana na taaluma za shule nyingine.

Ninaomba sana Serikali iangalie kwa kina ili walimu hawa waweze kukubali kwenda kufundisha vijijini, kwa sababu kwa kweli hata sisi tufikirie kama mtoto anapangiwa kufundisha kijinini mahali ambapo zahanati hakuna, barabara hakuna, maduka hakuna; hivi mzazi utaridhika kweli kumwacha mwanao! Homa ndogo kwake ni tatizo, matokeo yake utamkuta mwalimu anaanza na lifti za baiskeli, mwishowe lifti za pikipiki, mwishowe ndoa. Tutawafanya walimu wafunge ndoa ambazo hawakuzitarajia, kwa sababu ya huduma ndogo ndogo. Ninawaomba walimu tuwafikirie tuwape motisha ambazo zitawasaidia hata kama wana shida muhimu, hata taxi mjini iwafuate, sasa hivi mtandao mpaka vijijini upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumzia hilo kwa kina, nina hakika kabisa Serikali imenisikia, naomba nizungumzie juu ya mtihani wa darasa la saba. Kuna mwaka hapa wanafunzi wa darasa la saba hawakupata vyeti nchi nzima mpaka leo. Kwenye ziara zetu vijijini swali hili kila leo tunaulizwa, sasa hivi mpaka ukigombea udiwani unatakiwa ujaze umemaliza elimu gani, wanafunzi wetu hawana vyeti. Hebu Serikali ikumbuke mwaka huu angalau viandikwe vyeti watu wetu wapate vyeti ni kumbukumbu zao zitawasaidia kwa namna moja ama nyingine. Kwa sababu kama kweli mtu alihitimu elimu ya msingi lakini hana cheti, tutakuwa hatumtendei haki kabisa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naomba nizungumzie kuhusu walimu wa masomo ya sayansi, ni kweli tuna matatizo ya maabara na kero hii ni kubwa nchi nzima. Naishukuru Serikali angalau imepeleka maabara mbili kwa kila shule kwa kila mkoa, lakini bado haitoshi. Hebu tujaribu kuangalia tugawe shule hizi katika mkoa kama shule ni mia moja basi tuchukue angalau shule kumi tuzipe maabara, tuzifanye maalum kwa sababu utaratibu huu tulikuwa nao toka huko tulikotoka, ili angalau tupate maabara, hata

shule nyingine za jirani ziende zikajifunzie pale. Lakini kuwa na maabara shule moja tu, bado hapa hatujasaidia, matokeo yake tutapata wataalam wa *arts* pekee yake, hatutapata wataalam wa masomo ya sanyansi, wameshasema wenzangu.

Ninaomba Serikali iangalie kwa kina kabisa, tugawe hizi shule kwa makundi, masomo ya sanaa, masomo ya mchepuo wa *arts* ili tuone namna ya kuweza kupeleka maabara. Kwa sababu naelewa uchumi wa nchi ulivyo mgumu kwa kweli tukitaka kufukuzia sekondari zote hatutaweza na sekondari ni nyingi mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamesema walimu wa masomo ya sayansi ni wachache. Sasa wale wachache waliopo tuwapeleke kwenye Vyuo vya Ualimu ili waweze kupeleka elimu hiyo kwa wanachuo wetu ili tupate walimu wa fani ya sayansi. Kama Tanzania hawatoshi, basi tuazime kutoka nchi za wenzetu. Kwa kuwa nia ni njema, itakuwa ni bora zaidi tupate wataalam hawa ili katika wanafunzi wetu wanaosoma tusiwe na wataalam wa fani moja, watakosa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naungana na wenzangu waliotangulia kuchangia, kutoa salamu zangu za rambirambi kwa kifo cha Mheshimiwa Amina Chifupa. Mungu amlaze mahali pema peponi, *amen*.

Pigo kubwa zaidi tumepata sisi kwenye Kamati ya Maendeleoya Jamii kwa sababu alikuwa ni mwanakamati mwenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile natoa salamu zangu za rambirambi kwa wale wote waliopoteza roho zao kwa ajali mbalimbali. Nao pia Mungu awalaze mahali pema peponi na walioumia wapate nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa hotuba yake nzuri kabisa, yenye ufanisi, yenye kufahamika na yenye kuvutia kabisa. Nampongeza yeye pamoja na Manaibu Waziri wake, pamoja na watendaji wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa iliyofanya katika Awamu ya Nne. Haya matunda ni makubwa wala hayatasahaulika. Matunda hayo ni kuweza kujenga shule za sekondari karibu katika kata zote nchini. Kwa hiyo, naipongeza sana Wizara chini ya usimamizi wa Waziri Mkuu. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitishwa na kushangazwa sana na wale wenzetu wanaosema huu ujenzi wa shule kwamba wananchi wanadhalilishwa. Kwa kweli ni jambo la kushangaza, badala ya kufurahia maendeleo wao wanataka kuwarudisha nyuma wananchi. Maendeleo ya nchi huletwa na wananchi, kwa hiyo nawahurumia na mazungumzo yao hayo ya kurudisha nyuma maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kama tulivyofanikiwa kujenga shule za sekondari pamoja na hayo mapungufu ya vifaa na mambo mbalimbali, *inshallah* Mungu atajalia na hivyo vifaa vitapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili wanasema nia njema tabibu.

**NAIBU SPIKA:** Wabunge wanasema urudie, Waswahili wanasemaje?

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** "Nia njema tabibu." *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** *Okay*.

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, wenzangu waliotangulia wamenifilisi kwa upande wa suala la elimu maalum au wanafunzi wenye ulemavu. Nashukuru Mheshimiwa Waziri amezitaja baadhi ya shule ambazo ni maalum kwa watu wenye ulemavu kwamba zitaboreshwa na zitazidi kuimarishwa na kupatiwa huduma muhimu. Tunashukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hivyo bado mahitaji yanahitajika kwa wanafunzi wenye ulemavu na ukizingatia kuna kila aina ya ulemavu. Baadhi ya mahitaji tunalingana lakini baadhi ya mahitaji tunatofautiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote na hizo shule zilizojengwa, mwenzangu alizungumza asubuhi kwamba, *facilities* ziwepo. Tuanze kufanya marekebisho kama kuna wanafunzi wenye ulemavu wa viungo, wapatiwe *wheel-chairs* au *tricycles.* Kwa hiyo, zile shule ziwe na njia ili waweze kuingia mpaka madarasani.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo mengine kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa viungo ni vyoo. Inabidi milango ya vyoo iwe mipana ili waweze kuingia na visaidizi vyao mpaka ndani.

Hakuna lisilowezekana, nina imani vitarekebishwa tu ili wanafunzi wenye ulemavu sio lazima wapelekwe kwenye shule maalum waweze nao kufaidi matunda ya Awamu ya Nne kwenye hizo hizo shule zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu baadhi ya Walimu wenye ulemavu hawapati fursa na haki sawa kama Walimu wengine. Kwa mfano, kunatokea semina, kozi maalum za kuwaendeleza wao wanakuwa hawafikiriwi. Kwa hiyo, wamenituma na wao wanaomba wafikiriwe kwani nao wana ujuzi na wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna hili suala la *TEHAMA*, ambalo Mheshimiwa Waziri asubuhi alilizungumzia. Walimu wenye ulemavu wanaomba na wao wapatiwe mafunzo haya ya *TEHAMA*. Vilevile kumeanzishwa mafunzo ya lugha ya Kifaransa, wanaomba na wao wapatiwe mafunzo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu elimu mjumuisho. Mwenzangu alizungumza asubuhi na mimi nazidi kutilia mkazo. Hii elimu mjumuisho ningeomba kama kuna uwezekano iwe inatolewa kama dozi kwenye Vyuo vyetu vya Ualimu ili Walimu wote wanaopitia kwenye vyuo hivyo, wapate hii dozi ya elimu mjumuisho ili wakikutana na wanafunzi wanaohitaji elimu hiyo isiwe tena wanapata shida, wawe tayari wanayo dozi au mafunzo. Naomba mtaala wa Wizara ya Elimu, uingize hili somo la elimu mjumuisho katika Vyuo vyetu vya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu Maafisa Elimu. Mheshimiwa Bhujiku Sakila hapa alisema kuwe na Maafisa Elimu wa Wilaya na Mikoa wawili wa shule za sekondari na shule za msingi. Lakini mimi naomba wawepo na Maafisa Elimu wa Elimu Maalum katika Wilaya na Mkoa ili kupunguza huo msongamano na huo usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu mishahara. Wengi wamezungumzia mishahara, posho na mazingira. Lakini ukija pia kwa Walimu wanaofundisha wanafunzi wenye ulemavu yaani elimu maalum, kwa kweli wao wana mzigo mara mbili. Halafu yule mwanafunzi kwa mujibu wa ulemavu, kuna kazi kweli namna ya kumwelekeza mpaka akaweza kumudu kile kinachofundishwa. Kwa hiyo, hawa nao wafikiriwe maana wana kazi mara mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la vifaa. Naomba Wizara ijitahidi kupata vifaa kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum au wanafunzi wenye ulemavu. Pamoja na kwamba tunajua kweli vifaa ni ghali lakini hata hivyo wajitahidi angalau viweze kupatikana kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho, ni kuhusu hivi vyuo vya *VETA*. Hivi vyuo vya *VETA* tungeomba navyo pia wawepo wataalam ambao wanaelewa kuhusu wanafunzi wenye mahitaji maalum ili iwe rahisi na wao waweze kushiriki au kuingia katika vyuo vyetu vya *VETA*. Hilo ni ombi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa kabla sijasahau, naipongeza hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu na naiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia na kumi juu naongeza, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, kwa hotuba yako nzuri sana na yenye ufasaha mwingi. *(Makofi)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ambayo nimeitafuta kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kuanza kwa kuupongeza Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi tukianza na Mheshimiwa Waziri; Manaibu wake wawili; Katibu Mkuu na Maafisa wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niungane na wote ambao wametoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Amina Chifupa na mumewe ndugu yetu Mpakanjia, ambaye inasemekana hivi sasa anaumwa sana. Basi tunamwombea Mwenyezi Mungu, ampe nguvu na ikimpendeza aweze kupona.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda kuipongeza Wizara hii kwa kufanya kazi nyingi sana za kuhamasisha ujenzi wa shule za msingi na sekondari katika Taifa letu. Mimi kwa sababu ni Mbunge kutoka Wilaya ya Mufindi, napenda kuupongeza Uongozi wa Wilaya pamoja na wananchi wote wa Mufindi kwa namna walivyoshirikiana wao kwa wao wakisaidiwa misaada na fedha mbalimbali kutoka Serikalini, kujenga shule nyingi za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi ya Wilaya, napenda kumpongeza sana Mkuu wetu wa Wilaya, Mheshimiwa Katalu na *DED* wetu, Ndugu Hida na Viongozi wa Chama cha Mapinduzi katika ngazi zote. Kwa sababu viongozi wa Chama ndio wahamasishaji wakubwa wanaohamasisha siasa. Kwa hiyo, napenda wote hawa niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na MMEM kwa sababu huu ni utaratibu ambao ulileta mapinduzi ya elimu katika nchi yetu ni kama vile ilivyokuwa *UPE. UPE* ilifungua elimu katika Taifa hili. Mimi sikufaidika na *UPE* kwa sababu nilishapanda juu kidogo lakini wadogo zangu wote walionifuata walisomeshwa chini ya utaratibu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sina sababu kwa kweli ya kutompongeza Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Wengi wetu hapa ni matunda ya Baba wa Taifa. Nina hakika bila Baba wa Taifa inawezekana labda robo tatu tuliopo hapa tusingekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, MMEM inafanya vizuri sana na napenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iendelee kuitetea na sisi Wabunge humu ndani tuendelee kuitatea ili iendelee kufanya kazi nzuri kama inavyofanya hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilianza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake wawili na watendaji wao wote. Sasa nije kwenye Mpango wa Elimu ya Sekondari. Kwa kweli huu mpango unakwenda sambamba na Mpango wa MMEM. Tumejenga shule nyingi sana. Mimi Wilayani kwangu wakati naingia Bungeni tulikuwa na shule moja lakini sasa hivi ziko shule nyingi hata idadi yake siijui, maana ni nyingi sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunalo tatizo. Tatizo letu ni kwamba, tunajenga shule nyingi kutoka kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne lakini kidato cha tano mpaka sita kasi ni ndogo sana, yaani vijana wanaomaliza kidato cha nne kwenda kidato cha tano wanakuwa wachache.

Nadhani hii ni changamoto kubwa sana kwa Wizara hii. Tunaiomba Wizara ifungue milango ya kuingia kidato cha tano ili vijana wamalize kidato cha sita wawe na uwezo wa kwenda Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia kuingia katika Shirikisho au katika Jumuiya ya Afrika Mashiriki, tunahitaji kuwa na wasomi wengi. Wasomi wanapatikana Vyuo Vikuu hawapatikani kidato cha sita au cha nne. Naiomba sana Serikali ijitahidi kwa kadri iwezavyo iongeze nafasi za kidato cha tano ili tuwe na wahitimu wengi wa kidato cha sita hatimaye tuwe na maelfu ya vijana wanasoma Chuo Kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kule Mufindi tumeleta maombi mara kwa mara Wizarani. Tunazo shule zetu nne ambazo tungependa tupewe kibali cha kuwa na kidato cha tano na sita. Shule hizo ni Igowele Shule ya Sekondari, Mgololo Shule ya Sekondari, Mdabulo Shule ya Sekondari, Itengule Shule ya Sekondari. Kwa maneno haya nadhani imeshaandikwa hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua uzuri wa jambo hili ni nini? Vijana wanapokuwa na hakika kwamba akifaulu kidato cha nne nafasi ya kidato cha tano inakuwa rahisi watasoma kwa bidii. Inakuwa tunawapa moyo kwamba nafasi zipo. Akifaulu ana hakika atakwenda kidato cha tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni kuhusu Walimu. Ni kweli kwamba tunayo shida kubwa sana ya Walimu kwanza wapo wachache. Lakini pamoja na kwamba wapo wachache nadhani tunashindwa kuwahudumia vizuri, nyumba hawana na hasa Walimu wa shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua vijiji vyetu vilivyo. Ziko shule nyingine ziko mbali sana na miji. Ziko sehemu nyingine nyumba ya bati ni ya shule na labda nyumba mbili za Walimu zilizojengwa pale. Kwa hiyo, napenda Wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ijaribu sana kushughulikia ujenzi wa nyumba za Walimu. Mwalimu akiwa na nyumba nzuri na mishahara yao tukiiboresha, watu wataipenda kazi ya Ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mwalimu pamoja na kwamba ni Mhandisi. Niliacha kazi ya Uhandisi nikakubali kwenda kushika chaki miaka minane. Kwa hiyo, nafahamu utamu wa Walimu na pia nazijua adha za Walimu mpaka nikapewa Ukuu wa Shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli katika hili naiomba sana Wizara ya Elimu iwaonee huruma Walimu. Tena kwa bahati nzuri Waziri ni mama na akina mama ni watu wenye huruma, naye ni Mwalimu pia. Sina haja ya kuzungumzia sana matatizo ya

Walimu kwa sababu anayafahamu na aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Walimu kwa hiyo anayafahamu sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Alikuwa Rais.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** *Okay*, alikuwa Rais wa Chama cha Walimu. Kwa hiyo, matatizo ya Walimu wake anayajua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua mimi nimekulia kijiji kimoja kinaitwa Ng'enza, kiko Iringa Vijijini. Juzi juzi niliitembelea ile shule. Sikusoma pale lakini nilikulia pale, nikatembelea shule ile ya msingi ya Ng'enza. Nikakutana na kijana mmoja Mwalimu alikuwa amenizidi madarasa kwa hiyo *he is senior to me,* nyumba yake anayoishi imeezekwa kwa nyasi, nilisikitika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa nizungumzie ni Baraza la Mitihani. Baraza la Mitihani kwa kweli wanajitahidi kufanya kazi yao vizuri sana lakini nao wana matatizo ya fedha. Wana jengo moja pale zuri sana, wamejenga jengo kubwa la kifahari lakini halijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika kupitia kwako na Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa tena ananiangalia, naomba toeni pesa za kutosha ili mkamilishe jengo lile. Ni jengo zuri. Jengo lile inasemekana litakuwa la kusahihishia mitihani. Walimu watakuwa wanakaa pale wanasahisha mitihani yao vizuri. Naamini hata huu wizi wizi au kuvujavuja mitihani kutakwisha maana Walimu wanakaa mahali pazuri wanasahisha mitihani kwa utaratibu, wanakaa kwenye hewa nzuri pale, iko juu kabisa pale, hewa ya baharini yote unapata kwa usafi. Kwa hiyo, naombeni sana mmalizie jengo lile ni zuri mno, liko Mbezi kule Mlimani kabisa, safi. Naomba sana sana mlimalizie jengo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka michache iliyopita tulikuwa tunasikia mara nyingi mitihani inavuja, napenda kulipongeza Baraza la Mitihani kwamba mwaka 2006 hatukusikia kabisa mtihani uliovuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndio maana ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Hatutaki mitihani iwe inavuja. Tunataka watoto wetu wanaposhinda wawe wamefaulu mtihani kwa sababu wana akili, wamefundishwa vizuri, elimu imejaa kichwani, ndio tunachotaka, sio watu wanaibaiba mitihani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua kuiba mtihani ni kitu kibaya sana. Kuna shule moja ya msingi kule Manyoni walifaulu wanafunzi 83 wote wakaenda sekondari. Kufika darasa la 10 waliokwenda *Form III* ni watatu tu. Hii maana yake nini? Huu ni mfano hai. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia napenda nilipongeze Baraza la Mitihani kwa Mitihani yao ya Kidato cha Sita mwaka 2006. Mitihani ile ilikuwa mizuri sana na haikuvuja. Pamoja na kwamba wanasema ilikuwa migumu, tumeshindwa ile ni changamoto katika Wizara ya Elimu, tungeni mitihani kama ile, endeleeni kutunga

mitihani kama ile kijana anayefaulu tujiridhishe kweli amefaulu mitihani inayofikia viwango. Hii ndio mitihani, sio unatunga mtihani asilimia 97 *pass,* aaaah, ni mtihani huo kweli tena wa Kidato cha Sita? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa wito wa dhati kabisa kwa Wizara ya Elimu, tungeni mitihani ambayo vijana watajipima kuonesha uwezo wao, iwe ni mitihani ya kutosheleza elimu sio mtihani wa kupitapita tu, hapana. Tunataka kijana akitoka pale akienda *Oxford University,* wanasema kweli huyu kidato cha sita kutoka nchi ya Tanzania, kijana ameiva, mitihani yao iwe inaivisha vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo hapa lakini kwa sababu nimebakiwa na dakika moja, naomba kwa ufupi kabisa niseme naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia zote kabisa. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa hotuba nzuri.

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia nikiwa nimesimama. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Afadhali. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Waziri pamoja na Manaibu Mawaziri, kwa utayarishaji na uwasilishaji wa bajeti hii kwa ufanisi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nataka kutamka moja kwa moja kwamba, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, nataka kutoa hongera kubwa kwa kazi kubwa ambayo imefanyika katika ujenzi wa shule mbalimbali za msingi pamoja na sekondari. Kazi kubwa iliyofanyika katika kipindi cha miaka hii miwili, haihitaji mtu kuelezwa kwamba ilikuwa ni nzuri. Ni nzuri na hatuna budi kutoa pongezi kwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa aliyoifanya lakini na watu wengine mbalimbali wakiwepo Mawazirina Naibu Mawaziri waliotembelea sehemu mbalimbali katika kuhamasisha ujenzi wa shule hizi za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kutoa pongezi kubwa sana kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, kwa kazi kubwa ya kuweza kuzitembelea na kuhakikisha kwamba shule za sekondari zinakamilika. Mkuu wa Wilaya, Bwana Gama vilevile amefanya kazi kubwa na Halmashauri ya Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Mbeya Vijijini, kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya kuweza kushirikiana nasi katika ujenzi wa shule za sekondari hizo. Kazi hiyo walioyoifanya inaonekana na kila mtu ameridhika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotolewa kwa ajili ya bajeti ya elimu kwa mwaka huu ni ya kutosha na natumaini inadhihirisha kwamba elimu inapewa umuhimu unaostahili. Utafiti uliofanyika duniani kote unaonesha kabisa kwamba elimu ndio msingi wa maendeleo. Natumaini hata sisi Watanzania tumeamua kabisa kwamba elimu ndio urithi pekee ambao tunaweza kuwapa watoto wetu na kazi kubwa ambayo Serikali imeweza kufanya ni kuhakikisha kwamba vijana wetu wanaweza kupata elimu hii muhimu na hivyo kuwekeza katika elimu imekuwa ni suala la kipaumbele. Asilimia 18.2 katika bajeti ni kiasi kikubwa sana katika utekelezaji wa suala la elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyo mbele yetu ni jinsi ambavyo fedha hizo zinaweza kutumika vizuri na kwa kuwajibika ili kuhakikisha kwamba tunaboresha mazingira mazuri ya shule ambazo zimejengwa.

Sasa hivi tunazungumzia kuhusu mazingira mazuri kwa sababu shule zilijengwa, kama zisingekuwa zimejengwa tusingekuwa tunazungumzia kuhusu kuboresha majengo hayo. Kwa hiyo, pongezi ya kwanza ni katika kujenga na sasa tupo katika hatua ya pili ya kuweza kuziboresha na nina uhakika kazi hii itafanyika kwa kuongeza madarasa zaidi ili kuweza kukidhi ongezeko la wanafunzi watakaokuwa wanaongezeka.

Lakini cha msingi vilevile ni kuweza kuhakikisha kwamba, tunakuwa na nyumba za walimu za kutosha, tunakuwa na maabara, tunajua kwamba zitajengwa lakini tunahitaji kufanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa zaidi na kwamba fedha zitakazotumika zitumike bila ubadhirifu wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha nyingine zimetengwa kwa ajili ya Maktaba lakini Maktaba zenyewe ni chache lakini angalau juhudi zimeanza kuonekana kwamba angalau mkazo wa kujenga Maktaba katika shule zetu umeanza kujitokeza. Pamoja na Maktaba hizo tunahitaji kuwa na vitabu vya kiada na ziada. Elimu ni kujenga uwezo wa mtoto kujisomea, bila kuwa na vitabu vya kutosha katika shule zetu inawezekana kwamba elimu ambayo itakuwa inapatikana itakuwa ni duni kidogo. Kwa hiyo, kuwe na fedha za kutosha kwa ajili ya kuweza kununua vitabu vya Kiada na Ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mabweni natumaini limezungumzwa na wengi na mimi naliunga mkono lakini cha mwisho kabisa ni kuhakikisha kwamba katika shule zetu hasa za vijijini zinakuwa na umeme. Hata kama ikiwezekana tuweke juhudi za kuwa na umeme wa kutumia jua yaani umeme wa jua kwa sababu masomo ya jioni ukitaka kusoma ni lazima kuwe na mwanga wa kutosha. Vijana wetu hawapati nafasi ya kujisomea nyakati za jioni kwa sababu shule zetu hazina umeme wa kutosha na kuweza kuhakikisha kwamba wanapata nafasi ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zipo lakini wasiwasi wangu ni kwamba ujenzi unakuwa mgumu na wakati mwingine huchelewa kuanza kwa takriban miezi miwili kwa sababu kipindi cha kufanya majadiliano ya kupitisha bajeti ni kipindi ambacho kinakuwa ni mwanzo wa mwaka wa fedha. Kipindi cha mwaka wa fedha kinakwenda sambamba na kujadiliana bajeti kwa hiyo, fedha za Serikali zinaanza kutumika miezi miwili baada ya

kumaliza bajeti, maana yake ni kwamba tumechelewa miezi miwili katika utekelezaji wa bajeti hiyo.

Kwa hiyo, nashauri kama ikiwezekana mfumo wa kujadili bajeti urudi nyuma, yaani uwe unaanza mwezi wa nne, wa tano mpaka wa sita na tukimaliza kufanya majadiliano hayo na kuipitisha bajeti, mwaka wa fedha wa Serikali unapoanza, fedha zinaweza kupatikana kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi mbalimbali wa mipango tuliyojiwekea. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunaanza ujenzi wakati wa kipindi kizuri, ujenzi wa miradi yoyote ile unawezekana kufanyika vizuri zaidi kuanzia mwezi wa saba mpaka mwezi wa kumi na moja wakati mvua hazipo. Lakini mara nyingi ujenzi unachelewa kwa hiyo utaona hata tunapoanza kujenga shule zinaingiliana na matatizo ya mvua na hatma yake ni kwamba shule zetu huchelea kuanza hazianzi mwezi Januari au Februari wakati msimu wa shule unapoanza, huwa zinachelewa mpaka mwezi wa tatu au wa nne.

Kwa ushauri wangu ingekuwa ni kujaribu kuangalia kama ikiwezekana kubadilisha mfumo wa kuweza kujadili bajeti ukafanyika mwezi wa nne, wa tano na wa sita na mwaka wa fedha unapoanza bajeti zinakuwa zimeshapitishwa na Serikali iko tayari katika kutekeleza mipango ambayo imewekwa mbele yetu. Kwa kufanya hivyo tutakuwa na uhakika wa wanafunzi wetu kuanza masomo katika kipindi ambacho kinafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi ambayo inafanyika na Wizara vilevile napenda kutoa pongezi kubwa kwamba, mishahara ya walimu sasa imeanza kufika mapema katika maeneo yao. Lakini kwa bahati mbaya mishahara hiyo kwa wakati huo inapitia katika benki moja tu ya *NMB,* sasa ukichukua benki moja katika Wilaya kwa walimu wote, inakuwa ni kazi kubwa kidogo. Kwa hiyo, kunakuwa na msongamano mkubwa sana kwa siku moja au mbili walimu wakiwa wanangoja mishahara.

Kwa hiyo, natumaini kuna umuhimu wa kuboresha namna ya kutoa mishahara hiyo lakini kwa kuanzia natoa pongezi angalau fedha hizo zinafika katika maeneo yao mapema. Tatizo tulilonalo ni kwamba walimu wanaotoka vijijini wanasafiri siku moja wanakwenda wanapanga mstari siku nzima wakingojea mishahara yao na siku ya pili wanarudi. Kwa hiyo, kunakuwa na siku tatu zinazopotea bila kutoa mafunzo yoyote kwa wanafunzi kwa sababu ya kuchukua mishahara.

Ushauri wangu ni kwamba, labda umefika muda muafaka wa kuanza kufanya utafiti jinsi ambavyo tunaweza kuzitumia *SACCOS* zilizopo kwenye ngazi ya Kata. Siyo kwamba *SACCOS* zote zimeimarika, lakini nina imani kwamba kuna *SACCOS* nyingine ambazo zimeimarika zinafanya vizuri, mishahara ingeweza kuwa inakwenda kuchukuliwa kwenye benki na ikapelekwa kwenye ngazi ya Kata kwa kupitia kwenye *SACCOS* na walimu wakapata huko huko kwenye Kata kwa kupitia *SACCOS* zao.

Sisemi kwamba ni kitu ambacho kinaweza kuanza kesho lakini ukifanya utafiti unaweza kubaini *SACCOS* mbalimbali na tukaanza kujenga uwezo wa *SACCOS.* Kama sasa hivi tumeweza kuziamini kuweza kuzikopesha, nina imani kwamba zimeanza

kujenga uwezo na zinaweza kutekeleza kazi ya kuweza kulipa walimu katika ngazi hiyo na kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunaokoa muda mrefu sana wa walimu wanaoupoteza wakati wa kufuata mishahara. Kwa upande wetu sisi watu wa Mbeya Vijijini utaratibu wa kuweza kuzitumia *SACCOS* kwa ajili ya kufanya malipo ya Pareto umeanza na umefanikiwa vizuri sana, hatuna matatizo hayo. Kwa maana hiyo, inaonesha kwamba *SACCOS* zetu tukiweza kuziimarisha na tukazitumia vizuri, mishahara inaweza kufika kwa walimu bila matatizo yoyote kwenye ngazi ya Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waratibu wa Elimu za Kata wanafanya kazi kubwa ni wengi lakini wana mazingira magumu ya kazi. Kazi yao ni muhimu katika kuboresha elimu ya msingi pamoja na ya sekondari. Natumaini tunachostahili hapa kufanya ni kuweza kuwasaidia kupata nyumba za kulala pamoja na usafiri ili waweze kuendelea na kazi yao hiyo vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kidogo kuhusu shule za sekondari, sasa hivi zinajengwa na Halmashauri lakini fedha za MMES hazipitii kwenye Halmashauri, zinatoka Mkoani na zinakwenda moja kwa moja kwenye shule. Lakini vilevile walimu wa sekondari huwa hawaripoti au hawatoi taarifa kwa Viongozi wa Elimu wa Wilaya, wanawajibika kwenye ngazi ya Mkoa. Sasa tatizo linaweza kujitokeza kwa wakati huu kwa sababu shule za sekondari zinakuwa nyingi zaidi kwa maana hiyo ni kwamba nafasi ya mkoa kuweza kuzisimamia shule za sekondari inakuwa ngumu kwa kadri siku zinavyoongezeka na kadri shule za sekondari zinavyoongezeka. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuweza kuangalia utaratibu ambao unaweza kufaa katika kuzisimamia shule za sekondari na kuna sababu za kila aina za kuhakikisha kwamba uongozi wa kuzisimamia shule za sekondari unafanyika kwenye ngazi ya Halmashauri, kwa sababu sisi ndiyo wajenzi wa shule za sekondari hizo. Kwa hiyo, kama tunaweza kuzijenga basi tuweze kuziendesha na Walimu Wakuu waweze kuwajibika kwenye ngazi hiyo.

Kwa bahati nzuri, utaratibu wa fedha za *Donors* wanapitishia kwenye utaratibu wa kuweka kwenye Kapu, kwa hiyo, natumaini utaratibu ambao umekuwa ukitumika kutoa pesa kujenga shule kwenye ngazi ya MMEM, unaweza kutumika kwenye ngazi ya MMES ili kuhakikisha kwamba fedha zote zinatumika bila matatizo ya aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia nataka kusema tu kwamba, wiki mbili zilizopita Naibu Waziri alikuwa ametupatia taarifa kwamba, kuanzia mwaka 2008 kutakuwa na utaratibu wa wanafunzi kufanya mitihani, yaani wanafunzi wanaoingia kidato cha kwanza. Kwa sababu imeonekana kwamba, wanafunzi wengi wanakuwa hawana ubora wa elimu ambao unategemewa. Hili linaonesha kwamba mitihani ya darasa la saba imekuwa ikivuja na ndiyo sababu labda vijana wengi wanaweza kuingia na kujipenyeza kuwa katika shule za sekondari wakati hawana sifa za kuwa katika nafasi hiyo.

Kila nikisema kuhusu mitihani ya darasa la tisa, najaribu kufikiria je, hii mitihani itakuwa ni ya kitaifa na gharama zake zitakuwaje? Mwanafunzi anafanya mtihani darasa la saba, halafu darasa la tisa anafanya mtihani na darasa la kumi pia anafanya mtihani. Kwa hiyo, kunakuwa na mitihani mfululizo miaka mitatu, gharama zake zikoje; hivi

tatizo liko wapi? Tatizo linawezekana ni katika kuhamasisha walimu kusimamia walimu wa Shule za Msingi, inawezekana kwamba kuna matatizo katika kuwatambua, kuwalipa, kuwasimamia pamoja na kutoa motisha kwa walimu wa msingi, kiasi ambacho elimu wakati mwingine huwa inalegalega katika ngazi hiyo na wakati mwingine huwa inavuja katika ngazi hiyo.

Kwa hiyo, ninashauri labda kuwe na utafiti wa kuweza kuangalia kuna matatizo gani ya kufanya watoto wanaomaliza darasa la saba wasiwe na kiwango hicho cha elimu ambacho kinahitajika, kiasi ambacho tunalazimika wafanye mitihani wakiwa darasa la tisa. Inawezekana kwamba kufanya mtihani darasa la tisa ni suluhisho kwa muda mfupi lakini natumaini tutakuwa tunakimbia ukweli wa matatizo ambayo yapo katika Shule za Msingi katika kiwango cha kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o ajiandae na Mheshimiwa Ponsiano Damiano Nyami ajiandae.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyo mbele yetu.

Naanza kwa kuishukuru Serikali. Mimi ni Mjumbe wa Kamati inayoshughulikia Wizara hii, Serikali imesikia Kilio chetu, tumekuwa tukiiomba ijitahidi kuongeza nguvu kusaidia Wizara ya Elimu kwa sababu elimu ndiyo maisha na imeitika, naishukuru sana sana. Namshukuru zaidi kwa kweli anachacharika si weupe wa sura hata wa moyo, anatembea kila sehemu, ana hiari ya kukaa kwake na kupumzika lakini anawaita Wakuu wa Mikoa wote na *DOs* wote, anakuwa nao mpaka usiku. Kwa kweli ni kazi nzuri ambayo kama kuna ambaye hawezi ku-*appreciate* basi ana matatizo na tukubali kwamba ni lazima tufanye hivyo.

Wenzetu Kenya walianza kwa shida namna hiyo, wakaanza na harambee wakajitahidi mpaka wakafikia mahali walipo, baada ya kuona wamefanikiwa wakapumzika harambee. Sasa wenzetu wanasema wamekataza harambee, lakini wamepumzika wameshamaliza ni kwamba katika kila kilomita mbili wana shule. Kwa hiyo, wameshamaliza na walichobakiza sasa hivi ni kuchanga harambee kwa ajili ya kuangalia watoto ambao hawana uwezo wanawafanyia harambee wakati sisi tunachangia harusi. Kwa hiyo, ni kazi nzuri ambayo inafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wizara, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Viongozi wake, Naibu Wake, Katibu Mkuu na hata Wakurugenzi, kwa kweli wanafanya kazi nzuri hata ukiangalia kitabu, angalia vitabu vyote ulivyokwisha pokea, kitabu chao kimepangwa kila *topic* na rangi yake inaonesha ni walimu na *margin* ina-*indicate* kwamba, hapa *there is learning* ni walimu hawa. Vitabu vingine havina hata *margin,* kwa kweli kazi yao ni nzuri, tunajua kuna kitu hapa. Mimi

kwa kweli nilikuwa ninapata taabu sana lakini kadri ninavyoona, mimi ni mwalimu *by profession*, unaona mtoto wa shule anavyopanga kazi unasema hapa natengeneza *Professor*, kwa hiyo hawa wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja moja aliizungumza Mheshimiwa Bujibu Philip Sakila, suala la mikondo. Ni kweli kwamba, *standard* nzuri ni mikondo minne kwa darasa lakini kiuchumi na ukiangalia *Education Financing* na *Education Economics,* zinakuwa ni ya faida zaidi kuliko shule ndogo kwa sababu ni *laboratory* utajenga moja, kama viwanja vitakuwa ni vichache palepale na *Headmaster* ni mmoja bahati mbaya *headmasters* wetu hawapewi *allowances* kubwa kubwa, lakini wanataka hatuna uwezo tu. Lakini kama ingekuwa ni kujenga shule mbili mbili kila kata, kwa kweli nadhani itakuwa ni gharama kubwa na michango itakuwa ni mikubwa. Kwa hiyo, nami nina-*encourage* na kuwashauri kwamba, kama mikondo inaweza kwenda mpaka sita au hata minane, siyo mbaya. Kitu muhimu hapa ni *management*, unapunguza hata kutumia *resources* nyingi, hata kufanya *double session* bado inawezekana kwa sababu shule za *government* zilikuwa zinakwenda hivyo. Nadhani hiyo ni muhimu sana kuweza kuliangalia ili kupunguza *duplication* ya kujenga shule nyingi, gharama inakuwa kubwa mno.

Mheshimiwa Waziri nitakuwa sikutendei haki nisiposema nashukuru kwa msaada ulionipa wa kuleta gari ni wajibu wako lakini lazima nikushukuru, umenipa gari la ukaguzi, nashukuru sana.

Kuhusu kilio chetu cha MMEM angalau maboma kidogo tumepunguza lakini bado tunaomba jitahidi tena kwa sababu sisi tulijitahidi sana. Nakushukuru sana kwa kazi yako ni nzuri, najiuliza sijui ni kwa nini labda ni mzoefu wa ualimu maana mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Napenda nikushukuru kwa kuanzisha michezo, kwa kweli ni jambo zuri sana, kwa mtu ambaye haelewi umuhimu wa michezo katika kukua kwa binadamu, basi ana matatizo. Tusiletewe tena habari kwamba waraka tumeupeleka kwa Mawaziri sasa Mawaziri wasioelewa michezo hao watakuwa na matatizo. Kwa hiyo, tunataka tuone kiwanjani inafanyika. Tunakushukuru sana.

Katika kitabu chako cha hotuba umesema mmechangia mwaka 2006 yamejengwa madarasa 2,631 na nyumba za walimu 1,000. Kweli mimi kama Mjumbe wa Kamati, tulikuwa tunazunguka sehemu mbalimbali tukaona yaliyofanyika. Lakini Wilaya ya Geita ina shule 41 zote ni za kujengwa na wananchi, Jimbo langu la Busanda lina shule 14 nilikuta lina shule na sasa hivi tumefikisha shule 14, yaani kila kata ina shule. Kata moja ina shule mbili lakini Mheshimiwa Waziri nikueleze tu kwa masikitiko kwamba, katika shule zote 14 hakuna hata moja iliyopata fedha ya MMES, yaani ni *formula* ya ajabu ilifanyika kule Mkoani. Inawezekana siyo tatizo lako lakini najua fedha zilipelekwa kule sasa mtu mmoja kakurupuka katengeneza *formula* yake, pesa hizo zikaruka Jimbo langu.

Sasa Mheshimiwa Waziri naomba nisaidie kuwaeleza wananchi wangu ni nini kilitokea na nitakutajia shule ukaangalie kama kweli fedha zilipelekwa kule? Shule hizo ni Bukondo, Chiluluma, Chigunga, Nyakangomba, Katoro, Rwamgasa, Busanda, Nyarugusu, Bukoli, Kamena, Nyamalime na Nyamigota. Shule hizi hazikupata hata senti tano ya MMES, wananchi wamechangia kuku, mbuzi, wamehangaika kila kitu wamefanya na Halmashauri. Naishukuru Halmashauri ilitumia nguvu zote lakini hela ya MMES walikuwa wakiniambia nazunguka, kuna *formula* ilifanyika, sielewi. Mheshimiwa Waziri nafikiri hapa kuna tatizo na sijui kama kuna Mikoa mingine imepata tabu kama hii lakini Jimbo langu hata senti tano haikufika.

Mheshimiwa katika hili nakusudia kuondoka na hela yako, unieleze kama katika hizi zitakazokuja utanilipa na za mwaka 2006? Angalau na mimi watu wangu waende vizuri kwa kweli ni taabu. Kwetu sisi elimu ndiyo ukombozi, vinginevyo utakuwa unatutakia sisi tuendelee kuua vikongwe na wazee kwa sababu ya kukosa elimu kwamba, wazee wakizeeka sura inabadilika unafikiri kwamba ni mchawi kwa sababu macho yanakuwa ni mekundu kwa kupuliza moto na uzee. Nitaomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ni ulimwengu wa ushindani, hizi shule tunazojenga tunaomba kuwe na programu ya kuwawezesha kuona, yaani mwanga angalau wa majenereta kwenye shule. Tupate hata majenereta ili vijana wasome. Kwa sababu bila hivyo, vijana wetu watakuwa ndiyo wale wanaopata *Division III* na *IV* na hawatapata hata siku moja mkopo wa Chuo Kikuu na hawatasoma. Kwa hiyo, Chuo Kikuu kitakuwa cha wale wengine wenye nafasi nzuri. Naomba ujaribu kuangalia inawezekana shule zangu ziko kijijini zinaweza kupata angalau majenereta, tena pale kuna uwezekano wa kupeleka hata umeme watu watalipa ni eneo la wachimbaji, unaweza kupeleka kule umeme. Sasa si vyema mtoto akalale saa 12 na watu wazima nao walale saa 12. Tupate vitu kama hivi angalau watu wasome ingawa na watu wazima tunahitaji umeme ili tuweze kuzalisha zaidi na zaidi badala ya kusinzia na kuongeza *population. (Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naomba nizungumze polepole, kuna maswala ya walimu. Mimi nashindwa nimwulize nani kwani ninazo hoja nyingi sana sasa sielewi Wizara ya Elimu ninyi mnaajiri; mnasomesha; mnasajiri walimu; mnatoa pensheni; mnahamasisha; mnaadhibu au mnafanya nini? Maana ziko Wizara nne hapa. Maana yake sielewi wewe tukutume nini, inaniwia vigumu kueleza matatizo labda naweka kidole kwa mtu ambaye hahusiki. Wakati wa sherehe tulimwomba Mheshimiwa Rais kwamba, chombo cha walimu ni muhimu, kwa sababu idadi ya walimu kwanza imeshakuwa kubwa ina zaidi ya watumishi 50%. Tufanye kama wenzetu Kenya wanavyofanya. Kenya baada ya kuona idadi ya walimu ni kubwa sana wakawapa chombo chao, yaani *Teachers Services Commission*. Chombo chao ndicho kinachoajiri, kinaangalia, kinasajiri, kinatoa adhabu na mambo mengine kwa hiyo, kinawajibika moja kwa moja kwa mwalimu. Sasa kwetu sisi inakuwa ni vigumu mwalimu atasaidiwa vipi?

Inanikumbusha mwaka 2004 ulitokea mgogoro wa namna hii, nilikwenda kwa Waziri wa Serikali za Mitaa kuhusu matatizo ya walimu wa shule za msingi. Tulipomwendea alituambia fedha zinatoka Wizara ya Elimu kwani mimi nina

Mkurugenzi wa Wizara ya Elimu hapa. Tukaenda Temeke tukakutana na Waziri wa Elimu tukamweleza, akatuambia kuwa masuala haya yako kwa Waziri wa Serikali za Mitaa, tukasema hapana. Mwenyekiti wangu Kwankabara akasema uongo, atanituhumu hapa, tukasema hapana tujikusanye tukapelekana mpaka kwa Waziri Mkuu, maswali maswali tume ikaundwa na walimu wakalipwa. Sasa hatutaki tufike huko, tunaomba wakati wa ku-*wind up*, utuambie chombo cha walimu kitusaidie.

*Kenya Teachers Services Commission* ndiyo inayoajiri hata kama anakuja mgeni ni lazima aripoti pale, hata *private schools.* Ndiyo ina-*regulate* kwamba huyu anastahili kufundisha watoto wetu, sisi *private schools* zinajichukulia maamuzi hata unaweza ukatuambia *private schools* ni zipi zenye walimu wanaofaa na wasiofaa? Lakini kama kuna chombo wanaripoti pale wanasema ruksa kwenda kufundisha. Sasa sisi yeyote yule ruksa kwa sababu hakuna chombo kinacho *control.* Kwa hiyo, naomba sana katika hili, hebu tusaidie tupate uhakika, chombo hiki kinafanyiwa kazi au hakuna? Lakini nadhani sina sababu ya kukusamehe, wewe ulikuwa Rais wa Chama cha Walimu na mimi nilikuwa Mdhamini, unafahamu lakini sasa inawezekana unafanya makusudi. Kwa kuwa unafanya makusudi, mimi naondoka na shilingi leo nitaenda nayo kwenye hoteli yangu utakuja labda kama utanielezea huku au hapa lakini unieleze hiki Chama cha Walimu kinapatina vipi? Chombo kimoja cha walimu. Kwa sababu, siwezi kusema nikufundishe, wewe unajua kuliko mimi na ulikuwa unanifundisha; sasa umetugeuka au namna gani?

Kwa kweli kuna mambo mengi ukikutana na walimu wanatueleza, kuna takwimu ambazo nyingine zinachanganya kwa mfano, Utumishi wanasema kuna walimu 38 ndiyo hawajapandishwa madaraja, lakini malalamiko yaliyoko Chama cha Walimu na Walimu 72,000 hawajapandishwa madaraja; hao wengine wamepotelea wapi? Ukiwauliza *TSG* hawajui ni lini watapata *promotion*, jamani turejee Tume ya Makwetta, Sheria Namba 1 ya mwaka 1989, ilikuwa inaeleza vizuri baadhi ya mambo mengine mazuri tuyachukue.

Hata tusiende mbali, hapa Dodoma kuna walimu 1,800 wanatakiwa wapate *promotion* lakini Serikali inakusudia walimu 500 ndiyo watapata *promotion* wengine namna gani? Sasa inaonesha kwamba, kuna mchanganyiko. Tukubali tuige mambo mengine mazuri ya wenzetu. Naomba sana tafadhali kwa kuwa muda utakuruhusu, hizo Wizara sasa mimi nashindwa kueleza sijui nitakuuliza wewe halafu utawa-*consult* wenzako wale wane, yaani Waziri wa Fedha na wengine, watueleze kuna ugumu gani kuwapa chombo chao?

Chombo hiki ndiyo tungekiambia kama kina madhaifu kitusaidie hata *promotions* kinaweza kikatusaidia, siyo kuwakimbizia walimu tu. Walimu ni watu *complex* huwezi kusema utaweka kwenye *OPRAS, OPRAS* ina-*operate* kwenye viwanda ambapo unaweza ukahesabu ndoo ngapi zimetolewa, *cement* mifuko mingapi, magunia mangapi, unajua kwamba, huyu amezalisha. Sasa mwalimu utaangalia *turnover* ya wanafunzi kupitia pale shuleni kama hawashindi inawezekana mtihani umetungwa vibaya, mazingira ni mabaya, nyumba hana, usafiri hana na kuna vitu vingi hata hii 117 ilikuwa inafaa. Sasa nasema tukae pamoja tujadili *promotion* zao.

Mimi nina wasiwasi hivi vitu tuviangalie, ninashauri sana na ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, Chombo cha Walimu hebu kiangalie tuone nacho kitatusaidia nini kuliko kufanya mambo jumla jumla, tunashindwa hata matatizo ya walimu tuyaeleze vipi.

Hiyo shilingi naondoka nayo, kazi yenu mnayofanya ni nzuri, naomba vilevile wale wanaokula hela za kipindi kilichopita, sikuwepo nilikuwa naumwa lakini Waziri Mkuu alizungumza sana, wanaokula hela za MMES. Kwangu kuna watu wamekula, ingawa wameniambia lakini mimi nasema wamekula hela zile, wafanyiwe kazi, mtu yeyote anayekula hela ya umma ashughulikiwe.

Ahsante sana, nadhani Serikali imeshachukua hatua, washughulikiwe hao ni wezi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana hiyo ni kengele yako ya pili. Usiwatishe Waheshimiwa Wabunge, hela unayochukua ni ya kwako tu hakuna ya Serikali maana hakuna utaratibu huo. Kwa hiyo, nenda na shilingi yako mwenyewe siyo ya Wizara hii. Tunaendelea na Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o na Mheshimiwa Shellukindo ajiandae.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami ya kuchangia Wizara ya Elimu na Ufundi.

Napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Mawaziri wote wawili, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na watendaji wote wa Wizara hii muhimu kwetu. *(Makofi)*

Napenda pia niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kazi nzuri waliyoifanya hasa ya kuboresha elimu na kwa hiki tunachosema mapinduzi au mageuzi katika elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tutakuwa hatuna macho na tutakuwa hatukuwatendea haki Watanzania kama hatutakubali kwamba, kwa kweli kuna mageuzi makubwa katika Elimu. Sisi wengi tumezaliwa vijijini, tunaelewa kabisa watoto wengi walikuwa hawaingii darasa la kwanza kwa umri unaotakiwa. Mtoto amefikia umri wa kuanza darasa la kwanza, lakini kwa vile hakuna shule mtoto anabaki mpaka umri ule unazidi. Sasa Serikali imefanya mageuzi makubwa, kila mtoto mwenye umri wa kuanza darasa la kwanza anakwenda shule kwa sababu nafasi zipo; hivi hayo siyo mageuzi makubwa kweli?

Halafu tunaanza kuyabeza, kama kweli tumewania kwamba tunataka kuleta mageuzi ya elimu na kuondokana na umaskini, lazima kwanza elimu iwe ni mkazo wa kutiliwa umuhimu na ndiyo hiyo Serikali ya Awamu ya Nne imefanya. Tunaipongeza sana kazi hii, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Wabunge, Madiwani na Wananchi wote, waliofanya kazi kubwa hii ya kuongeza shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia suala la hosteli sitalizungumzia sana kwa sababu wenzangu wameshalizungumza na tunaelewa kabisa ni tatizo kubwa sana na

hasa kwa watoto wa kike wanaotoka mbali na pia shule nyingi zimejengwa mbali na vijiji. Kwa vile imekuwa ni shule ya Kata basi linatafutwa eneo katikati tena wakati mwingine siyo jirani na kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri pia kuna umuhimu wa kuangalia kama ni katikati ya Kata, basi tutafute kijiji kilichopo jirani ndiyo shule ijengwe. Shule inajengwa peke yake imejitenga. Hata likitokea tatizo wanakuwa hawana walimu, hawana mahali pa jirani pa kukimbilia na kunakuwa hakuna usafiri. Hebu tuangalie pia maeneo ya kujenga hizi shule pawe ni jirani na vijiji, ndiyo katikati ya Kata lakini pawe ni mahali ambapo ni jirani na kijiji ili tatizo likitokea kuwe na mahali pa kupata msaada wa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shule za *boarding*. Shule hizi nyingi hazina usafiri, ziko mbali, zinapopata matatizo kama ya wanafunzi kuugua kunakuwa hakuna usafiri wa kuweza kuwahudumia. Nafikiri hili pia Wizara iliangalie ili kuhakikisha kwamba zile shule zinakuwa na usafiri wa uhakika ili kuhudumia watoto pindi yanapotokea matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia suala la ujenzi wa nyumba za walimu. Limeshazungumzwa sana kwamba, ujenzi wa shule za sekondari uendane na ujenzi wa nyumba za walimu ili walimu waweze kuwa na mahali pazuri pa kuishi kwa sababu pia inawapa motisha ya kufanya kazi. Kama mwalimu atakuwa anakaa kwenye nyumba ambayo haina tofauti na ile ya kawaida, hapati moyo wa kufanya kazi.

Hata usiku hana mahali pa kuweza kufanyia kazi, kwa hiyo, inakuwa ni vigumu sana kupenda kazi hii ya ualimu na mwishoni inaonekana kama ni adhabu. Nafikiri kama tutajenga nyumba huko tunakofungua shule, itawapa motisha walimu kuweza kufanya kazi hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ujenzi wa shule, naomba pia nizungumzie suala la maji ya kunywa kwa watoto wa shule. Shule nyingi zimejengwa bila kuangalia kama hawa watoto wanahitaji maji. Mimi nakumbuka shule tulizosoma zamani zilikuwa na matenki ya maji. Nafikiri Wizara iangalie ramani zinazotolewa basi ziwe na ujenzi wa matenki hata kama ni mitungi ile mikubwa, watoto wawe wanapata maji safi ya kunywa, kwa sababu watoto saa nyingine wanachota maji kwenye madimbwi, inakuwa shida na kuleta magonjwa mbalimbali. Kwa hiyo ni muhimu sana kuangalia suala la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine naomba sana, tena naomba kabisa Mheshimiwa Waziri bahati nzuri ni mama, aangalie mahitaji muhimu ya watoto wa shule za msingi, watoto wa kike wa darasa la tano mpaka la saba. Wana mahitaji muhimu, nikisema hivyo ananielewa. Mahitaji muhimu kwamba pesa zinazotengwa za kupelekwa shuleni ziangalie pia taulo za usafi kwa watoto hawa. Watoto wengine wameacha shule, lakini hatutafuti sababu kwa nini hawa watoto wa kike wenye umri wa kuvunja ungo wanaacha shule. Wanaacha shule kwa sababu wanaona aibu kwa wenzao, hawana vifaa vya kujihifadhi. Sasa mama naomba kabisa hili nalo liwe katika mageuzi ya elimu. Watoto wa kike wenye umri huo waangaliwe na mahitaji yao muhimu kabisa na vyoo

vyao pia viangaliwe.  Nafikiri mama hilo utalitilia maanani sana, unajua maana yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la chakula mashuleni. Napongeza juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kuhakikisha kwamba, kunakuwa na vyakula mashuleni kwenye baadhi ya Mikoa kama Singida kwa kushirikiana na Mpango wa Chakula Duniani.  Matokeo yake yameonesha kwamba watoto wa shule wakipewa chakula wanasoma vizuri na matokeo yanakuwa mazuri.  Sasa mimi naona kwamba sasa hivi huu mpango ungesambazwa katika shule zote.  Nakumbuka sisi tulipokuwa tunasoma shule enzi zile, tulikuwa tunakwenda na chakula, kila mwanafunzi alikuwa anakwenda na chakula chake shuleni na kwa kweli kila mwanafunzi aliweza kusoma vizuri.  Kama watoto hawapati chakula na nyumbani pia hawapati chakula cha kutosha, wanasinzia darasani, hawasikilizi.

Kwa hiyo, suala la chakula nafikiri linahitaji kuundiwa Mkakati Maalum. Naomba Wizara iangalie jinsi ambavyo inaweza kujipanga kuhakikisha kwamba shule zinakuwa na chakula na maeneo ambayo yana chakula basi uanzishwe utaratibu wa watoto kwenda na chakula mashuleni na vijiji ambavyo havina chakula, Serikali itafute utaratibu wa kuweza kusaidia Wilaya ambazo zina mazingira magumu na upungufu wa chakula.  Hii itakuwa imeendana na mageuzi ya elimu ambayo tunayazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie adhabu zinazotolewa mashuleni na walimu hasa kwenye shule za msingi.  Sielewi walimu ambao wanawapa watoto adhabu zikiwemo za viboko mpaka watoto wengine wanapewa adhabu, wanalazwa mpaka hospitalini sijui hao walimu wamechukuliwa hatua gani?  Tuna mfano uliotokea Singida, watoto walitembea katika kokoto mpaka wakalazwa hospitalini na hii ni mifano michache sijui Wizara inachukua hatua gani ili kuwa fundisho kwa walimu ambao wanatoa adhabu za aina hii?  Wanakiuka haki za watoto kwa sababu hawa watoto hawana cha kujitetea na sina uhakika kama wamewalipa wazazi waliolala mahospitalini, wengi wao wakiwa akinamama wamelala wodini kuuguza hao watoto.  Mimi napenda nifahamu hatua zipi zilizochukuliwa kwa walimu ambao wanakiuka haki za watoto, wanawapa watoto adhabu kali namna hiyo ambazo zinawaletea mpaka ulemavu.  Wizara imechukua hatua gani ambazo ni mfano kwa walimu wengine wasiweze kufanya hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la mimba mashuleni kwa watoto wa kike.  Suala la mimba mashuleni kwa watoto wa kike wenzangu wamelizungumzia sana. Ni tatizo kubwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ziara zake amelizungumza sana. Naomba nimpongeze sana kwa kulizungumzia kwa nguvu zote.  Sasa tatizo mtoto wa kike anaachishwa shule kwa sababu yeye amekuwa mjamzito, mtoto wa kiume anaendelea na shule.  *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Sema, sema!

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Naibu Spika, mtu mzima baba aliyempa mtoto mimba na kumwambia usiseme anaendelea na shughuli zake kama

kawaida. Sana sana kunakuwa na makubaliano kama nitamsaidia, nitamtunza huyu mtoto lakini baadaye anamruka. Sasa nafikiri tuna kazi ya kuamua kama kweli huyu mtoto amepata mimba katika mazingira ya kutatanisha, basi apewe nafasi ya kurudi shuleni kwa sababu hawezi kukaa nyumbani wakati yule wa kiume anasoma. Mimi nafikiri hatutafikia nafasi tunazozingumza, hamsini kwa hamsini kwenye uongozi kama wasichana watakuwa wanarudi nyumbani kwa sababu ya kupewa ujauzito na watoto wengine wamebakwa na wengine wanaishi katika mazingira magumu, wamejikuta katika matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara iliangalie hili, Serikali iliangalie na watoto hawa waweze kuchunguzwa, wale waliopata mimba katika mazingira ya kutatanisha wapewe nafasi wakishajifungua, wanyonyeshe watoto wao, warudi shuleni. Wale waliopata kwa uzembe, hiyo ni sababu nyingine ila wale waliopata kwenye mazingira ya kutatanisha warudi shuleni wapate elimu, ile ni haki yao na wale waliohusika wachukuliwe hatua kubwa. Kama ni wafanyakazi basi nao waachishwe kazi, kwa sababu yule kaachishwa shule na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nizungumzie ujenzi wa shule za sekondari za kidato cha tano na sita. Kuna Wilaya nyingine hazina shule hizi. Kwa mfano, Wilaya ya Makete haina shule ya kidato cha tano na cha sita. Sasa napenda kutoa wito kwamba, pamoja na shule hizi kujengwa zingekuwepo pia kwenye Wilaya kwa sababu sasa tuna shule nyingi angalau shule moja ya wasichana kwenye Wilaya ambayo watoto wanaweza kulala ya kidato cha kwanza mpaka cha sita itasaidia sana wasichana kuweza kukaa pamoja na kubadilishana mawazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie walimu wanaofundisha watoto wenye ulemavu. Wenzangu wameshazungumzia, lakini nafikiri pia wanahitaji kupewa motisha kwa sababu nao wanafanya kazi ngumu na ni muhimu kwamba tuwaangalie wapate mafunzo zaidi, lakini pia motisha ya kufanya kazi ngumu ya kuweza kufanya hawa watoto mpaka waweze kuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ili kengele ya pili isije kunikuta, naomba kusema kwamba, naunga mkono hoja hii asilimia mia na naipongeza Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri inayofanya na tutakuwa tayari kuendelea kusaidiana nayo kufanikisha lengo la kuhakikisha kwamba, watoto wote wanapata elimu katika nchi hii na yule anayebeza maendeleo haya, atakuwa na choyo na nina uhakika kwamba hata watu hawawezi kumwelewa kama atabeza kazi kubwa hii iliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango wangu kidogo lakini umenistukiza. Sasa kuna Wabunge wengine hapa wameniambia wewe ni *Senator* utazungumza tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, wasaidizi wake; Manaibu Waziri wawili na watendaji wake wakuu; Katibu Mkuu na Afisa Elimu Mkuu, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Mimi wakati tunagawiwa kitabu nilikuwa na wasiwasi nikasema kitabu hiki kina kurasa zaidi ya sabini hivi Mheshimiwa Waziri atakimaliza. Lakini ule ufupisho alioufanya pale nilivyoangalia mimi umechukua mambo yote. Kwa hiyo, nampongeza sana. Huyu ni mwalimu hasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaniwia radhi kidogo, kuna jambo moja nimelisoma jana katika magazeti mawili, nimeshindwa kulinyamazia tu, nizungumze halafu niliache tu. Mtanzania ya Jumapili 8 Julai, 2007 limekuwa na kifungu kimoja kimesema: "Wabunge kujibu hoja za Wabunge wenzao au kutetea Serikali." Halafu Gazeti la Tanzania Daima la tarehe hiyo hiyo, limesema: " Bunge laanza kupoteza maana." Sasa nataka kusema hivi, mimi hapa ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, ni Wakili wa Chama cha Mapinduzi na Sera za Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, ni wajibu wangu kama sera hizo zinachezewa chezewa siwezi kunyamaza, lazima nitajibu. Sasa lazima tutofautishe hiyo. Lakini kama Mbunge anazungumza habari zake za Jimbo, sasa mimi nitamjibu nini. Lakini unapogusa sera na sisi tunanyamaza haiji, hata ile *Parliamentary Democracy* inakuwa haipo. Kwa hiyo, naomba sana wenzangu Wabunge, tupambanue mambo haya mawili. Kama unakosoa sera ina tofauti, kama unakosoa utekelezaji wa Waziri hayo ni ya kwako, lakini ukichanganya kwamba hakuna chochote kilichofanywa na mimi najua sera hizo zinafanya kazi, hatutakaa kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoa ufafanuzi sio kutetea. Serikali iliyopo hapa ni ya Chama cha Mapinduzi na mimi ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, ndiyo Serikali yangu ninayoijua. Sasa kama kuna jambo halieleweki vizuri na la kisera nitalieleza, kwa hiyo watu wa magazeti watuelewe, kuna taratibu zake humu ndani. Kazi yetu ni kusimamia na kuishauri Serikali. Sasa kushauri na kusimamia kuna taratibu zake hatukuja hapa kupigana ngumi, kuhukumu, kama tatizo limetokea, tunasema hili likatazamwe na tuletewe taarifa. Kama ni mtu wa kupelekwa Mahakamani atakwenda kuhukumiwa Mahakamani. Sasa isifike mahali hapa pakawa ni mahali pa kutoa hukumu kwa utendaji ambao unahitaji utazamwe na vyombo vingine. Kwa hiyo, naomba wenzangu Wabunge haya tusiyakubali. Kama Mbunge anatumia lugha safi, hawezi kupata tatizo lakini kama anatumia lugha ya kuudhi basi ategemee na mapigo vilevile yatakuwa ya kuudhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotaka hapa Bungeni ni *Constructive Opposition*, Upinzani Jenzi, siyo Upinzani wa hivi hivi. Wapo *senators* wengi sana, Mheshimiwa John Cheyo anaelewa hilo. Upinzani Jenzi, hili neno jenzi nimelitoa katika Kamusi mpya ya mwaka 2006, *Constructive Opposition* (Upinzani Jenzi). Nashukuru sana kwa kupata nafasi nifafanue hayo mambo mawili yaliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu elimu, napenda sana kuipongeza Serikali, Wizara ya Elimu na kwa upande wangu wananchi wa Jimbo la Bumbuli. Imefanyika kazi nzuri sana ya kuendeleza elimu ya sekondari. Nikitoa mfano wa Jimbo jipya la

Bumbuli lililoanzishwa mwaka 1995 wakati linaanzishwa tulikuwa tunaambiwa Lushoto kuna shule nyingi, lakini tumekuja kugundua kwamba, shule hizo zote zipo katika eneo moja la Lushoto.  Ukitaja Kifungilo, Mazinde Juu, Kongei ziko katika eneo moja, Bumbuli kulikuwa hakuna shule hata moja ya sekondari.  Kuna Kata kumi na mbili na sasa hivi kuna shule kumi na sita za sekondari. Kwa hiyo, kila Kata ina shule na Kata nne zina shule mbili mbili na wanaendelea.  Kwa hiyo, napenda kuipongeza sana Serikali na Chama cha Mapinduzi kwa sera hizi sahihi za elimu ya sekondari.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka tu kueleza kwamba, tunakwenda huko lakini tunatazamia nini kwa wanafunzi hawa wanaotoka vidato vya nne, sita, chuo kikuu, tunawaandaa kweli kwenda kujiajiri maana ajira hakuna.  Kwa sababu kila anayesoma anataka kuajiriwa, sasa tajiri wa kuajiri yuko wapi?  Naona kuna haja ya kuangalia mfumo wetu wa elimu tena.  Hapa tulipofika nadhani tufanye mambo mengine, kunahitajika elimu nyingine ya kazi.  Hii elimu ya kumfungua mtu itamsaidia.  Nilikuwa nasoma kitabu kimoja kimeandikwa na Bwana Robert Kayasoki, kimeandikwa *Rich Daddy and Poor Daddy*, Baba Tajiri na Baba Maskini.  Baba Tajiri anamwambia mtoto wake nenda shule ukasome uje tufungue kampuni, tuiendeshe vizuri, wewe uwe maneja wa kampuni hiyo, kasome uje ufanye hiyo kazi.  Baba Maskini anamwambia mtoto wake, nenda ukasome, uje uajiriwe upate mshahara mzuri.  Ndiyo, kuna tofauti hapo na ndiyo tunavyofanya.  *Get good grade* upate *promotion,* upate mshahara mzuri wa kuajiriwa, lakini siyo wewe mwenyewe kujiajiri.  Sasa ikiwa wote tunategemea kuajiriwa nani atajenga ajira.  Kuna haja ya kutazama sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru sana Wizara ya Elimu, imetoa mwelekeo huu wa kwenda kujenga shule za ufundi kwenye Wilaya.  Nadhani hili neno la ufundi linapotosha kidogo, kwa sababu *vocational education* siyo elimu ya ufundi, si ndiyo ninyi mnaojua Kiingereza, ni elimu ya kazi.  Sasa *vocational education* hii kwa mfano Lushoto pale nimkute mzee ambaye analima kabichi amwambie kijana wake, nenda ukachukue masomo ya kilimo uje tulime vizuri zaidi tujenge kampuni ya *Mboga Limited* tuuze zaidi.  Hiyo itasaidia zaidi.  Kwa hiyo, kuna haja ya kulitazama hilo.

Halikadhalika watu wengine kwenye maeneo ya korosho wafanya hivyo.  Kwa sababu kila mtu sasa hivi anakwenda shule akitegemea kuajiriwa.  Kwa kweli kwa mtindo wetu wa elimu ni kumjenga mtu akaajiriwe, hakuna ambaye anasema nitatoka huko niende nikaanzishe ajira, nianzishe kampuni, niajiri watu wengine, kila mtu anataka kuajiriwa, kwa hiyo tuna tatizo kubwa sana.

Wanakwenda watu wengi mpaka sekondari wenzangu Waheshimiwa Wabunge walisema tusomeshe watoto mpaka Chuo Kikuu sawa, lakini unataka wakafanye nini. Kwa hiyo, hata mitaala nadhani tuitazame, kama kuna watu wanachukua *academics* kama zilivyo kwa kufundisha Chuo Kikii lakini tunataka watu wa kwenda kujifanyia kazi wenyewe ili wajenge uchumi. Nilikuwa na haya ya kusema, yananipa wasiwasi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale vijana waliomaliza kidato cha sita wasiokwenda Chuo Kikuu wataajiriwa wapi, ajira ziko wapi, zimeshajaa labda watu wafe au wengine wafukuzwe kazi ndiyo kunatokea nafasi na kuna haja ya kuitazama hiyo kwa kweli.

Hatusemi Wizara ya Elimu bali ni nchi kwa ujumla, tutazame mwelekeo huo. Kama ni kufungua vyuo vya mafunzo ya kazi kwa sababu *vocational training* ukiitazama kwa sasa ilivyotafsiriwa mafunzo ya ufundi, wanadhani ni *carpentry, mechanical* na *electrical, technicians* kumbe sivyo, unaweza kufundisha mambo yote, *hotel management* yanafanyika hayo. Sasa tutazame kitu ambacho tutakipanua kuweza kuangalia uchumi wa nchi unahitaji wataalam wa namna gani. Kwa hiyo, vyuo hivi vielekezwe katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu naipongeza kwa azma yao ya kutoa kipaumbele kwenye ajira ya walimu. Wananchi wapo tayari wanajenga shule, sasa walimu nao tujitahidi wapatikane wa kutosha. Napenda kuipongeza Wizara kwa kuanzisha Kada ya Waratibu wa Elimu ya Sekondari, tunawahitaji sana. Kama walivyosema Wabunge wengine, hakuna kiungo pale na halafu ninavyojua mimi hawa watumishi wa Serikali *(Civil Servants)* kama katika barua yake ya ajira wewe huonekani basi huwajibiki kwake. Kwa hiyo, yeye anawajibika kwa Katibu Mkuu wa Elimu, lakini utafutwe utaratibu ambao wangewajibika mahali pale katika Wilaya. Kwa mfano, wale Waratibu sasa watahitajika sana wapewe nyenzo hasa usafiri ili waweze kufika kwenye shule za sekondari hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya *headmasters* hawakai kwenye shule zao, sijui kwa wenzangu, lakini mimi nina mfano wa shule yangu ya Sekondari inaitwa Fumta. Nimeletewa hii taarifa mara nyingi sana kwamba, *headmaster* haonekani anatoa kisingizio anakwenda Tanga kupata mwelekeo sijui wa nini. Mambo namna hii ni kwa sababu hakuna kiungo hapa karibu na napenda nimshauri Waziri wa Elimu aitazame hiyo kwa sababu yule ni mfano mbaya wa nidhamu kwa sababu pale anaacha walimu wenzake tu, tena wadogo, yeye ambaye angewaongoza anakaa mwezi mzima au miezi miwili haonekani. Sasa Mbunge ukisema unaambiwa wanaleta siasa hawa. Tuweke huo utaratibu. Sisi tutatoa taarifa kwa huyo Mratibu, kwamba mwalimu wake analalamikiwa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa shule hasa za sekondari. Huu ungeimarishwa kwa sababu nina hakika katika shule zangu zilizoanzishwa, nadhani ni chache sana ambazo zimekaguliwa. Sasa shule kwa kweli kupita mwaka mmoja bila kukaguliwa si vizuri. Nimeona katika taarifa yako Mheshimiwa Waziri, katika shule za msingi zimeweza kukaguliwa asilimia sabini, sekondari asilimia sitini na sita, lakini kwa mwaka wa fedha 2007/2008, mnatazamia kukagua zote.

Tutaunga mkono kwenye hilo na naomba wale Wakaguzi wajitahidi kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ili wanapokwama kwa usafiri waweze kupata msaada na sisi tutajitahidi kwenye Halmashauri tusaidie Wakaguzi hao ili watusaidie kurekebisha matatizo ambayo kama yakiachwa yanaweza kuharibu kabisa elimu ambayo tunaitoa katika shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa muda huu na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ambayo naiita ni ya upendeleo, kwa sababu mara ya kwanza uliponiita nilikuwa Mtera kwa maana ya kutokuwepo hapa, nasema asante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijiunge na wenzangu kutoa pole kwa Wabunge wote, ndugu na wale wote ambao walipata pigo kwa vifo vya Marehemu Juma Akukweti na Marehemu Amina Chifupa Mpakanjia, ambavyo kwa kweli vimetugusa sana sisi sote kama Wabunge na tunamwomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia najiunga na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa hotuba nzuri sana aliyoitoa hapa leo asubuhi. Lakini pia nawapongeza Manaibu Waziri na wale wote waliohusika katika matayarisho ya hotuba hii. Ilikuwa ni hotuba iliyogusa kila eneo na pia ni hotuba ambayo imeelezea kwa kina sana, kazi ambayo wenzetu hawa wameifanya katika mwaka uliopita na hotuba ambayo inatupatia matumaini makubwa kwamba, kasi hii ambayo wameanza nayo wataiendeleza katika kipindi kijacho.

Naomba kama wenzangu wa Chama cha Mapinduzi, nifikishe pongezi zangu kwa Chama changu na Serikali yake ya Awamu ya Nne, kwa kazi kubwa sana waliyoifanya katika ujenzi wa shule za sekondari. Kwa wakazi wa maeneo kama yale ambayo mimi natoka kwa maana ya Dodoma, mabadiliko ambayo yameletwa na ujenzi wa shule hizi na madarasa haya ambayo yameongeza wigo wa shule za sekondari kwa kweli yameleta tofauti kubwa sana kwetu.

Katika kufanikisha kazi hii ningependa kutoa pongezi maalum kwa Mkuu wetu wa Mkoa, Mheshimiwa William V. Lukuvi na pia Mkuu wa Wilaya ya Dodoma Mjini, Mheshimiwa Tupa, ambao walisimamia kidete kabisa shughuli zote za kuhakikisha kwamba hizi shule zinajengwa na hata kufanikisha lile lengo la kusajili watoto asilimia mia kwa mia wale wote ambao walifaulu mtihani wa darasa la saba mwaka jana. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawapongeza sana wananchi wa Jimbo langu la Dodoma Mjini, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika ujenzi huu wa shule. Huu ulikuwa wakati mgumu sana kwao kwa sababu mwaka 2006 ulikuwa ni mwaka mbaya sana kwa masuala ya chakula, kulikuwa na njaa kubwa sana lakini pamoja na matatizo hayo walisimama kidete, tukashirikiana na tukakamilisha hiyo kazi ambayo ilikuwa mbele yetu.

Nasema nawashukuru sana, nawapa pongezi na nina matumaini kwamba, hawatachoka kwa sababu kazi iliyopo mbele yetu bado ni kubwa lakini nina imani kutokana na ushirikiano wao, mambo yatakuwa ni mazuri tu. Pia naomba niwapongeze wanafunzi waliofanya mtihani wa darasa la saba katika Jimbo langu la Dodoma Mjini, lakini pia walijiunga na wenzao katika Mkoa huu wa Dodoma kwa sababu walifanya kazi nzuri wakafaulu.

Katika mlolongo wa Kitaifa, Mkoa huu ulikuwa wa tatu katika Mikoa bora katika ile mitihani. Nawapa pongezi sana wanafunzi hao, walimu wao pamoja na wazazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Waziri anasoma hotuba yake alizungumzia azma yao ya kufanya mapitio ya mpango mzima wa MMES kwa kipindi kijacho. Bila shaka lengo kuu ni kuhakikisha kwamba, huu mpango unaendana na kasi mpya katika ujenzi wa shule za sekondari ili tusije tukajikuta vijana wanaomaliza kidato cha nne wanakuwa ni wengi mno, kiasi cha kukosa nafasi za kuendelea pale ambapo watakuwa wamefuzu.

Kwa hiyo, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na wenzake huko Wizarani kwa kazi hii ambayo wanatarajia kuifanya na bila shaka wataifanya kama vile ambavyo wameshazifanya zile kazi nyingine huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu hautakuwa mrefu sana na utajikita zaidi kwenye ombi maalum, ambalo naomba kulielekeza kwenye Wizara hii lakini pia kwenye Serikali.

Ombi lenyewe ni kwamba, Mkoa wetu wa Dodoma na hususan Wilaya yangu ya Dodoma Mjini, kwa miaka iliyopita ya huko nyuma pamoja na kwamba tulikuwa na shule za sekondari za Serikali, si wanafunzi wengi ambao walikuwa wanapata nafasi ya kupenya na kupata elimu ya juu.

Sababu zilikuwa nyingi mojawapo ni kwamba, shule za kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne zilikuwa ni chache sana ukilinganisha na mikoa mingine. Mikoa mingine wenzetu walikuwa na bahati shule za watu binafsi zilikuwa nyingi na zilisaidia katika kuleta maendeleo katika elimu ya watu.

Hapa kwetu sisi hali ilikuwa tofauti na matokeo ya ufinyu huo wa nafasi za elimu umejidhihirisha sana sana kawa vijana wanaotoka eneo hili, ambao walipata nafasi ya kwenda vyuo vikuu au vyuo vingine vya elimu ya juu kiasi kwamba, ukilinganisha na idadi ya watu, baadhi ya wakazi wa Mkoa huu na Wilaya hii ni wachache sana hasa ukiangalia mikoa mingine ambayo kielimu wamepiga hatua siku nyingi.

Ombi maalum ni kwamba, katika kupitia Mpango huu wa MMES katika kupitia tufanye nini ili kupanua nafasi za kidato cha tano na cha sita ambayo ndiyo ngazi kuu tunapoelekea kwenye Chuo Kikuu au kwenye Vyuo Vikuu na elimu ya juu. Tuipatie ile mikoa ambayo kwa siku za nyuma ilikuwa na nafasi chache, tuipe upendeleo maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, upendeleo kama huu hautakuwa kitu kigeni kwa sababu kama unavyojua tumeshalizungumzia hili suala kwenye masuala ya uchumi na masuala ya kuhakikisha kwamba tunaelekeza nguvu zetu kujenga miundombinu na mazingira mazuri kwenye mikoa ile ambayo ipo pembezoni ili wasije wakaachwa nyuma kiasi kwamba mambo yakawa siyo sahihi kwa sababu nchi ni moja, ni vizuri tuendane.

Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba katika kupanua elimu ya kidato cha tano na cha sita, hii mikoa ambayo ilikuwa *disadvantaged,* tuipatie au tuiangalie kwa jicho la huruma ili nao angalau wapige hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu ni hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia hauwezi kutosha mchangiaji mwingine, kwa hiyo, naomba niwashukuru sana kwa kazi tuliyoifanya pamoja leo.

Waheshimiwa Wabunge, mmechangia vizuri, lakini kama alivyoeleza Mheshimiwa William Shellukindo, tunapojadili hapa mradi hututukani mtu, kama unajua jambo vizuri zaidi kuliko mwingine aliyesema, kanuni zinaturuhusu kuweza kuchangia kwa maana ya ufafanuzi. Kanuni zetu zinaruhusu, mradi humshambulii Mbunge wala humtukani ila unajenga hoja ya lile alilosema. Kwa hiyo, magazeti hayakuwa sahihi kusema kwamba Wabunge wengine wanawajibu wenzao, hapana. Kama kuna Mbunge anayejua jambo fulani zaidi kuliko mwingine, anaweza kujibu kama alivyofanya Mheshimiwa Rita L. Mlaki, hakuwa anajibu kwa niaba ya Waziri Mkuu, alikuwa anajibu kwa sababu ni Mbunge wa Kinondoni, anajua kinachofanyika, ila usimshambulie Mbunge mwenzio.

Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa siku ya leo, naomba niahirishe kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.34 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 10 Julai, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*